# MADA : "MAUDHUI KATIKA USHAIRI WA M.M. AMIR."

NA : MUAKA LEONARD LISANZA.

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA " MASTER OF ARTS " KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

1993.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146591 3

EAST AFRICANA COLLECTION
UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

UNGAMO .

" Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote "

Muaka Leonard Lisanza.

(Mtahiniwa)

" Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa Idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu "

Ndg. Kithaka Wa Mberia.

Ndg. Mungai Mutonya.

YALIYOMO UKURASA

Ungamo................................ (i)
Yaliyomo................................ (iii)
Tabaruku................................ (iv)
Shukrani................................ (vi)
Muhtasari................................ (vii)

SURA YA KWANZA.

1:1:0 Utangulizi................................ 1
1:2:0 Somo la utafiti................................ 2
1:3:0 Madhumuni................................ 3
1:4:0 Sababu za kulichagua somo hili................ 4
1:5:0 Upeo na mipaka................................ 5
1:6:0 Haipothesia................................ 6
1:7:0 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili................ 7
1:8:0 Msingi wa kinadharia................................ 8
1:9:0 Njia za utafiti................................ 12
Tanbihi................................ 12

SURA YA PILI.

2:1:0 Utangulizi................................ 13
2:2:0 Kuhusu M.M. Amir................................ 14
2:2:1 Baadhi ya wanamapokeo wengine................ 16
2:3:0 Ukoloni................................ 20
2:3:1 Athari za ukoloni katika utamaduni........... 22
2:4:0 Biashara ya utumwa................................ 36
2:5:0 Vita vya ukombozi................................ 38
2:6:0 Vyama vya kisiasa................................ 43
2:7:0 Siasa ya Ujamaa................................ 47
2:8:0 Hitimisho................................ 51
Tanbihi................................ 52

SURA YA TATU.

3:1:0 Utangulizi................................ 53
3:2:0 Majilio ya Waarabu na mateso.................. 54
3:3:0 Wajerumani na Waingereza Tanganyika.......... 61
3:4:0 Waafrika katika siasa................................ 67
3:5:0 Mchango wa Nyerere................................ 69
3:6:0 Pingamizi kwa wapiganiaji uhuru.............. 76
3:7:0 Upungufu wa Watanganyika................................ 78
3:8:0 Hitimisho................................ 81
Tanbihi................................ 81

SURA YA NNE

4:1:0 Utangulizi........ 82
4:2:0 Unyonge........ 82
4:3:0 Uadilifu........ 88
4:4:0 Siasa na Uzalendo........ 94
4:5:0 Maonyo kuhusu maovu na dunia........ 100
4:6:0 Malezi........ 104
4:7:0 Majaaliwa........ 110
4:8:0 Mapenzi na swala la Unyumba........ 114
4:9:0 Hitimisho........ 119
Tanbihi........ 119

SURA YA TANO.

5:1:0 Hitimisho........ 120
Tanbihi........ 125
5:2:0 Marejeo........ 126

## TABARUKU .

Kazi hii namtabarukia Marehemu Baba yangu mzazi Herman Lyayuga Muaka kwa kunitakia mema maishani na kwa kunitunza kwa mapenzi ya mzazi hadi alipoiaga dunia. Aidha namshukuru kwa kunitakia hili ijapokuwa hakuishi kuliona.

Na kwa mama zangu wapendwa Serah Vugutsa na Aidah Agidza, ni mama aujuao uchungu wa mwana.

### Huba kwa Wazee Wangu.

Mama, mpendwa mwenye huruma, mchunga wa roho yangu
Mama, ukikesha kwa lazima, amani iweko kwangu
Mama,ukae ukusimama, kwa kuhofu chozi langu
Nitakulipaje wema, ikubali twaa yangu

Mama, kinichombeza kwa hima, nitulize ari zangu
Mama, ukiimba na kusema, kunipoza roho yangu
Mama,unilaze na mapema, pale kitandani pangu
Nitaulipaje wema, ikubali twaa yangu

Mama, na usiku nigutuke, maziwa yako nataka
Mama, nitupe vitekete, nawe ukishughulika
Mama, na kinyesi kinitoke, hakika ukisumbuka
Nitaulipaje wema, ikubali twaa yangu

Mama, mikono yako himaya, mimi nilihifadhika
Mama, na joto likiningiya, hadi nikiburudika
Mama, nawe kinikumbatiya, kwa imani iso shaka
Sina la kukulipiya, Mamangu muhibaka

Mama, na kitako uniweke, nilipotimu miaka
Mama, kwa miguu nisoteke, napita nikianguka
Mama, dede miguu nitake, na viambaza kushika
Na wewe ushughulike, nisije nikavunjika

Mama, nikue nikaramke, unitie na chuoni
Mama, nisome nielimike, niwe mtu duniani
Mama, upowe ufurahike, ili upate amani
Hakuna wa kuipita, hadhi yako duniani

Mama, bado ninakuhitaji,kwa furaha na simanzi
Mama, leo ninakutaraji, nizidishie mapenzi
Mama, nipate njema siraji,mamangu nakuenzi
Jambo lako silivunji, natenda bila upinzi

Baba, wewe sijakusahau, uli huko kaburini
Baba, wala sifanyi dharau, usinitie kosani
Baba, mimi hukuweka juu mlezi wa utotoni
Msaada wako mkuu, sisahau abadani

Baba, na wewe msaidizi, sikutoi shukurani
Baba, rohoyo ina mbawazi, wende urudi kazini
Baba, kunikumbuka kizazi, mote mwangu utotoni
Chakula pia mavazi,daima uli mbioni

Baba, unibebe kwa ulezi, unapokuwa nyumbani
Baba, unipanguse machozi, unisuke mikononi
Baba, unipe na uongozi, niongoke ukubwani
Sinacho cha kukujazi, pokea yangu imani

Mama, sitosahau faraji, na wema wako ulinzi
Baba, na damu haiwi maji, sitojitia kisunzi
Nyote, imani yenu saruji, ni msingi wa mapenzi
Radhi zenu nahitaji, dunia ina simanzi

1. S.A. Mohamed (1980:46)

## SHUKRANI .

Nimeweza kuikamilisha kazi hii kutokana na usaidizi nilioupata kutoka kwa watu wengi. Sina namna ila kuwataja baadhi yao. Hata hivyo kwa wale ambao sitawataja kwa sababu ya wakati na nafasi nawaomba waelewe kuwa usaidizi wao ulinifaa zaidi.

Kwanza kabisa nawashukuru wasimamizi wangu Ndg. Kithaka wa Mberia na Ndg. Mungai Mutonya kwa kuniongoza na kunishauri katika utafiti wangu. Mapendekezo yao ndiyo ambayo yameniwezesha kujitokeza na kazi kama hii.

Ningependa vile vile kuwashukuru Waalimu wangu wengine katika idara ya Isimu na lugha za Kiafrika kwa kunipa misingi katika mambo ya usomi. Hususan ningependa kuwataja Ndg. John Habwe, Gichobi Mungania, Prof. Abdulaziz, Prof. J. Kitsao, Prof. M. Bakari, Kineene wa Mutiso. Nawashukuru pia Mwalimu Wafula wa Kenyatta na Mwalimu Wamitila wa Kikuyu kwa msaada mkubwa alionipa kabla na wakati wa kuiandika hii tasnifu. Sitamsahau daima dumu.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu tulioabiria pamoja kwenye chombo cha usomi na kwa kunipa fursa ya kutaalamika kutokana na mijadala yao. Wengi wao walikuwa marafiki ambao walirahisisha maisha Chuoni. Hawa ni pamoja na Faith Njeri, Grace Chepkwony, Evans Mirieri, Kamau Gatare, N. Michira, G. Mwaro, F.Baya, Z. Mosoti. Upande wa Isimu kulikuwa na Lillian Kaviti, Mary Gitau, Lydia Kimani na Lucy. Bila wao kungekuwa na upweke usioelezeka.

Nashukuru familia ya Herman Muaka kwa usaidizi wao kihali na mali. Mapenzi yenu yalinifaa sana. Mama Aidah, Mama Serah, Simon, Ken, Dorothy, Lucy, Patty, Nancy, Mac, Hilda na Edwin.

Shukrani za kipekee ziwaendee Angaluki na Hulda Kwa kunilea na kunisomesha. Mlikuwa kama baba na mama. Mungu hatawanyima japo kitu kidogo.

Rachael na Gillet. Yote mliyonifanyia sitayasahau. Na kila siku mtabarikiwa kwa huruma zenu.

Sitawasahau wengine kama Margaret Njuguna, Elijah Tali, Amunga,Jairus Muaka, John Marani, Bw. Amatsimbi Misigo, Shemeji Nyadawa. Kwenu nyote namuomba Mungu ayahifadhi maisha yenu na amjaze kwa baraka zake siku zenu hapa duniani.

Namshukuru Ndg. Lijodi kwa kunipigia chapa hii kazi kwa ufasaha

Namshukuru Mungu mweza vyote kwa kunipa uzima ili nifikie hiki kiwango.

**Nyasaye ave harara nende munyi.**

## MUHTASARI .

Utafiti huu unahusu uhakiki wa maudhui katika ushairi wa M.M. Amir na una jumla ya sura tano.

Katika sura ya kwanza tumetambua somo letu la utafiti na malengo yetu. Tumeweza vile vile kutoa haipothesia ambazo zilitusaidia katika utafiti wetu.

Sura ya pili inazungumzia masiala ya jumla hasa kabla ya majilio ya wakoloni na athari walizoziacha Afrika baada ya nchi za Afrika hususan Tanganyika kupata uhuru wa bendera.

Katika sura ya tatu tumechambua maudhui yapatikanayo katika **Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika.**

Sura ya nne imechunguza maudhui yanayopatikana katika diwani ya **Tungo Zangu** na **Malenga wa Mrima** . Masiala kama vile majaaliwa, unyonge , siasa na uzalendo na mengine mengi yameweza kuchambuliwa kwa mujibu wa nadharia yetu ya Mbeko.

Sura ya tano ni hitimisho ambamo tumejaribu kuonyesha maoni yetu kuhusu kazi za M.M. Amir . Hapa tumeweza vile vile kuzipima haipothesia zetu.

Kila mwisho wa sura tuna tanbihi lakini marejeo yametolewa mwisho wa sura zote.

## 1:1:0 UTANGULIZI

Utafiti wetu ni wa kifasihi. Ijapokuwa fasihi imegawika katika makundi matatu, yaani tamthilia, ushairi na riwaya sisi tumejikita katika utanzu wa ushairi. Fasihi yoyote ile hutokana na jamii mahsusi na tunakubaliana na A. Abdalla anaposema yakuwa:

> Hakuna fasihi hata moja ulimwenguni ambayo imechimbuka na kuendelea kuishi katika ombwe tupu. Fasihi yoyote iwayo itakuwa imeupata uhai wake, miongozo yake na hata maudhui yake kutokana na hali ya kitamaduni, ya kisiasa na ya kiuchumi ya jamii hiyo iliyochimbukana nayo.[1]

Tunaamini ya kuwa lengo kubwa la fasihi ni kuielemisha jamii. Kwa hivyo, kutokana na yale msanii atakuwa ameyachota kutoka kwenye jamii, wanajamii wanapaswa kufaidika kutokana na mafundisho yatakayojitokeza. Ni jukumu la kila mwandishi wa kimaadili kuhakikisha ya kuwa anaiandika upya hali ya jamii kisanaa ili hiyo hali ijitokeze kwa wanajamii kwa namna ambayo itawafanya wahisi kuwa ule ukweli unawagusa.

Tunashughulikia kazi za mshairi wa kimapokeo Mwinyihatibu Mohamed Amir. Huyu ni mshairi ambaye anawekwa katika tapo moja na wanamapokeo wengine kama vile, Abdilatif Abdalla, Shaaban Robert, Amri Abeid, Mathias Mnyampala miongoni mwa wengine wengi

Utafiti wetu umejikita katika kipengee cha maudhui na tunaongozwa na nadharia ya Mbeko ambayo ni mojawapo ya nadharia za kijamii na tunatarajia ya kuwa itatupa mwelekezo unaofaa kwa kazi yetu.

1:2:0 SOMO LA UTAFITI :

Tumekwisha taja ya kuwa fasihi ni zao la jamii. Tunaamini ya kuwa mwandishi yeyote wa fasihi aichukuapo kalamu yake kuandika juu ya jamii fulani huwa ana kitu fulani ambacho anataka wasomaji wake wafaidike nacho. Kwa hivyo somo letu la utafiti lilihusu kazi za M.M. Amir ambaye kutokana na uchunguzi wetu wa hapa na pale tumeona ya kuwa hakuwa amepewa nafasi ifaayo katika uhakiki wa kifasihi.

Hilo kwetu lilikuwa tatizo. Ili kulitatua hilo tatizo ilitubidi kutambua ni mambo yapi ambayo M.M. Amir alikuwa ameandikia na ni kwa vipi alivyokuwa ameyashughulikia. Na ikiwa ni kweli yeye amewekwa kwenye tapo la washairi waliosifika kama vile Mathias Mnyampala, abdilatif Abdalla na wengine wengi kwa nini hana nafasi yoyote katika uhakiki wa kifasihi ?

Utafiti wetu umejaribu kwa hivyo kuyajibu maswali ambayo labda bila huu utafiti huenda hayangejibiwa ifaavyo. Kwa mfano tumetaka kujua ikiwa M.M. Amir alikuwa akijiimbia tu au alikuwa akiyashughulikia maadili. Tumetaka vile vile kuelewa ikiwa aliyashughulikia kwa upana wake au alijifinyia tu katika sehemu yake ya Mrima. Kuhusu haya maswali mawili imetubainikia ya kuwa Mshairi aliyaandika baadhi ya mashairi kutokana na msimamo wake wa kisiasa na kuna uwezekano mkubwa kuwa aliandika mashairi na utenzi uliokuwa na nia ya kuwatukuza na kuwafurahisha viongozi waliokuwa katika chama cha kisiasa alichokuwa akiunga mkono. Haya kwa

kiasi kikubwa yaelekea ya kuwa aliyafanya bila kuelewa yale aliyokuwa akiyaunga mkono.

Hata hivyo kwa upande mwingine M.M. Amir hakujikita katika sehemu ya Mrima bali alizungumzia hali inayoweza kupatikana katika jamii nyingi za Afrika Mashariki na maadili aliyopendekeza ni yale ambayo yanaweza kuzifaa jamii nyingi pia.

## 1:3:0 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni yetu katika huu utafiti yamekuwa kubainisha maudhui yanayojitokeza katika kazi za M.M. Amir. Matokeo ya huo ubainishaji yalipaswa kutuonyesha ikiwa M.M. Amir alikuwa ametimiza lengo lake kama mwanafasihi muadilifu au la.

Fauka ya hayo tumekuwa na nia ya kuyatafutia nafasi hayo maswala ambayo mshairi ameshughulikia katika jamii ya sasa. Je, M.M. Amir ana chochote cha kuiambia jamii ya sasa ambayo imekumbwa na matatizo mengi yanayoletwa na mabadiliko ya kisiasa, kijamii, kitamaduni, kiitiksadi na kadhalika ?

Kwa vile tulikuwa tunazishughulikia kazi zake kadhaa, lengo letu limekuwa la kutaka kuonyesha falsafa yake kuhusu maisha. Katika huu utafiti tumedhamiria vile vile kuonyesha mapendekezo ya mwandishi kuhusu uadilifu na mbeko zinazofaa katika jamii kwa jumla.

Tumegundua ya kuwa M.M. Amir ni Mshairi aliyekuwa ameyaandika mashairi yake baada tu ya uhuru - yaani wakati nchi nyingi za Afrika mashariki na kati na Afrika kwa jumla zilipokuwa ndio tu zimejinyakulia uhuru wa bendera. Mashairi yapatikanayo katika

Malenga wa Mrima (1977) yameandikwa miaka kadhaa baada ya uhuru. Kutokana na huo uchunguzi tulitaka kujua ikiwa yale yaliyokuwa yakifanyika yalimfanya M.M. Amir abadilishe mtizamo juu ya maswala muhimu kisiasa, kiuchumi na kijamii ya wakati huo.

Waaidha imekuwa nia yetu kuchangia katika uhakiki wa kazi za fasihi kwa kiasi fulani. Pia tumekusudia kuwapa moyo wale watakaotaka kuongezea kufanya hivyo.

## 1:4:0 SABABU ZA KULICHAGUA HILI SOMO

Kutokana na uchunguzi wetu wa hapa na pale imetubainikia ya kwamba M.M. Amir ni mshairi aliyekuwa akijaribu kuchangia katika uandishi wa fasihi ya kiswahili. Kwa kuzishughulikia kazi zake nia yetu imekuwa kuyaweka wazi wazi yale ambayo anayashughulikia.

Imekuwa muhimu kwetu kuzishughulikia kazi za M.M. Amir kwa sababu hazikuwa zimeshughulikiwa ipasavyo. **Utenzi wa uhuru wa Tanganyika** (1967) na **Tungo Zangu** (1977) ni kazi ambazo hazijawahi kuhakikiwa kadiri tujuavyo. Kwa vile tunamuweka katika tapo la wanamapokeo ambao wamewahi kusifiwa na kazi zao kushughulikiwa tungetarajia ya kwamba naye vile vile angekuwa amepawa nafasi katika uhakiki wa kifasihi.

Uchunguzi wetu umeonyesha ya kwamba M.M. Amir ni mshairi anayeshughulikia maudhui mbalimbali. Maudhui haya yatapata nafasi katika jamii ikiwa yatahakikiwa na kuwekwa bayana kwa manufaa ya wanajamii.

S. Chiraghdin katika utangulizi wa **Sauti ya Dhiki** (1973)

akimnukuu Shaaban Robert anasema ya kuwa :

> "... uzuri wa ushairi ni uzuri wa milele... Mashairi yenye vipopo vya fikira, vito vya adili na utukufu wa matendo ambayo watu wa karne yoyote hawataridhia kuyatupa na kuyasahau ndiyo maana ya ushairi " 2

Tukitilia maanani nadharia yetu ya Mbeko na uzito uliomo katika hili dondoo tunapata hamu ya kutaka kujua ni yapi ambayo M.M. Amir anashughulikia. Ni kutokana na uhakiki huu ndipo tunaweza kujua ikiwa ushairi wa M.M. amir una uzuri na maadili ambayo daima yatawanufaisha watu wa karne yoyote. Nadharia ya Mbeko ndiyo hasa imetuongoza na ndiyo imekuwa mizani yetu.

Licha ya kuwa dhima ya fasihi ni kuielemisha jamii mwandishi anayoiandikia, tuliichagua mada hii ili angalau tuweze kuchangia katika uhakiki wa kifasihi. Kwa vile sisi tumejikita tu katika kipengee cha maudhui tunawapa wahakiki wengine nafasi ya kushughulikia vipengee vingine maanake kama asemavyo Hough (1966) hakuna kazi ambayo huhakikiwa kikamilifu. Uhakiki haufanywi mara moja mara moja tu, ni kitu kinachofanywa mara kwa mara kwa mitizamo tofauti tofauti.

## 1:5:0 UPEO NA MIPAKA

Utafiti wetu umejikita kwenye uhakiki wa kimaudhui wa kazi za Mwinyihatibu Mohamed Amir. tumezishughulikia diwani zake tatu ambazo zilichapishwa wakati tofauti tofauti.

1. <u>Utenzi wa uhuru wa Tanganyika .</u>

2. Malenga wa Mrima.

3. Tungo Zangu.

Tungependa ieleweke ya kwamba hizi diwani tatu ijapokuwa zimechapishwa wakati tofauti tofauti, kuna baadhi ya maudhui ambayo yanaingiliana sana. Yaani yanapatikana katika zaidi ya diwani moja. Kwa hivyo jambo ambalo tunataka kueleza ni kwamba tumezishughulikia diwani zote tatu ili tuweze kutambua jinsi ambavyo maudhui yanayopatikana yanavyoendelea kukua au yanavyoonyesha mitizamo tofauti tofauti ya mwandishi kuhusu jamii na maisha kwa jumla.

Jambo jingine ambalo ni muhimu kutajwa ni kuwa kutokana na upana wa maudhui yanayojitokeza katika diwani zote tatu, imekuwa afadhali kuyagawa maudhui haya katika mafungu. Kwa mfano tumepata vichwa kama vile uzalendo na siasa, unyonge, malezi na kadhalika.

Waaidha, ili kuyashughulikia kikamilifu mashairi haya imetubidi kuushughulikia **Utenzi wa uhuru wa Tanganyika** katika sura moja na zile diwani mbili zingine katika sura nyingine moja.

## 1:6:0 HAIPOTHESIA

Utafiti wetu umekuwa na haipothesia kadhaa ambazo tutajaribu kuzipima katika sura ya tano.

Kwanza kabisa tulikisia ya kwamba M.M. Amir ni mwandishi aliyeathiriwa na imani kuwa yote yafanyikayo kwa binadamu na dunia yake ni majaaliwa.

Mwandishi anaonyesha chembechembe za taasubi za kiume katika

uandishi wake.

M.M. Amir ni mwandishi wa kuimba tu wimbo wa viongozi wa nchi ya Tanganyika na sera zao bila kufikiria kwanza.

## 1:7:0 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI .

Ushairi wa kiswahili na washairi wa kiswahili wameandikiwa na wahakiki wengi wakichukua mitizamo tofauti tofauti. Kuna wale wamezihakiki kazi za kifasihi kimaudhui, kuna wale ambao wamezihakiki kifani na kuna wale wamezichunguza katika hizo daraja zote kwa pamoja.

Sisi tumezishughulikia kimaudhui kazi za M.M. Amir ambaye kadiri tujuavyo hajawahi kushughulikiwa ipasavyo. Mengi ya yale makala tuliyowahi kuyasoma yalikuwa yakizitaja tu kazi zake au yeye mwenyewe.

M. Mulokozi katika jarida la Kiswahili anamtaja tu M.M. Amir. Hapa Mulokozi alikuwa akimpinga yeye pamoja na wenzake wa tapo la wanamapokeo kuhusu msisitizo wao kuwa asili ya ushairi wa kiswahili ni vina na mizani. Hapana zaidi ya hayo tunayoambiwa na Mulokozi kuhusu kazi za M.M. Amir.

Katika Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili kitabu kilichohaririwa na F.M. Topan (1975), A.H. Taruka anaitaja diwani ya Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika (Ibid) kuna baadhi ya kazi zilizoishughulikia siasa ya Tanganyika kiutenzi.

Kazi iliyojaribu kushughulikia maudhui ya baadhi ya kazi za M.M. Amir ni yake G.K King'ei (1985) katika Mwongozo wa malenga wa mrima. Kwa kweli King'ei (ibid) alikuwa akiyataja yale maudhui

yanayojitokeza katika diwani ya Malenga wa Mrima na wala hakuyahakiki. Isitoshe yeye aliyazungumzia mambo mengi ya kimaudhui na fani na akawa anayatajataja tu. Lengo lake wakati ule lilikuwa kuwapatia wanafunzi wa shule za upili mwongozo wa kujibu maswali ya kidato cha nne.

Hata hivyo hii ni kazi ambayo imetufaa sana katika kutambua upungufu au sehemu ambazo hazikushughulikiwa katika diwani ya Malenga wa mrima.

Diwani zile zingine mbili, **Utenzi wa uhuru wa Tanganyika** na **Tungo zangu** kadiri tujuavyo hazijafanyiwa uchunguzi. Kazi yetu imekuwa ndiyo ya kwanza kuzishughulikia kazi za M.M. Amir tuzijuazo

## 1:8:0 MSINGI WA KINADHARIA :

Kigezo tulichokitumia katika uhakiki wa kazi za M.M. Amir kilikuwa nadharia ya mbeko au kama wanavyoiita nadharia ya kiadilifu.

Hii ni nadharia ambayo ilianza zama za kina Plato huko Ugiriki na kwa hivyo ni nadharia ambayo ina historia ndefu.

Plato na wengine katika tapo lake waliiweka sanaa mahali pake na kuamini kuwa sanaa ilikuwa na umuhimu fulani kwa jamii. Plato aliamini hasa kuwa ushairi ni lazima uhakikiwe na kupitishwa na kamati ya wanasheria wenye ujuzi wa mashairi, kuwa ni ya kufaa na kuwa mambo yaliyomo yatawafaa watoto na vijana kukua na tabia ya kuzitii sheria za nchi yao.

F.E.M.K Senkoro (1988) akilizungumzia hili swala la sheria za Plato anasema :

> msisitizo kuhusu dhima ya uelemishaji inayojitokeza katika ushairi na ambayo kwa hakika ulienea kote Ugiriki kwa wakati ule ulijitokeza mno katika maandiko ya Plato. Ushairi ni lazima utumikie mtu kiroho, umnawirishe kiroho na kumpa uadilifu wa kijamii. 3

Kwa hivyo tunaona ya kwamba dhima ya mshairi kama anavyopendekeza Plato na wenzake ni kuelemisha wanajamii.Katika utafiti wetu tumejaribu kuonyesha jinsi M.M.Amir alivyolitimiza jukumu la mshairi katika kuielemisha jamii kwa kutalii mengi ya maudhui yapatikanayo katika kazi zake.

Ijapokuwa tumekubaliana kwa kiasi kikubwa na yale Plato asemayo kuhusu jukumu la fasihi la kuelemisha, hatukubaliani naye asemapo kuwa ni lazima ushairi ueleze mazuri tu ya mashujaa na watawala wa nchi. Tunaamini ya kuwa kazi nzuri ya kifasihi ni lazima iyaeleze hata yale mambo mabaya (maovu) ya viongozi na kupendekeza njia za kuyaepuka hayo mambo ambayo hayaambatani na maadili ya jamii. Pale ambapo tutasita kuyafichua maovu ya viongozi tutakuwa tukiwapatia fursa na uhuru wa kuendelea kuwanyanyasa wanajamii kwa kufuata yale yanayoweza kuiangamiza ile jamii. Wanapaswa kuongoza kwa kufuata maadili yaliyoko.

Aristotle alikuwa mwanafalsafa wa kigiriki na alikuwa mmoja wa wahakiki na wananadharia wa Urasimu baada ya Plato. Aristotle alikuwa mtetezi wa dhana ya mwigo akidai ya kuwa watu hupenda kuona kwa mifano - yaani viwakilisho. Sanaa huwakilisha maisha ya watu kisanaa. Mara nyingi katika hayo maisha ya watu tofauti am-

bayo huwa yamesawiriwa huwa kuna mifano mizuri na mibaya. Huwa ni uamuzi wa mwanajamii kufuata mifano itakayomletea heri. Mshairi muadilifu huwaelimisha wanajamii ili waifuate mifano mizuri na kuiasi ile mbaya. Katika kundi la urasimi mpya mtu huonekana kuwa yu kiumbe ambaye hakukamilika. Alikuwa ni kiumbe mwenye kasoro na kwa hivyo alipaswa kurekebishwa kupitia mafundisho ya sanaa. Kwa hivyo tunaona jukumu la fasihi la kuelemisha likijitokeza tena. Majina ambayo tunaweza kutaja katika hili kundi ni pamoja na Horace, Virgil, John Dryden miongoni mwa wengine.

L. Tolstoy ambaye pia anachukuliwa kuwa mmoja wa wananadharia ya Mbeko anasema ya kuwa namna ambavyo ujuzi unastahili kuelekea zaidi kwenye ukweli na kuchukua nafasi ya dhana za kupotosha, ndvyo sanaa nayo inastahili kutufunza kuwa wenye huruma na upaji zaidi na kutupilia mbali uroho na tabia zote zisizofaa. Kwa Tolstoy hilo ndilo jukumu la sanaa.

Vile vile Tolstoy aliamini ya kuwa jukumu jingine la sanaa ni kuleta undugu miongoni mwa watu wote. Alikataa kukubali mpangilio wa watu katika matabaka na akaamini ya kuwa watu wote ni sawa. Aliona sanaa bora kuwa ile iliyoleta umoja na wala sio ile iliyowagawanya wanadamu.

Aidha, Tolstoy aliamini ya kuwa jamii ni lazima iwe na maelekezo ya kidini ya kuwapa watu mkondo sawa wa kufuata. Sanaa kwaake inatakikana isababishe umoja kati ya watu wote ulimwenguni. Huu umoja utawezekana tu ikiwa sanaa itahusika na mambo ya kidini ya kutuhusisha na mungu wetu au mambo ya kuamsha hisia sahili ambazo zinaweza kumuathiri kila mmoja.

Wataalamu kama vile S.A.K Mlacha wanaona mojawapo ya majukumu ya fasihi kuwa uchunguzi wa dunia ya binadamu na kuamsha kuelewa kwa jamii. Kwa hivyo binadamu anahusishwa na jamii na ni huu uhusiano ambao huchangia sehemu kubwa ya wao kuwa wanadamu. Kwa kufanya hivi, jukumu kubwa la fasihi linakuwa la kijamii na kimaadili kwa sababu fasihi huchukua mfumo wa kuirekebisha jamii. Hii inaweza kuwa kisiasa, kisaikolojia, kiitiksadi, kijamii au kitamaduni. Hii inaonyesha ya kuwa kupitia fasihi jamii inaweza kurekebishwa katika vipengele vyake vyote. Jambo muhimu wakati wa kuzihakiki kazi za M.M. Amir limekuwa ni kujaribu kumpima tukizingatia maelekezo ya huu mtizamo.

T.S.Y Sengo anatoa mawazo yake kuhusu fasihi kwa kusema kuwa :

> Taaluma ya fasihi kama taaluma zote ina dhima kubwa katika kujenga, kuhifadhi na kuendeleza hadhi na taadhima ya jamii.

Sengo anaona ya kuwa fasihi ina wajibu wa kutumia yale iyapatayo kutokana na utafiti wake kuzidi kuiendeleza jamii. Kwa hivyo, kwake fasihi ni chombo kinacholeta uhusiano bora miongoni mwa watu.

A.G Gibbe (1978) anasema kuwa:

> Washairi wasishangilie tu, lazima wadadisi na kuchambua mambo.

Tunakubaliana kwa kiasi kikubwa na haya maoni ya Gibbe ambayo yanayapinga ya Plato kuhusu namna ambavyo viongozi wanapaswa kusawiriwa. Inafahamika ya kuwa kuna baadhi ya washairi ambao wa-

nawasifu tu viongozi bila ya kuwakosoa wanapokosa. Mtizamo wa Gibbe ni mpana na umetufaa sana.

Tuna hakika ya kuwa nadharia ya Mbeko umetufaa ipasavyo katika kuzishughulikia hizi diwani za M.M. Amir.

**1:9:0 NJIA ZA UTAFITI :**

Kazi tuliyoishughulikia kama tulivyokuwa tumetaja hapo awali ni ya fasihi andishi na kwa hivyo tulisoma makala mengi ya kifasihi na hasa yale yaliyokuwa yakihusu ushairi.

Tulizitalii na kuzihakiki kwa makini diwani zote tatu za M.M Amir ili matokeo yetu yasawiri picha kamili ya uandishi wake.

Kwa vile kigezo chetu kilikuwa cha nadharia ya Mbeko tulisoma makala tofauti tofauti yaliyoshughulikia hii nadharia . Kulikuwa na mitizamo tofauti tofauti na hii ilitufanya tuchuje baadhi ya mambo na kushikilia mitizamo ambayo tuliamini ndiyo iliyopaswa kutuongoza.

Kwa kiasi kikubwa utafiti wetu ulifanyiwa kwenye maktaba ambamo tulifaidika kutokana na makala mengi yaliyoshughulikia somo la ushairi. Tuliwahi vile vile kufaidika kutokana ba mijadala nje ya maktaba kutoka kwa wataalamu wa ushairi.

**TANBIHI :**

1. Tazama A. Abdalla (1978)
2. S. Charaghdin (1973)
3. Tazama F.E.M.K Senkoro (1987)

# SURA YA PILI

## 2:1:0 U T A N G U L I Z I .

Katika sura hii tunakusudia kushughulikia mambo kadhaa kiujumla Haya yatakuwa kama msingi kwa sura zitakazofuata. Mbali na kuchunguza mazingira alimokulia M.M. Amir, tutataja pia baadhi ya wanamapokeo na yale waliyoyashughulikia. Hata hivyo tunaposema hivi si kwamba utafiti wetu unawahusu hawa washairi wengine bali tunajaribu tu kuwahusisha na M.M. Amir.

Historia ya Afrika masharikI, hasa nyakati za washairi wengi wa kimapokeo zilikuwa za mabadiliko makubwa sana kwa sababu ni wakati huo ambapo wakoloni walikuwa wakija sehemu hizi kwa minajili ya kujitafutia mali. wageni waliwatawala wenyeji wa Afrika mashariki na kutokana na huo utawala wakaweza kuwaathiri. Itajwe kuwa wakoloni nao waliathiriwa kwa kiasi fulani na wenyeji kutokana na maingiliano baina yao. Kwa hivyo katika sura hii tutajaribu kujadili zile athari zilizoletwa na wakoloni. Kwa kiasi kikubwa tutajishughulisha na athari za wazungu katika dini, malezi, ndoa, elimu, uongozi na kifo.

Inapaswa kutajwa pia, kutokana na majilio ya wageni, na kwa sababu ya wenyeji kugundua madhumuni ya hawa wageni, walianza kutafuta njia na mbinu za kuwaondao wakoloni kutoka nchi zao.

Wananchi walianza kupigania haki zao. Kulikuwa na vita baina ya wakoloni na wenyeji katika nyakati tofauti tofauti.

Tutachunguza baadhi ya hivi vita ili kuelewa umuhimu wake na jinsi wananchi walivyojishughulisha navyo. Hata hivyo haya yatakuwa mambo ya jumla tu na tutajikita sana katika vita vya ukombozi nchini Tanganyika.

Tunakisia ya kwamba Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa nchi ya Tanganyika alichangia kwa kiasi kikubwa siasa nchini Tanganyika. Tutagusia mchango wake kupitia siasa ya ujamaa na chama cha TANU.

## 2:2:0 K U H U S U M . M . A M I R

Mwandishi wa kazi tunazozihakiki ni Mwinyihatibu Mohamed Amir M.M. Amir alizaliwa katika kijiji cha Tongoni, Tanga mnamo mwaka wa 1920. Elimu yake ya kwanza aliipata katika shule ya msingi kwao Tongoni. Aliendelea na masomo yake na akafikia kiwango ambacho kinafikiriwa kuwa sawa na kidato cha pili katika mfumo uliokuwepo hapa kenya wa 7-4-2-3.

M.M. Amir alianza kufanya kazi mnamo mwaka wa 1937 alipoajiriwa na East African Customs and excise Department.

Kuhusu utunzi wake, M.M. Amir alitunga shairi lake la kwanza baina ya mwaka wa 1957 na 1959. Shairi lenyewe linaitwa , **"Tungo zimo hatarini"** ambalo linapatikana katika diwani yake ya

Malenga wa Mrima (1977). M.M. Amir alianza kuandika mashairi yake katika magazeti ya wakati huo kama vile Mambo Leo, Ngurumo, Mapenzi Ya Mungu.

S. Chiraghdin (1975:9) katika utangulizi wa Malenga wa mrima (Ibid) anasema ya kwamba M.M. Amir aliupata umalenga wake kwa itifaki na kongomano la walinzi wa kunga za ushairi na jaza za wakurufunzi wake wa kishairi.Anaendelea kusema ya kuwa jaza hii nakongomano la umalenga wa M.M. Amir limepatikana kwa kina mwalimu Mwabando,Sheikha Mohamed Ali, Sheikh Amir Abedi na wengineo. M.M.Amir ametunga mashairi yake hasa katika nyakati za akina Shaaban Robert, Hassan Mbega, Abdalla Baruwa, miongoni mwa wengine.Inafahamika kuwa wengi wa hawa washairi waliandika kufikia miaka ya sabini ijapokuwa wengine hawakufikia nyakati hizi na hata wengine nao wamevuka mipaka na kufika mwanzo mwanzo mwa miaka ya themanini.

M.M. Amir ni mmoja wa wale wanaoshikilia msimamo kuwa mizani na vina ndivyo uti wa ushairi wa kiswahili. Katika hotuba yake aliyowasilisha katika chuo kikuu Dar-es-salaam mwaka wa 1973, "Utunzi bora wa ushairi wa kiswahili", alidai ya kuwa ushairi una miko, misingi, mipaka na ustadi wake kama fani nyingine za ulimwengu. Na katika jumla ya miko ni miko ya vina na mizani. Ijapokuwa huo ndio msimamo wake inafaa tuyafikirie mawazo ya wataalamu wengine kuhusu hilo swala. K.W. Wamitila (1992:17) anasema ya kwamba ushairi kama utanzu wa fasihi - kipengee cha utamaduni hauna budi kubadilika kadiri wakati unavyosonga.

M.M. Amir ni mshairi anayepania kushughulikia kila akionacho kuwa ni cha manufaa kwa jamii yake. Mwenyewe anasema hivi katika dibaji ya Utenzi wa uhuru wa Tanganyika (1968) :

> Matukio ya nchi yetu yaliyotukia toka siku za kabla ya uhuru wetu na hasa mambo na vituko vilivyodhihiri wakati wa kugombea uhuru yalinitia shauku kubwa ya kuyatia mambo hayo katika uandishi.

## 2:2:1 BAADHI YA WANAMAPOKEO WENGINE.

Tunapozungumzia juu ya wanamapokeo huwa hasa tunamaanisha washairi waliofuata arudhi za kiswahili kama vile mizani na vina. Hawa ni washairi wanaofikiria ya kuwa bila mizani na vina shairi haliwezi kuitwa shairi. Tumeipatia hii sehemu nafasi katika utafiti wetu kwani M.M . Amir ni mmoja wa hao wanamapokeo.

S. Chiraghdin (Ibid) anasema ya kuwa lazima shairi liwe na ulinganifu wa mizani, vina na lugha iliyo tukufu yenye kuvuta masikizi na fikra kama ambavyo sumaku huvuta chuma. Ni msimamo kama huu ambao wanamapokeo wengine kama vile A. Abedi (1965), D.P M. Massamba (1976) wanashikilia.

Hata hivyo kuna mambo mengi ambayo hulifanya shairi kuwa shairi na pia dai kuwa mashairi yenye vina na mizani ndiyo mashairi hasa ya kiswahili linatatiza sana. Hii kwa sababu hapo awali ushairi wa kiswahili haukuwa ukifuata hizo mbinu. A.M. Mazrui na E.K. Kazungu (1984:32) wanasema ya kuwa ushairi wa kiswahili hapo awali ulikuwa haufuati mbinu hizi za arudhi. Wanaendelea kudai

ya kuwa arudhi hii tuifuatayo leo inatokana na athari ya waarabu na waajemi. Hali kama hizi zinadhihirika hata katika nyanja nyingine ambapo watu wengi huuchukua utamaduni uliotoka Uarabuni na kudai ya kuwa ni wao lakini wa kizungu wanaukataa na kudai kuwa huo ndio wa kigeni. Katika mashairi ya ' Tungo ' uk .27, 'Tungo zimo Hatarini' uk. 28, 'Lea Mwema' uk. 25 , ambayo yanapatikana katika diwani ya Malenga wa Mrima yanaonyesha pingamizi ya mshairi kuhusu ushairi wa wanamapinduzi. Hata hivyo katika kitangulizi cha shairi la 'Tungo' uk. 27 mshairi anaonekana kukubaliana na wanaodai ya kuwa vina na mizani haitoshi wakati anaposema kuwa ' kweli vina na mizani ni alama ya utungaji mwema lakini huitwa baadhi tu ya kanuni za utungaji.' Mshairi anadai kuwa kuna wale wanaoandika mashairi ambayo yana vina vilivyochakaa.

Baadhi ya wanamapokeo ni kama vile Shaaban Robert ambaye ameandika mashairi mengi na riwaya kadhaa. S.N. Eliufora (1967) anasema:

> Jina la marehemu Shaaban Robert limeota mwamba usiobomoka mioyoni mwa waafrika wengi wa Afrika ya mashariki katika karne yetu ya leo. Sifa za marehemu huyu zimeenea pote duniani kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kalamu yake kuihusisha lugha ya kiswahili na kueneza makini yake.1

Haya ni maneno yasemwayo kuhusu Shaaban Robert kutokana na mchango wake mkubwa katika uwanda wa lugha ya kiswahili.

J. Habwe (1993) anasema:

> Shaaban Robert ni fanani ambaye katamba pakubwa katika mwanda wa uandishi wa tanzu tatu muhimu

katika fasihi ya kiswahili. Licha ya kujihusisha na hadithi amejishughulisha vile vile na riwaya, insha na ushairi. 2

Anayosema J.Habwe (Ibid) ni mambo ambayo tunaweza kupata ushahidi kutokana na riwaya na diwani lukuki alizoziandika Shaaban Robert. Kwa mfano katika masomo yenye Adili (1967) tunaona namna anavyoongelea maadili:

Kweli nimo kutafuta, nisaidie rafiki
Na endapo tutaipata, zitakoma zetu dhiki
Kweli taa ya mafuta, yatosha kibanda hiki
Yatosha tukiipata, aso kweli haridhiki. 3

Shaaban Robert anaandika mashairi yake akiongozwa na falsafa iliyojikita katika imani ya dini, nayo ni kwamba dunia imejaa uovu, ujinga, uzandiki, udanganyifu, dhuluma na mengine mengi. Hata hivyo anaamini ya kwamba vitu hivi vyote vitashindwa ikiwa wanadamu watafuata maadili yanayohitajika. M.M. Amir naye yuaweza kutizamwa katika huu mkabala hasa katika diwani zake mbili Tungo - Zangu na Malenga wa Mrima ambazo zinajadili maovu yafanyikayo na kutoa maonyo yanayopaswa kuwaelimisha wanajamii kimaadili.

Aghalabu Shaaban Robert alijihusisha na maswala kama vile unyanyasaji wa wanawake, ubaguzi wa rangi, athari za ukoloni kwa Mwaafrika, uhuru wa Mwaafrika, uovu duniani na namna ya kujenga jamii mpya. Haya ni masuala ambayo yamejitokeza bayana katika maandishi yake husasan katika Wasifu wa siti binti saad, Siku ya Watenzi wote, Ashiki kitabu hiki miongoni mwa vitabu vyake vingi.

Waaidha Shaaban Robert ni mshairi ambaye aliuangalia utamaduni kama kitu kinachoweza kubadilika katika maswala mengi ya kijamii tunaona mtizamo wake ukilandana na wa M.M. Amir.

Abdilatif Abdalla naye aliandika diwani yake ya Sauti ya Dhiki (1973) alipokuwa kifungoni baina ya 1969 na 1972. Aidha ameandika Utenzi wa Adamu na Hawa.

Mengi ya mashairi aliyoandika ni ya kisiasa na ya uhusiano baina ya waja. Kwa mfano katika shairi lake la 'Ukamilifu wa mja' anasema:

> Ameumbwa mwanaadamu kwa lililo zuri umbo
> Bali si wote fahamu, waliyo na sawa mambo
> Wako waliyotimamu, na wengineyo wa kombo
> Na watu kuwa na tumbo, si kwamba wamekamilika.

Katika ' Tuza Moyo ' uk. 6 anasema:

> Akhi tuliza mtima, uwate kusononeka
> Hakuna lisilokomo, siku kifika tatoka
> Kusubiri ni lazima, na kumuomba Rabbuka
> wasiya wako meshika

Katika hilo dondoo tunaona dhana ya majaaliwa ambayo kwa kiasi fulani imejadiliwa na M.M. Amir pia. Waaidha dini inampatia matumaini maishani kama inavyodhihirika miongoni mwa wanamapokeo wengine.

Mathias Mnyampala ni mwanamapokeo mwingine kama tulivyotaja katika 2:2:0 ambaye aliandika wakati mmoja na M.M. Amir na ambaye aligundua haja kubwa ya kuandika kwa sababu ya wanajamii wake. Hivyo basi akichukua msimamo wa kiuadilifu, analenga kuwaelemisha wanajamii ili maisha yao yawe bora na wao wenyewe wawe binaadamu wazuri. Anaangalia maswala ambayo yanaiharibu jamii kama vile rushwa, mamlaka, ukorofi, choyo na mengine mengi. Haya ni mambo muhimu ambayo tunafikiri kwa kiasi kikubwa yanapiga mwengo yale M.M. Amir anazungumzia katika ushairi wake. Kwa kuwataja baadhi

ya hawa washairi tumejaribu kuonyesha ya kuwa wengi wa wanamapokeo lengo lao kubwa katika ushairi lilikuwa kuiboresha jamii na hilo lilikuwa jambo muhimu sana katika teneti za uadilifu. Tunatarajia kwa hivyo M.M. Amir ayashughulikie maswala haya kwa upana wake.

## 2:3:0 U K O L O N I.

Ukoloni ni jina linaloelezea namna jamii moja inavyoitawala nyingine. Kwa hivyo tunaweza vile vile kusema kuwa ukoloni ni tabia ya nchi moja kuitawala nchi nyingine kwa madhumuni ya kuimarisha uchumi, fahari na ulinzi wa nchi inayotawala. Inafahamika ya kwamba nchi ikiwa chini ya utawala wa kikoloni huachwa maskini kwani utajiri wake wote unachukuliwa na kutumiwa katika kuinua maisha ya watu wanaotawala.

Sura hii ni muhimu sana kwa utafiti wetu kwa sababu inalizungzia swala la ukoloni na athari zake na kwa hivyo inajenga misingi ya uhakiki wa kazi za M.M. Amir hasa katika sura ya tatu ambapo ameshughulikia ukoloni na jinsi Watanganyika walivyonyanyaswa jambo ambalo halikuhimiza udugu na uhusiano mwema kati ya wakoloni na Watanganyika.

Bara la Afrika liliwahi kutawaliwa kikoloni katika wakati fulani wa historia yake. Kulikuwa na wakoloni tofauti tofauti ambao walizitawala sehemu tofauti tofauti za bara la Afrika pamoja na visiwa vyake. Tukiangalia janibu la Afrika ya mashariki

tunalotambua ni kwamba Waarabu ndio waliokuwa watu wa kwanza kuifanya pwani ya Afrika mashariki kuwa koloni. Wao walianza kufika sehemu za upwa wa Afrika ya mashariki mwisho mwisho mwa karne ya kumi kutoka Bara Arabu ambako magomvi yao wenyewe yalisababisha wale walioshindwa kukimbilia Afrika mashariki. Ni hawa Waarabu ambao walianzisha biashara ya utumwa huku Afrika Mashariki.

Wareno pia nao wanatajwa kuwa walifika huku na kutawala pwani ya Afrika Mashariki. Inasemekana ya kuwa waliwafanyisha kazi wenyeji kando ya bahari bila malipo yoyote.

Carl Peters, Mjerumani, ndiye aliyeweka misingi ya ukoloni wa ujerumani katika Afrika Mashariki hususan Tanganyika. Alifanya mikataba isiyoeleweka na viongozi wa sehemu kadhaa za Tanganyika ambayo iliishilia katika Ujerumani kuweka bendera yao kwenye udongo wa Watanganyika.

Ni mateso na dhuluma waliyofanyiwa Watanganyika ndiyo iliyosababisha vita ambavyo M.M. Amir anashughulikia katika <u>Utenzi wa uhuru wa Tanganyika</u> (Ibid). Watu wengi walipoteza maisha yao katika jitihada zao za kupigania haki na uhuru.

Wazungu wengine ambao waliwahi kutawala sehemu kubwa ya Afrika Mashariki ni Waingereza. Hawa walizitawala nchi za Kenya na Uganda pia. Waliwadharau Waafrika sana na kuleta athari nyingi ambazo hadi sasa zimeota mizizi kweli kweli. Ni hizi athari ambazo M.M. Amir amejaribu kuonyesha katika ushairi wake jinsi zilivyofanya wanajamii kuasi maadili ya jamii na kujiingiza katika maovu ambayo yanaichafua jamii yote.

## 2:3:1 ATHARI ZA UKOLONI KATIKA UTAMADUNI.

C.K. Omari (1980) anasema kuwa :

> Utamaduni ni hali, mwenendo, imani na hayo yote ambayo yamekuwa sehemu ya kuwepo kwetu kama wanadamu wa jamii fulani. Utamaduni ni matunda ya mikono ya mwanadamu kama vile ujenzi, ufundi, uvumbuzi na uundaji wa vitu. 5

J.K. Nyerere naye anasema :

> Utamaduni ni moyo na uzima wa taifa. Taifa lisilo na utamaduni wake ni kama kaumu ya watu wasio na moyo unaowaunga pamoja kama taifa. 6

Jambo ambalo tunaweza kudondoa kutokana na hizi fasihi ni kuwepo kwa jamii fulani ambayo inatambulikana kutokana na utamaduni wake. Hata J.K. Nyerere (Ibid) anapotaja taifa bado anazungumzia juu ya watu ambao hapana shaka wanapatikana katika jamii fulani. Kwa hivyo utamaduni unajumuisha mambo mengi ambayo huendelea katika jamii kama vile siasa ya watu, dini yao, mavazi yao miongoni mwa mambo mengine mengi.

Yaelekea kuwa kabla ya wageni kufika huku Afrika, Waafrika walikuwa na utamaduni wao ambao ijapokuwa hatuwezi kudai ya kuwa ulikuwa sawa kote kote, tunaweza kusema kuwa baadhi ya mambo yalielekea kufanana ijapo kwa mbali. Ajabu ni kwamba wageni walipofika huku waliwadharau wenyeji na kudai ya kwamba Mwafrika hakuwa na utamaduni wowote na kwa hivyo wakaona ni wao ambao wangewapatia mwanga na kuwatoa katika giza na ushenzi. Walidai ya

kuwa mambo ya Waafrika pamoja na utamaduni wao ulikuwa wa kishenzi. F. Fanon anazungumzia swala hili kwa uzuri sana anaposema:

> Utawala (ukoloni) wa kitamaduni haungetenganishwa na utawala wa kigeni. Hii ni kwa sababu ukubalifu wa desturi za mzungu ulichukuliwa kuwa muhimu sana katika kumfanya Mwafrika akubali kutawaliwa. ...Ukoloni haukuinyima jamii uhuru wake wa mali tu pia nafsi yake, na <u>kuwaacha wanajamii kiakili na kimaadili</u> bila msimamo wowote. 7
> (Tafsiri na msisitizo ni wetu.)

Anayosema F. Fanon (Ibid) ni mambo ya kweli kabisa na yanadhihirika bayana katika jamii nyingi za kisasa. Ili kuzielewa vyema hizi athari itatubidi turudi nyuma katika historia ya watu wa Afrika na tuone namna mambo yalivyokuwa kabla ya majilio ya wakoloni. Hatutarajii kuwa na usawa katikaa yale tutakayosema kwa sababu kama tulivyowahi kutaja, tofauti hujitokeza ijapokuwa kidogo miongoni mwa Waafrika.

NDOA :

Ndoa ni muungano kati ya mwanaume na mwanamke. Tusisahau hata hivyo ya kwamba katika hali fulani mwanamke huweza kuoana na mwanamke na vile vile Mwanaume kwa mwanaume. Hata hivyo haya si mambo yanayotokea sana na kwa hivyo tutaangalia ndoa inayofahamika kwa wengi, yaani baina ya mume na mke au wake.

Katika jamii nyingi za Kiafrika ijapokuwa ndoa ilikuwa kati ya watu wawili (mke na mume), ilikuwa muhimu kwa jamii yote. Kwa hivyo wanajamii walihusishwa katika mipango ya ndoa na kila mtu katika familia akawa na jukumu katika mambo kama hayo.

Kayongo-Male (1985) anasema kuwa kijadi, wazazi wenyewe na jamaa yake walikuwa muhimu sana katika kuwatafutia watoto wao wale wachumba waliofikiria kuwa bora kwa ndoa. Anaungwa mkono na J. Mbiti (1969) ambaye pia anataja mambo kama hayo.

J.S. Mwakipesile (1974) anasema kuwa katika baadhi ya familia za Tanganyika, wazazi waliangalia mambo fulani fulani katika kumchagulia mtoto wao mchumba ;

> Katika jamii nyingine wazazi huhakikisha ya kwamba msichana wanayemtaka anatoka katika ukoo wenye heshima, familia ambayo haina wizi, ugomvi, uchawi na kwa jumla jina la ukoo liwe zuri. 8

Kwa kiasi fulani mambo mengi yalifanyika katika sehemu mbalimbali. Kwa mfano hayo yaliyotajwa hapo juu ijapokuwa yalihusu jamii za Tanganyika, itagunduliwa ya kwamba hata katika baadhi ya jamii za Kenya mathalani Waluhya, mambo kama hayo yalichunguzwa sana. Wazazi walichunguza mambo mengine kama vile magonjwa ya kifafa, kifua kikuu, ukoma na mengine mengi. Ikiwa msichana au mvulana alipatikana kuwa anatoka katika familia ya mojawapo ya hayo magonjwa, wazazi wangesita kumruhusu mtoto wao kuwa na uhusiano wowote naye.

Mambo kama haya yalipotiliwa maanani ilikuwa nadra kusikia visa vya kutalakiana. Mke na mume waliheshimiana. Mahari yaliyotolewa yalikuwa ishara ya shukrani kwa wazazi wa msichana kwa kumlea na kumkuza vizuri na pia kwa kumruhusu aende kuungana na familia nyingine.

Kama tulivyowahi kutaja hapo awali, mwanamume angeweza kuoa zaidi ya mwanamke mmoja. Wanaume wengi ambao walioa zaidi ya mwanamke mmoja iliaminika ya kuwa walikuwa na mali nyingi. Waaidha iliaminika ya kuwa angeweza kupata watoto wengi wa kufanya kazi za nyumbani kama ukulima. Aidha Mke wa kwanza angesaidiana na bwanake katika maamuzi ya kuoa mke wa pili aidha kwa sababu alikuwa tasa au kwa minajili ya kufanya na kusaidia katika kazi za nyumbani.

Siku hizi mambo si hivyo tena ijapokuwa kuna chembe chembe za mambo kama hayo katika baadhi ya jamii lakini ni katika zile zinazopatikana mbali na miji.

Hivi leo utamaduni wa kigeni umezivamia jamii zetu katika hii taasisi ya ndoa kiasi cha kutoweza kuwa na mwelekeo madhubuti. Kuna visa vingi vya mke na mume kuachana na hii hutokana na tamaa ya mmoja wao kutaka kupata mali. Wanawake wengi wameanza kupeleka malalamiko kortini wakidai talaka huku wakifahamu vizuri ya kuwa watapata sehemu ya mali ya waume zao wakidai ya kuwa mali hiyo ni ya kuwakimu wao na watoto.

Wale wanaofanya ndoa zao kwa kufuata sheria za dini ya kikristo hawaruhusiwi kuoa zaidi ya mke mmoja; yaani mitala.

Umuhimu wa wazazi na jamii katika uchaguzi wa mchumba haupo tena. Wengi wa vijana wa siku hizi ambao waliwahi kupata elimu ya kikoloni mara nyingi hawawahusishi wazazi wao katika mipango yao ya kujitafutia mchumba. Mara nyingi Mvulana hudai ya kuwa

hamuoei mtu yeyote katika jamii.

Kwa jumla ndoa za siku hizi zimepoteza heshima zilizokuwa nazo. Mali ndiyo inayoheshimiwa kuliko ule uhusiano baina ya mke na mume. Si ajabu kumpata mke wa mtu akiwa na uhusiano usio halali na mchumba wa kando ambaye labda na yeye ni mume wa mtu. Dhana ya mababa sukari na mama sukari inajitokeza hapa. Maovu na madhara yatokanayo na hii dhana mpya ya ndoa kama vile kuteseka kwa watoto,ukahaba ndiyo mambo ambayo tunatarajia kuyapata katika diwani za M.M. Amir na tutazishughulikia katika sura ya nne.

ELIMU.

Elimu ya jadi ilikuwa ikitolewa kwa jamii kwa kufuata utaratibu wa umri mbalimbali au utaratibu baina ya wanaume na wanawake Hii ilifanyika kwa sababu hapakuwa na shule ambazo kwetu huku Afrika zimetufikia kupitia kwa wageni na wamishonari ndio waliokuwa wa kwanza kutuletea elimu ya kizungu.

Lengo kubwa la mafundisho ambayo mara nyingi yalitolewa na wazee kwenye jamii lilikuwa kuwawezesha wanajamii kushiriki katika shughuli mbalimbali za maisha ya kila siku kama vile uchumi na ustawi wa familia au ukoo kwa jumla.

Kulikuwa na tofauti katika haya mafundisho kulingana na uwana kama asemavyo Y. Halimoja (1977) kuhusu baadhi ya jamii za Tanganyika :

> Wavulana walifunzwa ushujaa, ulinzi, heshima

> historia ya kabila au ukoo, na kadhalika. Wasichana walifunzwa maarifa ya nyumbani, heshima na namna ya kuishi na waume zao wakioelewa. Kwa mfano walifunzwa ngoma ya 'tingla' (kimakua) ambayo ilifanana na 'sindimba' ya wanamakonde ambapo wanawake walioaminiwa kuwa wataalamu kuliko wenzao walichezesha kiuno wakifundisha namna ya ya kufanya mapenzi na waume zao mbele ya safari kwa shabaha ya kudumisha ndoa. 9

Jambo ambalo tunapaswa kufahamu ni kuwa ndoa haipaswi kudumu kutokana na ustadi mtu alionao katika mambo ya kufanya mapenzi bali ndoa inapaswa kujengwa kwenye misingi ya mapenzi halisi. Anachokitaja Y. Halimoja ni kipengee kimoja tu katika ndoa na hakipaswi kuwa ndicho ambacho kitaidumisha ndoa.

Kama tulivyotaja hapo awali, shughuli kama hizi ziliendeshwa na wazazi au wazee. Inafahamika ya kuwa vijana wa rika moja walikuwa muhimu sana katika kufundishana. Walihakikisha ya kwamba kila mmoja wao alizifuata taratibu za jamii kubwa. Adhabu ilitolewa kwa wale wenye utovu wa nidhamu. Mambo kama haya ndiyo yaliyofundishwa katika jamii nyingi za Afrika. Ieleweke hata hivyo ya kwamba kulikuwa na tofauti ndogo ndogo kutoka jamii moja hadi nyingine.

Kufika kwa wageni kulileta mabadiliko makubwa ambayo yaliishilia katika upotovu wa baadhi ya wanajamii.

S.A.K. Macha (1988) anasema yafuatayo kuhusu wakoloni na elimu yao:

> Ni wakati ambapo wakoloni walipoanza kufundisha baadhi ya wanajamii na ku-

waonyesha utamaduni wao ili wapate kuungwa mkono na kuweza kuwatawala kiuchumi na kisiasa ndipo utamaduni wao (wakoloni) uliingia miongoni mwa jamii ya Mwaafrika na hasa miongoni mwa kizazi kichanga. 10

(Tafsiri yetu).

Wakoloni walipokuja, kazi iliyokuwa ikifanywa na wazazi ilichukuliwa na waalimu katika shule ambazo zililetwa na wakoloni Elimu hii iliaminika kuwa yenye hadhi na mafanikio kwa yeyote aliyeipata. Yale wazee walikuwa wakifundisha hayakutiliwa maanani tena. Jambo ambalo lilidhihirika ni kuwa elimu hii iliwasifu wazungu waliofika Afrika ya Mashariki kwanza kama vile Carl Peters, David Livingstone, Rebmann miongoni mwa wengine. Haieleweki ni kwa nini mtu kama Carl Peters alisifiwa sana hata baada ya kuwanyanyasa Watanzania wengi. Hata hivyo Waafrika wameweza kufaidika kutokana na elimu ya kigeni katika nyanja za maendeleo ya kiufundi.

J. Mbiti (Ibid) yuasema kuwa :

Jukumu la kufundisha hivi sasa linachukuliwa na walimu na shule kutoka kwa wazazi na jamii Vitabu ndivyo vinavyosomwa na wala si elimu tena ambayo inawaandaa vijana kwa utu uzima na kazi za siku za baadaye. 11

(Tafsiri yetu)

Haya mawazo kuhusu elimu yana ukweli kwa kiasi kikubwa kwani ni elimu ambayo imepoteza jukumu lake la kukuza na kuendeleza utamaduni wa Mwafrika. Elimu hii inawafanya baadhi ya watu kufikiria ya kuwa wao ni bora zaidi kuliko wale hawakukipata hicho kisomo.

Kwa sababu ya elimu ya kisasa wanafunzi wa kike wanahiari kutatiza mimba ili wapate kuendelea na elimu yao.

E. Kezilahabi (1971) anasema:

> Tunasikia ya kwamba siku hizi wasichana wengi wanaosoma wanafanya hivyo ili wapate kuendelea na masomo yao. Wanapenda masomo zaidi kuliko watoto. 12

Tunaona namna mama Rosa Mistika hapa anavyolalamika juu ya watoto wa siku hizi kupoteza maadili ya jamii kwa kunyonga vijitoto vyao kwa sababu ya elimu. Jambo jingine ambalo latokana na hayo ni pesa, ambazo zimeingia katika shule za siku hizi kutoka kwa wale wanaofanya kazi na hivyo kuwapotosha wanafunzi wa kike katika viwango vyote vya elimu. Mbeko hazipo tena miongoni mwa watoto wa siku hizi.

Jambo ambalo linasisitizwa na ambalo vijana wa siku hizi wanapaswa kujiuliza kabla ya kuzikubali hizi tamaduni za kigeni ni, je zote zinafaa ? Ikiwa zote hazifai basi hapana haja ya kuzichukua zote. Wazichukue zile ambazo zitawafaa tu. Tunakubaliana na Shaaban Robert anaposema ya kwamba hatavumilia yale ambayo hayafai tena katika utamaduni wake. Atakubali mabadiliko ndiyo, lakini yawe yanayofaa.

**MALEZI.**

Jamii nyingi za Afrika Mashariki zilikuwa na jukumu la kuwalea watoto, wazee na pia wale watu katika jamii ambao hawakuwa

wakijiweza kwa namna moja au nyingine kama vile vilema na wagonjwa.

Kayongo-Male (1985) anasema :

> Malezi na heshima kwa wazee hasa wazazi wa mtu yalikuwa mambo muhimu sana. Mtoto alihitajika kumheshimu mzee sana. Usaidizi wa kila namna ulitakikana kupewa wazee ili miaka yao ya uzeeni isiwe na matatizo yoyote. 13
>
> (Tafsiri yetu)

Tumekwisha kutaja ya kuwa watoto walikuwa muhimu sana katika jamii. Mtu aliheshimiwa kwa kuwa na watoto wengi. Inaeleweka pia kwamba watoto wangeachwa bila mlezi labda baada ya kifo cha mzazi Lilikuwa jukumu la familia kubwa kuwalea na kuwatunza hao watoto. Wazazi wa kambo na jamaa wengine walitarajiwa kuwa wa manufaa kwa watoto hao ili na wao wafurahie maisha.

Katika sehemu nyingi za Afrika mke wa mtu alipokufa, mume aliruhusiwa kuoa mke mwingine au kuchukua dada ya mke wake ili awalinde wale watoto dada yake aliacha. Hii ilisaidia katika kuhakikisha ya kwamba hao watoto hawakupata taabu chini ya mtu ambaye hakuwa na uhusiano wa kidamu.

Kwa sababu wazazi ndio waliokuwa wakikaa na watoto wao kwa muda mrefu walitarajiwa kuwalea watoto wao na kuwafundisha tabia zinazofaa katika jamii ile. Waaidha wanajamii walikuwa na jukumu la kusaidia katika kuwaelemisha hao watoto ili wasiiletee jamii aibu. Hivyo basi utovu wa nidhamu miongoni mwa watoto halikuwa

jambo la kawaida kwa sababu aibu haingewafika wazazi tu bali jamii yote.

Hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa lakini kama tunavyoendelea kuona ukoloni ulileta mabadiliko makubwa. Wazazi walinyang'anywa kazi ya malezi na waalimu wakachukua huo wadhifa. Aghalabu waalimu husahau jukumu lao na kuwaacha watoto kujiingiza katika mambo maovu. Watoto wanapofahamu ya kuwa hawako karibu na wazazi wao hasa wale ambao wako katika shule za mabweni, hufanya mambo ambayo wazazi wao hawangewaruhusu kufanya. Vijana hutoroka shule usiku na kwenda kushiriki katika anasa mijini ambako madhara huwapata. Wasichana hupata mimba, magonjwa na madhara mengine mengi.

Kutokana na shule za mabweni visa vya unajisi vimezidi sana Hii ni kwa sababu wasichana hawana ulinzi imara na wanaowanajisi wamepoteza mbeko ambazo zinatakikana kuwaongoza. Maafisa wa serikali, wenye magari na mali nyingi wanavitumia hivyo vifaa kuwadhalilisha wasichana. Umaskini ambao unadhihirika katika familia nyingi za kiafrika umewafanya wasichana wakubali kuuza hata mili yao angalau hadhi yao ipande. Haya yote yanaishilia katika uozo ambao ni wanambeko tunaoweza kuuzuia kwa njia ya kuwaelemisha wanajamii juu ya hatari zake.

Katika familia za mijini wakati mwingine baba na mama wote wanafanya kazi kwa hivyo jukumu lao la malezi hawalitimizi. Imekuwa ni mayaya ambao wameachiwa hilo jukumu. Mayaya wanaoajiriwa hutoka sehemu tofauti tofauti na ambazo zina utamaduni tofau-

ti pia. Kwa vile huyo yaya hana uhusiano wowote na huyo mtoto hajali atakavyokua. Huenda atampiga, akamuacha akiteseka kwa njaa na mambo mengine maovu ambayo mwenyewe lau angekuwepo hangeyaruhusu. Bila malezi bora mtoto hukua katika hali isiyostahilika. Ni jukumu la wazazi kuhakikisha ya kuwa watoto wao wanalelewa vyema ili wawe raia wema baadaye.

Maswala kama haya ndiyo yanayoshughulikiwa na wanajamii wa kimbeko ambao hupendekeza waja kuwatendea wenzao wema. Diwani ya M.M. Amir ya <u>Tungo Zangu</u> inalishughulikia hili swala la malezi kwa kina na hapana shaka ya kuwa hii sehemu ni msingi bora kwa uhakiki wa hiyo sehemu.

## UONGOZI.

Sehemu hii ni muhimu katika uhakiki wetu kwa sababu inatuonyesha uongozi uliokuwepo na ambao ulifuata maadili fulani na kwa hivyo kutuwekea misingi ya kuwahakiki viongozi ambao tutakumbana nao katika kazi za M.M. Amir.

Hapo awali kila kabila lilikuwa na kiongozi wa aina fulani Kulikuwa na ufalme katika baadhi ya makabila kwa mfano Wahehe, Wachagga. Makabila mengine nayo hayakuwa na utawala huo kwani watu walijiona kuwa sawa. Sababu moja iliyowafanya wahisi hivi ni kuwa walikuwa watu wa kuhamahama. Makabila haya ni kama vile Watindiga, Wanadza na wengine wengi.

Wakoloni walipokuja waliwadharau wazee na viongozi wa kienye-

ji na wakaingiza mifumo yao ya uongozi. Ijapokuwa hata katika jamii za kijadi viongozi walitunukiwa zawadi, katika jamii ya kisasa haja na tamaa ya kuwa tajiri na kumiliki mali nyingi imekuwa ikiwasukuma watu wengi kutaka kupata utawala. Hii inadhihirika kupitia pale majaribio mengi hufanywa na majeshi na raia ya kutaka kuzipindua serikali zao. Baadhi ya nchi ambazo zimewahi kushuhudia majaribio kama haya ni pamoja na Somalia, Sudan, Kenya Nigeria miongoni mwa nchi nyingi za Afrika.

Viongozi wengi walioko hujali tu maslahi yao na kuwaacha wananchi wakiteseka kutokana na hali ngumu za kiuchumi. Ni hao viongozi wanaopaswa kulaumiwa kwa kiasi kikubwa. Mtizamo kama huu utatusaidia kuelewa namna M.M. Amir anavyolishughulikia swala la viongozi na maovu wayafanyayo katika jamii zao.

DINI.

Kipengee cha dini kitatusaidia katika kufikia uamuzi juu ya M.M. Amir kuhusu mtizamo wake wa maisha. Kutokana na hii sehemu tutaeleza ikiwa anaongozwa na maadili ya kiislamu au maadili ya jamii yake.

J. Mbiti (Ibid) anasema kuwa kila jamii iliamini katika mambo ya dini na mambo mengi katika ile jamii yalihusiana na dini. Kayongo-Male (Ibid) yuadai kuwa wakati Uislamu na Ukristo ulipoanza kusambaa katika sehemu mbalimbali za Afrika, watu walipoteza baadhi ya imani zao katika dini za kitamaduni ijapokuwa baadhi ya

hizo imani zilihifadhiwa na kuchanganywa na hizi dini mpya.

Wengi wa Waafrika hususan wa pwani ya Afrika walipoathiriwa na Uislamu waliuchukuwa na kuufanya wao. Wengi walisilimishwa na tangu wakati huo imani zao zikawa za dini ya Kiislamu. Hali kama hii inawafanya wengi kusahau ya kuwa hata dini ya Kiislamu ni ya kigeni na badala yake ni Ukristo tu unaoshambuliwa. Ukristo ulienea katika Afrika karibu wakati mmoja na ukoloni na inaaminika kutokana na historia yetu kuwa wamishonari ndio waliokuwa miongoni mwa watu wa kwanza kuwa na uhusiano na Waafrika kutoka nchi za magharibi. Hatuwasahau wavumbuzi kama vile David Livingstone katika Afrika mashariki na kati. Aidha wamishonari waliofika Afrika Mashariki wa shirika la C.M.S Ludwig Krapf na wengine wengi wa U.M.C.A ambao walifika kupitia mwito wa David Livingstone. Inafahamika ya kuwa katika Afrika ya watu weusi, wamishonari ndio waliokuwa watu wa kwanza kuanzisha shule na athari za hizi shule tumezijadili kitambo na katika sura zifuatazo tutaona namna hizo athari zimewapotosha wanajamii.

Tunaloweza kusema ni kuwa utamaduni mpya umeweza kuchukuliwa na Waafrika kutoka hizi dini kama vile taasisi ya ndoa ambayo tumekwisha irejelea. Baadhi ya madhehebu yamepinga mila za Waafrika na kuziita za kishenzi. Mfano ni kama tulivyotaja hapo awali ya kuwa baadhi ya madhehebu yanapinga mitala.

Dhana ya majaaliwa imejitokeza sana katika dini za kisasa ambapo watu huamini ya kuwa maisha ya sasa ijapokuwa wengine wataayafurahia na kupata fahari ilhali wengine wanateseka kutokana

na umaskini, hayo yote ni mapenzi ya mwenyezi Mungu na kwamba watu wasife moyo kwani maisha baada ya kifo cha humu duniani ni bora zaidi mradi tu roho zetu hapa duniani ziwe safi. M.M. Amir yualekea kuwashauri watu kustahimili shida zote zinazowapata kwani ni takdiri ambayo haina kinga.

Hata hivyo, J. Mbiti anaonyesha mtizamo tofauti anaposema ya kuwa wengi wa Waafrika waliamini kuwa maisha ya sasa ndiyo yaliyokuwa bora na wala sio yale ya baada ya kifo.

Tunapaswa hata hivyo kutambua kuwa hizi ni imani tu na kwa hivyo ukweli wake utaendelea kutegemea mikabala ya watu.

KIFO.

Binadamu amekubali ya kwamba kifo ni kitu cha kawaida maishani. Hata hivyo kuna baadhi ya watu ambao hukihusisha na sababu kadha. Wengine huenda wakaamini ya kwamba urogi ulihusishwa katika kifo cha mtu. Wakati mwingine hudaiwa ya kwamba waliokufa huwa wamekasirishwa na mmoja wanajamii na kwa hivyo kama adhabu kwa jamii wakadai mmoja wao. Waaidha huaminika miongoni mwa jamii kama vile Waluhya wa magharibi ya Kenya kuwa ikiwa mtu aliyekufa hakufanyiwa yote yahitajikayo wakati wa mazishi, huenda akadai mmoja wa watu katika familia yake. Anaweza kupitia kwa ndoto akatuma habari ya kuwa anataka mmoja wa watoto wake.

Jamii za Ulaya mara nyingi hazijali kifo sana. Katika hizi



UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

jamii mtu akisha kufa hana tena faida. Wanachojali ni urithi ulioachwa na yule aliyekufa. Katika hizi jamii sherehe za mazishi sio muhimu kama ilivyo Afrika katika baadhi ya jamii. Siku hizi baadhi ya Waafrika wameathirika kiasi cha kutojali kifo.

Wanamajaaliwa nao wanaamini ya kuwa kifo ni amri ya mungu na kuwa kila mwana-wa-Adamu ataipitia hiyo njia. Siku yako ikifika hakuna kinga hata wale madaktari wanaosifika hawawezi kuyaokoa maisha yako. M.M. Amir katika kazi zake anapowaliwaza waliofiwa tunaona mtizamo kama huu ukijitokeza.

**2:4:0 BIASHARA YA UTUMWA .**

Biashara ya utumwa ndicho chanzo cha watu weusi wengi katika nchi za Uropa kama vile Uingereza, Ufaransa na vile vile sehemu nyingi za Amerika. Biashara hii ilifana sana hadi ilipofikia wakati dunia nzima iliposadiki ya kuwa biashara hii iliwadhalilisha watu sana na kuwa hakuna binadamu aliyestahili kuteswa kwa namna ambavyo watumwa walikuwa wakinyanyaswa kinyama.

Katika Afrika Mashariki Waarabu ndio waliohusika sana na hii biashara. Waafrika wengi walikamatwa kutoka sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki na kuuzwa katika soko la watumwa huko Unguja.

Ulikuwa ni udhalimu usioelezeka chini ya Mwarabu. Familia nyingi zilibomolewa kutokana na hii biashara. Watu waliwaua kinyama na katika safari zao za kwenda walikotakikana waliteswa na wengi walikufa kabla ya kufika. Mara nyingi safari yao iliis-

hilia Arabuni au India.

Mnkondo...[et al] (1971) anasimulia kisa cha kusikitisha kuhusu mateso ya mtumwa mmoja :

> Hata inafahamika ya kuwa wakati mmoja, mtoto wa sultan alimwambia baba yake kuwa hajui namna bunduki inavyoua. Sultan akaamuru wamwite Mwafrika mmoja na kumsimamisha mbele yake na kumpiga risasi. Halafu Sultani huyo akamwambia mwanae `hivi ndivyo bunduki inavyoua'. Baadaye akamuru vijakazi vyake viondoe maiti kwa haraka.14
> (Tafsiri yetu).

Hivyo ndivyo Waafrika walivyoteswa. Na hii ndiyo sababu hii sehemu ni muhimu katika utafiti wetu maanake inaangazia yale M.M. Amir anashughulikia katika Utenzi wa uhuru wa Tanganyika.

Jambo ambalo lafaa kutajwa hapa ni kuwa wazungu walikuwa wakiunga mkono biashara ya utumwa kwa sababu watumwa wengi walipelekwa kufanya kazi katika mashamba yao. Ni wakati walipogundua ya kwamba hawakuwahitaji tena ndipo walianza kuipinga biashara hii. Hii ilitokana na mapinduzi ya viwanda yaliyotokea karne ya kumi na tisa. Walikuwa wamegundua njia mpya za kufanyia kazi zao kwa haraka.

Kwa vyovyote vile biashara ya utumwa ilipoingia katika jamii za Kiafrika, iliacha madhara ambayo hayangeweza kusahaulika kwa haraka. Jambo linalosikitisha zaidi ni kuwa baadhi ya watu walioathiriwa na utumwa hivi kwamba miaka mingi baadaye walikuwa wakiwanyanyasa wenzao kiutumwa.

## 2:5:0 VITA VYA UKOMBOZI.

Kuna mabadiliko makubwa yaliyotokea Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla katika karne ya kumi na tisa. Ni wakati huo huo ambapo mabadiliko makubwa zaidi yalikuwa yakifanyika huko Uropa kutokana na mapinduzi ya viwanda. Kote duniani uwezo wa Uropa kivita na kiuchumi ulikuwa ukiwalazimisha watu wengi kusalimu amri na kutawaliwa kikoloni na wazungu. Nchi kadhaa za Kiulaya ziligawana janibu ya Afrika Mashariki.

Kipengee hiki ni muhimu sana katika tasnifu yetu kwa sababu kinatalii juhudi za Waafrika wa Tanganyika katika kujitafutia uhuru kwa njia ya vita. M.M. Amir amelishughulikia hili swala katika Utenzi wa uhuru wa Tanganyika na kwa hivyo imetupasa kuchunguza hali ilivyokuwa Tanganyika Kabla ya kuingilia uhakiki wa maudhui, M.M. Amir anayojitokeza nayo katika sura ya tatu.

Ni chini ya uongozi wa Wajerumani ambapo wakazi wa pwani ya Afrika Mashariki hususan Watanganyika walipoanza kuupinga utawala wa wakoloni. Hii ni kwa sababu ya yale mateso wenyeji walikuwa wakipata kutoka kwa wakoloni. Utetezi wa wenyeji ulianza mwaka wa 1888. Waasisi wanaotajwa ni Abushiri bin Salim, mwenyeji wa asili ya kiarabu na Bwana Heri, Mtanganyika kindakindaki. Ingawa hawa watu walishindwa, ni dhahiri kuwa walikuwa wameonyesha kutopendezwa kwao na utawala wa kikoloni. Mnamo mwaka wa 1889,Desemba huko Pangani, Abushiri alinyongwa, naye Bwana Heri akajisalimisha kwa Wajerumani mnamo Aprili 1890.

Vita vingine vilivyofuata hivi vilikuwa vile ambavyo viliongozwa na Mkwawa wa Wahehe.Mkwawa alitaka awe na uhuru wake lakini alitarajia kulipata hili bila vita. Kwa bahati mbaya hili halingewezekana. Wajerumani na Waafrika walikuwa na uadui kati yao ambao haungemfanya yeyote kati yao kumuamini mwenzake. Mkwawa alipowatuma wajumbe wake kwenda kufanya mkataba na Wajerumani,Wajerumani hawakuwaamini na badala yake wakafikiria ya kuwa hao watu walikuwa wamekuja kwa sababu ya vita. Matokeo yake ilikuwa ni kuwanyonga hao wajumbe wote.

Mkwawa alipozipata hizi habari hakuwa na jingine ila kujiingiza vitani. Katika hivyo vita Wajerumani mia mbili na tisini waliuawa.Kwa muda fulani Mkwawa alipigana vita vya msituni hadi alipolemewa na maradhi na upweke.

Mkwawa alihiari kujiua kwa risasi badala ya kuteswa na Wajerumani. Kifo cha Mkwawa kiliashiria mwisho wa pingamizi kwa Wajerumani.

**VITA VYA MAJI MAJI.**

Kutokana na gharama kubwa ya kutawala, Wajerumani walisisitiza maendeleo ya kiuchumi na kwa kufanya hivi wakawa wanajaribu mbinu kadhaa ambazo zingeufaulisha mradi wao. Kwanza kabisa walianzisha mashamba ya mimea, pili, waliwaajiri Waafrika wengi na tatu,waliwahimiza au kuwalazimisha Waafrika kukuza mazao ili waweze kulipa kodi yao.

Historia inadai ya kuwa maisha chini ya utawala wa Wajerumani yalikuwa magumu sana. Tutajaribu kuona namna M.M. Amir alivyoyaweka kisanaa katika sura inayofuata. Kulikuwa na kazi ambazo zilitakikana kufanywa. Lakini namna Y. Halimoja (Ibid) anavyosema hakuna kazi ambayo ilifanywa kwa hiari. Kazi zilikuwa za lazima. Watu walichukuliwa kuwabeba Maafisa wa serikali kwenye machela na waliobeba hawakutakikana kutembea polepole au kujikwa halafu aliyebebwa aanguke. Kulikuwa na kazi za kulima barabara, kulikuwa vile vile na kazi za kulima mashamba ya wazungu, walowezi au serikali. Hizi na kazi nyingine nyingi zilifanywa katika hali ya kusikitisha.

Hakuna hata wakati mmoja Mjerumani alipomheshimu Mwaafrika. Daima alimwita swaini (Nguruwe). Maisha ya watu wa Tanganyika yalikuwa ya kusikitisha sana kwa sababu wengi wa wazee waliishi katika hali ya wasiwasi tu.

Y. Halimoja (Ibid) anasema:

> Kati ya mambo yote yaliwasumbua na kuwaudhi sana wazee wetu shaka lililokuwa kubwa zaidi kuliko yote ni kodi waliyotakiwa kutoa bila kueleza matumizi yake. **15**

Wakati wa watawala wa kikoloni kulikuwa na aina mbili za kodi Ya kwanza ilikuwa kodi ya nyumba na halafu mnamo 1905 kodi ya kichwa ilianzishwa. Ilikuwa ni lazima mlipa kodi kutoa fedha taslimu- rupia tatu. Hii fedha haikuwa rahisi kwa Watanganyika ambao wengi walikuwa wakulima. Ulifika wakati wote walioshindwa kulipa walikuwa na uhuru wa kuchagua aidha kupigwa viboko 25

(hamsa kwa Ishirini) ili wahesabiwe kuwa wamekwisha kulipa kodi ya mwaka huo wote au wachukuliwe kufanya kazi ngumu katika mashamba ya pamba au mkonge. Si ajabu kugundua ya kuwa watu walipendelea kupigwa viboko maana ilikuwa ni kwa siku moja tu. Ajabu ni kwamba baada ya kuchapwa hivyo mtu alitarajiwa kusimama na kumshukuru aliyemchapa.

Mateso kama haya ndiyo yamewafanya wanasanaa wengi kuyarejelea yaliyopita ijapokuwa yalitokea miaka mingi iliyopita na tunamuona M.M.Amir hasa katika <u>Utenzi wa uhuru wa tanganyika</u> akipania kuikumbusha jamii yaliyopita.

Wazee hawakuheshimiwa kwa kuchapwa hata mbele ya watoto wao. Hata hivyo kama tulivyosema ni upanzu wa pamba ambao ulileta shida nyingi. Ardhi iliyochaguliwa kwa upanzi wa pamba haikuwa nzuri na mara nyingi mavuno hayakuwa mazuri.

G.C.K. Gwassa (1967) anaelezea mateso ya Watanganyika wakati huo:

> Wakati wa kupalilia ulikuwa na mateso mengi. Kwenye mstari wa mbele wafanyi kazi waliwekwa, nyuma yao alifuata mnyapara na kazi yake ilikuwa kuwachapa wafanyi kazi viboko. Nyuma ya Nyapara alisimama jumbe na nyuma ya jumbe ni Bwana kinoo mwenyewe aliyesimama. Na ikiwa Bwana kinoo angeona alama wayo alimchapa viboko yule jumbe kweli kweli. Mnyapara kazi yake ilikuwa kuwachapa wafanyi kazi wakithubutu kusimama. **16**
>
> (Tafsiri yetu)

Haya yalipozidi na mengine mengi Wazaramo walikataa peni tatu na ndururu walizopatiwa kwa kazi yao ya mwaka wa kwanza. Ilip-

ofika Julai, 1905 wafanyikazi waliamua kuanzisha vita. Tarehe 31 Julai, Wamatumbi waliwafukuza wageni wote na Akida wao waliyemchukia kutoka sehemu yake. Na kwa hayo vita vya maji maji vilikuwa vimeanza.

Kinjeketile, mganga mashuhuri aliyekuja na dhana ya maji ndiye aliyewaidhinisha Wazaramo na Wamatumbi kuanza vita. Waliamini ya kwamba maji yangewakinga wapiganiaji uhuru dhidi ya marisasi ya Wajerumani.

Wengi wa Watanganyika walipoteza maisha yao lakini hivyo vita vilikuwa muhimu sana kwa Watanganyika . Walitambua ya kuwa silaha zao duni hazingefaa. Hawakuwa na uongozi bora na pia hawakuwa na umoja. Tunaona kwa mfano Wangoni walipojiunga vitani walipigana kama kabila. Zaidi ya watu elfu mia moja na ishirini walipoteza maisha yao.

Hata hivyo tutakubaliana na wataalamu wanaodai ya kuwa vita vya majimaji vilikuwa funzo kubwa kwa Wajerumani na wenyeji. Wajerumani walitambua ya kuwa bila haki hapangewezekana kuwa na amani. Wenyeji nao walitambua kuwa umoja na uongozi bora ni jambo muhimu katika jitihada zao za baadaye. Ilikuwa rahisi kwao kupanga mambo yao chini ya uongozi madhubuti kama uliodhihirishwa na Julius K. Nyerere katika kazi za M.M. Amir.

Mbali na vita Watanganyika walijaribu mbinu zingine katika upiganiaji wa uhuru wao. M.M. Mulokozi (1976:25) anadai ya kuwa ushairi ndicho chombo kilichotumiwa sana kati ya vyombo vya fa-

sihi wakati Watanganyika walipokuwa wakipigania uhuru kutoka kwa Wakoloni. Sababu kubwa ni kuwa huu ndio utanzu uliohitajika kwa mapambano haya kwani mashairi yaliweza kuandikwa kwa haraka zaidi kuliko riwaya au tamthilia.

Fauka ya haya aliyoyasema Mulokozi (Ibid) tungependa kutaja ya kuwa hayo mashairi haikuwa lazima yaandikwe bali yangeweza hata kughaniwa tu katika sherehe fulani na tamasha za wanajamii.

Viongozi kama vile Nyerere walitumia mbinu ya mahojiano na tawala mbalimbali katika kupigania uhuru wa Tanganyika.

**2:6:0 VYAMA VYA KISIASA.**

Imedhihirika kutokana na yale tuliyoyaeleza kwenye (2:5:0) kuwa Watanganyika hawakutawaliwa na wakoloni kwa hiari yao. Kwa hivyo Waafrika walijaribu kila namna ya kujitafutia uhuru wao kwa kuwaondoa wakoloni. Mojawapo ya jitihada hizo ilikuwa uundaji wa vyama vya kisiasa ambavyo vilipigania uhuru wa wananchi.

Vyama vya kikabila ndivyo vilivyokuwa vya kwanza kuundwa na sehemu kubwa yavyo ilikuwa Dar -es -salaam - kwa shabaha ya kuwaunganisha watu wa kabila moja ili waweze kushirikiana. Ni wakati wa shida kama matanga ndipo vyama hivi vilikuwa vikizaa mawazo ya kuwa na umoja wa kitaifa.

Chama cha kwanza kuundwa Tanganyika kilikuwa cha T.A.A (Tanganyika African Association) mnamo mwaka wa 1927. Madhumuni ya T.A.A hayakuwa kupigania uhuru bali yalikuwa kupigania haki za

watumishi wa serikali waweze kuwa na hali njema ya maisha. Shughuli za chama hiki mwanzo mwanzo zilitetea hasa wafanyi kazi waliokuwa wakiishi mijini. Hata hivyo baada ya muda, shughuli zake zilienezwa hadi kwa wananchi wa vijijini. Rais wa kwanza wa T.A.A alikuwa Cecil Matola.

Baadaye kama anavyosema Y. Halimoja (Ibid) ni kuwa:

> Alikuwa Julius Kambarage Nyerere aliyeamua kukigeuza chama hiki kuwa chama cha ukombozi cha wananchi wa Tanganyika. 17

Mnamo mwaka wa 1953, Nyerere alichaguliwa kuwa Rais mpya wa T.A.A na ni yeye aliyezua wazo la kukifanya chama hiki kuwa cha kisiasa halisi na katika mkutano uliofanyika mnamo Oktoba 10, 1953, jina la chama hiki lilibadilishwa na kuwa T.A.N.U (Tanganyika African National Union).

**TANU :**

Ni muhimu kukishughulikia chama cha TANU kwa kifupi kwa sababu ndicho chama cha kisiasa nchini Tanganyika kilichopigania uhuru wa Watanganyika kutoka kwa wakoloni hadi walipoupata mnamo mwaka wa 1961.

Nyerere ndiye aliyekuwa Rais wake wa kwanza kilipoundwa mnamo mwaka wa 1954 mjini Dar-es-salaam.

Nyerere alizaliwa Butiana kijiji kilichoko karibu na Musoma mnamo mwaka wa 1922. Alipata masomo yake ya msingi Msoma na ya sek-

ondari, Tabora. Alisomea Diploma katika Chuo kikuu cha Makerere na baadaye akajiunga na chuo kikuu cha Edinburg ambako alichukulia masomo yake ya uzamili. Alipata shahada yake ya M.A mwaka wa 1952.

Ni wakati huu wa masomo yake ambapo aliweza kupanua mtizamo wake wa kisiasa kuhusu maswala yaliyokuwa yakiikumba nchi yake na Afrika kwa jumla kutokana na ukoloni. Ijapokuwa alikuwa ameelimika bado alitambua kuwa alikuwa mmoja wa wale waliokuwa wakitawaliwa kikoloni.

M.H.Y. Kaniki (1974) anasema:

> Ni kutokana na kuelewa kwake kwa <u>hali halisi ya mambo ya kisiasa</u> ndipo aliiona haja ya kubadili katiba ya chama cha T.A.A ambayo aliiona kuwa si toshelezi. [18]
>
> (Tafsiri na msisitizo wetu)

Nyerere akiwa kama Rais wa chama cha TANU alilifahamu jukumu lake na lile la wanachama wenzake kuwa la kutafutia nchi ya Tanganyika uhuru. Nyerere alifahamu pia umuhimu wa umoja wa watu wote katika kuleta mafanikio na akajitolea mhanga kama kiongozi mzalendo na mwenye maadili, kuwaunganisha watu kupitia chama cha TANU na vile vile akawahimiza wafanyakazi kuunda vyama vyao ili vikisaidie chama cha TANU katika malengo yake. Ni chama cha TANU ambacho katika kutafuta wanachama kutoka kwa Watanganyika wote kiliamua kuhimiza lugha ya kiswahili na mpaka wa leo kiswahili ni lugha muhimu nchini Tanzania. Ni lugha ya taifa na vile vile lugha rasmi.

Chama cha TANU kama vyama vingine kilijipatia jukumu la kuwashawishi watu wawe na imani katika mbinu zake na wakiunge mkono kwa vyovyote vile.

Nyerere alisafiri Ulaya mara kwa mara kuwatetea wananchi wake. Akiwa nyumbani alifanya ziara za sehemu zote za nchi na kuwapa moyo wale ambao hawakuwa na imani na kuwahakikishia wananchi juu ya jukumu la TANU katika kuwatetea. Aliitumia hii fursa katika kuchunguza yale matatizo ambayo chama cha TANU kingekumbwa nayo.

TANU ni chama kilichokumbwa na matatizo ya upinzani tofauti tofauti. Kwa mfano wale wakoloni ambao hawakuwa tayari kuiacha nchi ya Tanganyika. Kulikuweko pia na machifu waliokuwa wakitumiwa na wakoloni. Chama cha Masetla nacho kiliundwa ili kupambana na chama cha TANU. Hicho chama kilijulikana kama U.T.P ( United Tanganyika Party ).

Licha ya hiyo pingamizi, chama cha TANU kilijitahidi na kupata wafuasi wengi ambao walikuwa wazalendo hasa. Imedaiwa ya kuwa tofauti na nchi za Kenya na Uganda TANU kilikuwa chama cha kitaifa ambacho hakikutawaliwa na kabila moja lenye Nguvu. Kilikuwa ni chama ambacho hakikumbagua mtu yeyote.

Aidha chama cha TANU kilikuwa na viongozi ambao walikuwa tayari kuipigania nchi yao mathalan Nyerere. Hawa ni viongozi walieleta udugu katika chama na kwa hivyo hisia za kidini na kikabila hazikuruhusiwa kuwatenganisha wanachama.

Kiswahili kilitumiwa kama **Lingua Franca** katika kuwaunganisha wananchi wote wa Tanganyika. Kama anavyosema Kaniki (Ibid) kiliwafanya viongozi kukubalika kama viongozi wa Tanganyika badala ya wao kuonwa kama viongozi wa kikabila.

Pia chama cha TANU kilipata wafuasi au kuna wale waliowahurumia miongoni mwa wanachama wa umoja wa mataifa.

**2:7:0 SIASA YA UJAMAA .**

M.M. Amir ameandika mengi ya mashairi yake baada ya Azimio la Arusha ambalo ndilo lililozaa siasa ya ujamaa nchini Tanzania. Yeye kama washairi wengine walioandika miaka ya sabini walilitizama Azimio kama mkombozi mkubwa wa Tanzania. Tunaishughulikia hii siasa katika hii sura ili iwe kama msingi kwa yale M.M. Amir anayoyashughulikia katika baadhi ya mashairi yake.

Ilikuwa Januari tarehe 26 hadi 29, mwaka wa 1967 Halmashauri kuu ya Taifa ilipokutana mjini Arusha na kupitisha Azimio la Arusha ambalo ndilo lilikuwa tamko rasmi la chama cha TANU kuhusu siasa ya ujamaa na kujitegemea.

Hata kabla ya Azimio la Arusha, 1967 Nyerere alikuwa amewahi kulizungumzia swala la ujamaa kama anavyo sema Kaniki (Ibid). Katika makala yake 'Ujamaa' yaliyochapishwa mnamo mwaka wa 1962, Nyerere alijadili maswala tofauti tofauti ya ujamaa wa kiafrika bila kutaja wazi wazi kuchukuliwa kwa itikadi hii na chama cha

TANU. Jambo moja muhimu alilolitaja ni kwamba ujamaa ni imani.

Baadaye wakati chama cha TANU kilipoanzisha Azimio la Arusha ilikuwa katika jitihada yake ya kuangamiza unyonyaji na udhalimu Chama kilikuwa sasa kimeichukuwa njia ambayo ingewaongoza Watanganyika katika kujitegemea.

Kuna mambo muhimu ambayo Azimio la Arusha lilisisitiza. Kwanza lilidai usawa wa wananchi wote, kila mwananchi ana jukumu la kuchangia katika mipango ya maendeleo ya serikali kwa sababu serikali na nchi ni yao wote.

Kuhusu elimu Azimio liliamini katika elimu ambayo ingewafanya Watanganyika waweze kujitegemea na kwa hivyo masomo ambayo yangesisitizwa ni ya kilimo kwa sababu wengi wa Watanganyika walikuwa wakulima na kwa hivyo wale ambao hawangeendelea na elimu ya juu wangeweza kujitegemea wenyewe kutokana na yale ambayo walikuwa wamepata shuleni.

Azimio liliamua kuwa ingefaa zaidi ikiwa Watanganyika wangeishi kwenye vijiji vya ujamaa. Iliaminika ya kwamba serikali ingeweza kuwasaidia wananchi wakiwa pamoja kuliko wakiwa wametengana. Aidha iliaminika ya kuwa wananchi wakiwa pamoja wangeweza kufanya kazi kwa kushirikiana na hivyo basi kuboresha mavuno yao.

Serikali iliamini vile vile katika kutaifisha mali ya nchi ili kila mtu afaidike. Kutokana na huo uamuzi benki za biashara za kibinafsi ilibidi zitaifishwe kwa sababu serikali iliamini katika usawa. Haikutaka wengine wawe navyo na wengine wakose.

Swala la kazi nalo lilikuwa muhimu sana. Ilieleweka ya kuwa Watanzania walikuwa wakulima na kwa hivyo uvivu haungewafaa. Ilibidi kila mtu afanye bidii katika kazi ili kuleta mafanikio kwa nchi. Waliamini ni vizuri kusaidiana kutokana na jitihada zao na wala sio kutarajia tu misaada bila wenyewe kuonyesha nia ya kujitolea kikazi.

Kwa hivyo kutokana na hayo mambo Watanzania walitarajia kumng'oa adui wao mkubwa, umaskini. Kulikuwa vile vile na magonjwa na kutojua kusoma na kuandika.

Kwa vyovyote vile hayo yalikuwa malengo mazuri sana ambayo hapana shaka yangeleta ufanisi mkubwa kwa nchi ya Tanzania. Lakini je, Tanzania kama nchi ingeweza kukabiliana na hali halisi ya duniani bila msaada wa nje? Wataalam wengi wanaafikiana kuwa nchi ya Tanzania haikuwa tayari kwa hatua kama hizo ilizokusudia kutekeleza.

Nchi ya Tanzania kama alivyokiri Nyerere muasisi wa ujamaa, ilikuwa nchi maskini sana. Haingestawi bila misaada , ilihitaji misaada ambayo ingewasaidia wananchi ndiposa waweze kujitegemea.

Hayo yaliyodokezwa kwenye Azimio la Arusha yalikuwa mambo ambayo yangewezekana kimaandishi tu na wala sio katika hali halisi ya utenda kazi. Waaidha mengi ambayo yaliandikwa na washairi hayangeikomboa nchi ya Tanzania. Palihitajika hatua kabambe kuchukuliwa.

Imedaiwa ya kuwa swala la ujamaa halikukubaliwa na baadhi ya

Watanzania. Katika sura zinazofuata tutaona jinsi M.M. Amir anavyowasawiri viongozi wanafiki kuhusu swala la ujamaa. Ni kweli kuwa lilipotangazwa lilishangiliwa sana lakini baada ya muda ukweli halisi ulidhihirika ya kwamba hilo si jambo ambalo lingezungumziwa tu halafu lifaulu. Tunaweza hivi leo kulilinganisha Azimio la Arusha na masharti ya Shirika la pesa duniani (I.M.F) na banki ya dunia ambayo ijapokuwa ni mazuri, nchi za Afrika haziwezi kuyatekeleza bila wao wenyewe kuwasaidia katika kufanya hivyo. Matokeo yake ni mateso makubwa kwa Waafrika wengi walio maskini.

Hata hivyo hatuwezi kusema ya kuwa siasa ya ujamaa ilishindwa kabisa au ilkuwa mbaya. Tunalosisitiza ni kuwa nchi kama Tanzania haikuwa tayari kwa siasa ya ujamaa.

Miaka ishirini na mitano baadaye imedhihirika ya kwamba ujamaa hauna nafasi tena katika Tanzania. Kwa sasa siasa za vyama vingi ndizo ambazo zimeanza kuota mizizi na inaaminika ya kuwa hali nchini Tanzania ni mbaya sana kiasi cha kwamba kila mtu yuataka kufanya biashara ili ajitosheleze. Hali ya uchumi kwa jumla katika bara la Afrika ni mbaya sana. Hii imeleta umaskini na ubinafsi ndio ambao umeenea sana. Haiaminiki ya kwamba mtu atalitoa jasho lake ili kuwafaa wanajamii wote. Kila mtu yuapigania tumbo lake na familia yake..

## 2:8:0 HITIMISHO :

Katika hii sura tumeweza kuyashughulikia maswala ya kijamii ambayo kama tulivyosema katika utangulizi ni msingi kwa sura zitakazofuata. Mambo tuliyoyashughulikia yalikuwa ya kijumla lakini ni mambo ambayo mwanafasihi anayeandikia jamii ni sharti ayashughulikie.

Kutokana na uchunguzi wetu ambao ulitubidi tutafute data hata kutoka elimu jamii tumeweza kuonyesha jinsi jamii nyingi za Kiafrika zilivyokuwa zikiishi kabla ya majilio ya Waarabu. Uchunguzi wetu umetubainishia ya kwamba jamii ya Watanganyika ni moja katika jamii nyingi za Kiafrika kwa hivyo kwa kiasi kikubwa kuna mfanano katika baadhi ya mambo kutoka Dar-es-salaam hadi Lagos mji ulioko Afrika Magharibi.

Sura hii imeweza vile vile kutuonyesha jinsi maisha ya Waafrika wengi yalivyokuwa rahisi na ya kuweza kustahimiliwa na wanajamii wengi. Katika hali kama hiyo haikuwa rahisi kwa watu wa jamii fulani kuenda kinyume cha mbeko za jamii hiyo. Imetubainikia ya kwamba wale watu waliopewa jukumu la kuwaelemisha wanajamii walihakikisha ya kuwa wanalitimiza hilo jukumu lao. Kila mtu katika jamii husika alikuwa na wajibu wakuiletea jamii yake ufanisi. Visa vya ngoa na ubinafsi havikuwa vingi na iwapo kulikuwa na tatizo wazee wa jamii walihakikisha ya kwamba wamelitatua kwa njia ambayo haingeleta zogo kubwa.

Sura hii imeweza kudhihirisha kuwa mambo hayo yalibadilika kwa sababu ya muingiliano wa tamaduni mbili tofauti. Wakoloni walipofika Afrika Mashariki waliingiliana na Waafrika na matokeo

yake yakawa kuathiriana. Uchunguzi wetu uliweza vile vile kutuonyesha ya kuwa baadhi ya Waafrika walikengeushwa na matokeo yakawa uvunjaji wa kaida zilizokuwepo na ambazo kila mwanajamii alipaswa kufuata. Wakoloni walileta ubinafsi mwingi miongoni mwa Waafrika kiasi cha kwamba watu walianza kusahau jukumu lao la kuwafaa jamaa zao wengine ambao hawakufaidika kama apendekezavyo Tolstoy.

TANBIHI .

1. Tazama S.N. Eliuforo (1967).

2. J.H. Habwe (1993) "Tahaakiki ya Kusadikika" - hayajachapishwa.

3. S. Robert (1967).

4. H. Abdalla (1973).

5. Tazana C.K. Omari (1980).

6. Makala mengi ya Nyerere yanazungumzia utaifa na jinsi watu wa taifa fulani wanapaswa kuulinda na kuuhifadhi utamaduni wao.

7. Tazama F.Fanon (1967).

8. Tazama J.S. Mwakipesile (1974).

9. Soma Y. Halimoja (1977).

10. S.A.K. Mlacha (1988).

11. J. Mbiti (1969).

12. E.Kazilabahi (1971).

13. Soma K. Male (1985).

14. Mukondo (1971).

15. Kama 9 hapo juu.

16. G.C.K. Gwassa (1967).

17. Kama 9 hapo juu.

18. M.H.Y. Kaniki (1974).

## SURA YA TATU

### 3:1:0 UTANGULIZI .

Katika sura hii tutachunguza majilio ya Waarabu, Waingereza na Wajerumani Afrika Mashariki lakini tukijikita katika jamii ya Watanganyika. Tutaonyesha nia yao ya kuja Tanganyika na matendo yao ya unafiki ambayo yaliwaacha Watanganyika katika hali ya umaskini na mateso.

Tutaweza vilevile kuangalia jinsi Watanganyika walivyoamua kujikomboa kutokana na minyororo ya ukoloni na ile pingamizi waliyoikabili katika kulifikia lengo lao.

### 3:2:0 MAJILIO YA WAARABU NA MATESO .

Katika sehemu hii ya uhakiki wetu tunashughulikia majilio ya Waarabu katika Afrika Mashariki hususan Tanganyika. Sehemu hii ni muhimu kwetu kwa sababu itatuonyesha namna Watanganyika walivyopambana na wageni katika kupigania uhuru wao. Kuja kwa Waarabu kulikuwa na athari zake ambazo tumezishughulikia katika 2:3:1 na 2:4:0.

Wengi wa Waarabu waliofika Afrika Mashariki walikuwa wakimbizi kutokana na mzozo wa kidini uliokuwepo bara Arabu. Kwa hivyo haja yao kubwa ilikuwa ni kujitafutia makao mbali na vita.

Waarabu walikuwa wageni kama watu wengine wote waliofika Afrika ya Mashariki. Katika kujumuisha sababu zilizowaleta wageni Tanganyika, M.M. Amir anadai ya kwamba:

wageni wasingekuja
isipokuwa kwa haja
ya biashara za tija
Tamaa na manufaa. (ubeti wa 89)

Kwa M.M. Amir ni dhahiri ya kuwa biashara iliyowaleta wageni wengi huku ilikuwa na faida kubwa na kwa hivyo kwao ikawapatia tamaa ya kusafiri hizo safari ndefu mpaka walipofika huku. Ni dhahiri kuwa kama hiyo biashara haingekuwa ya manufaa hao wageni waliokuja hawangekuja.

Ili kuonyesha ya kwamba Waarabu walifika Afrika Mashariki kwa sababu ya shida na matatizo, M.M. Amir anasema kuwa:

Wa pili ndiye Mwarabu
Aliyetoka ghaibu

Kwa mashaka na taabu
Makwetu akaingia.

M.M. Amir anatutajia hizo sababu mbili kuhusu ujaji wa Waarabu. Ghaibu na hayo tunafahamu vile vile kuwa Waarabu wamehusishwa na sababu nyingine. Wamedai wanahistoria ya kuwa Waarabu walifika huku ili waieneze dini yao ya Kiislamu. Pia yaelekea Waarabu walifika Afrika Mashariki kwa sababu ya kisiasa wakiwa na nia ya kuwatawala wenyeji.

Katika huu utafiti wetu maoni yetu ni kuwa M.M. Amir anaipa sababu ya biashara uzito zaidi kwa sababu ni kutokana na hii biashara ndipo Watanganyika wengi waliteswa. Biashara hii kama anavyosema iliwaletea Waarabu faida kubwa hususan ya utumwa. Tunapozitoa sababu za majilio ya Waarabu au wageni kwa jumla itatubidi hata hivyo kutambua ya kuwa kulikuwa na sababu nyingi ambazo ziliwafanya hao wageni kuipenda janibu hii. Mazingara ya Afrika yaliwavutia wageni kufikia kiasi cha wao kuamuwa kuhamia huku. Mfano nzuri ni ule wa Seyyid Said aliyehamisha makao yake kutoka Muscat, Oman hadi Zanzibar. Tusisahau vile vile kuwa kulikuweko na sababu za kibinafsi zilizowaleta wageni.

Taswira ambayo M.M. Amir anatuchorea kuhusu Waarabu waliofika mwanzo kabisa ni ya watu wakarimu, watu ambao ni wazuri sana;

Alidumisha hekima
Kula na watu wazima
Majumbe na maulama
Kusudi apate njia. 98

Uvaziwe ni kilemba
Chenye hariri na pamba

Waliomuona wakamba
Wali katimilia 99

Mwarabu alifanya haya yote ili wenyeji wamdhanie kuwa yeye ni mtu mwema. Ukweli ni kuwa yeye alikuwa mtu laghai. Yote hayo aliyoyafanya yalitokana na hila zake ambazo ziliwapumbaza wenyeji na kumkaribisha. Kutokana na hizo mbinu zote alizoweza kuzizua Watanganyika na wenyeji wa Afrika kwa jumla walimkaribisha Mwarabu na kumfikiria kama mwenzi wao.

Kama tulivyotaja katika 2:4:0 Waafrika wengi waliteswa na Waarabu sana. Kukaribishwa kwa Mwarabu kuliwapatia fursa ya kuwanyanyasa wenyeji. Jukumu kubwa la fasihi ni kupinga dhuluma kama hii kufanywa na binadamu dhidi ya binadamu mwenzake. Taswira ambayo M.M. Amir anatuchorea ni ya kutupa mfano ambao unataka msomaji aingiwe na moyo wa ubinadamu na kuviona vitendo vya Waarabu kuwa vibaya na ambavyo kamwe havikustahili kufanywa. Fasihi nzuri ni ile inayoonyesha maovu yanayofanywa au yaliyofanywa na watawala au wenye mamlaka ili kuwakosoa na vile vile kuwapatia fursa viongozi walioko kutawala kwa busara. Kwa hivyo M.M. Amir anafaulu katika kutetea yale maovu yaliyofanywa kwa njia iliyo dhahiri na kuweza kueleza mengi katika beti chache sana.

Katika 3:4:0 tulizungumzia kwa kijumla juu ya mateso yaliyoletwa na biashara ya utumwa. Katika sehemu hii tunaona namna M.M. Amir anavyoyashughulikia na kutuonyesha namna Watanganyika waliyohusika na kutudhihirishia pingamizi lake kwa vile yote yaliyofanywa yalikuwa kinyume cha mbeko za jamii ya Watanganyika. Tunaw-

eza kusema kuwa athari zilizoletwa na Waarabu na hasa biashara yao ya utumwa zilikinzana sana na maadili ya jamii ya Watanganyika kufikia kiwango cha mtafaruku.

Itatubidi kila mara tunapozishughulikia kazi za M.M. Amir, kurejelea nadharia yetu inayohitaji upande wote wa swala kushughulikiwa. Tunaposema hivi tunamaanisha kufaulu kwa msanii kutaja hata yale maovu ili uwe mfano wa kuepukwa. Ikiwa tutachukua mwelekeo huu basi M.M. Amir amejaribu kwa kiasi kikubwa kutuchorea picha inayoonyesha mateso yaliyosababishwa na majilio ya Waarabu

Imedhihirika kutokana na yaliyosimuliwa katika <u>Utenzi wa uhuru wa Tanganyika</u> (Ibid) kwamba Waarabu walikuwa walaghai walioodhulumu wananchi wenzao kwa kuwafanya watumwa. Kulalamika kwa M.M. Amir kuhusu jambo hili kunatufanya na sisi tuhisi kama wanadamu na kukubaliana naye kuhusu hayo anayoyasema.

Nyakati za Waarabu, Waafrika wengi walichukuliwa na kusafirishwa hadi nchi za mbali ili wakafanye kazi katika hali za kusikitisha ambazo hapana binadamu anayestahili.

M.M. Amir anasema :

Hebu nanyi jaribuni
Muyatie akilini,
114 Hiyo ni kufuru gani
Mwenzio kumtendea

Kalipa pembe makamu
Kuliko ya binadamu
115 Asichelee jukumu
Kwa tamaa ya rupia

Wenye mimba matumboni
117 Wakazalia porini
Kwa mikwaju maungoni
Na twika zawangojea

Katika biashara, yeyote anayeifanya huwa na nia ya kupata faida. Kitu muhimu huwa ni faida. Tunaonyesha jinsi Waarabu walivyosahau thamani ya maisha ya binadamu. Waliwatesa Waafrika kwa tamaa ya rupia tu. Waafrika mbele ya Waarabu hawakuwa chochote. Rangi yao ilionwa kuwa duni kwa kila hali. Walidhulumiwa kwa sababu iliaminika kwamba chochote kuhusu Mwafrika kilikuwa cha kishenzi.

Na hata njiani kama tulivyodokeza hapo mwanzo ni kwamba yalikuwa mateso yasiyostahimilika - mijeledi hata kwa waja wazito. Inafahamika vile vile kuwa chakula walichopewa hakingeweza kuwafaa. Mizigo waliyoibeba katika hiyo safari ilihitaji nguvu. Ajabu ni kwamba ijapokuwa walinyimwa chakula, waliyotakikana kutimiza safarini ilipaswa yatimizwe bila pingamizi. Walitumiwa kama kielezo kwa watoto wa Waarabu waliotaka kujua namna mtoto anavyokaa tumboni mwa mwanamuke na vile vile jinsi bunduki inavyoua. Watanganyika na Waafrika wengine walinyimwa haki zao za kibinadamu za kuishi na jamaa zao, wakatenganishwa na wale waliowapenda na kupelekwa kule ambako hatima yao ni Mwarabu tu aliyeifahamu.

R. Mwaruka (1974) akisimulia kuhusu yayo hayo anasema kuwa hizi dhuluma zote kwa wananchi wa Afrika mashariki hususan Tanganyika, Mwarabu hakutishika, kwake ilikuwa furaha.

Anaendelea kusema ya kuwa hali ilikuwa mbaya sana katika kila

wilaya. Wananchi wa Tanganyika walitendewa ubaya na kila mji ukakumbwa na ukiwa. Nyumba zao zilichomwa na utumwani wakatiwa.

Waingereza walipowaomba Waarabu kuacha biashara ya utumwa walikataa. Said Bargash, sultan wa wakati huo alidai;

Hatuwezi kukubali
81 Utumwa kuuondoa
Hii ndiyo kazi yetu
Yenye manufaa kwetu
82 Twapata ukwasi wetu
kuuza na kununua. [1]

(Msisitizo wetu).

Hii ni dhuluma iliyoje ? Kwa watu kutajirika kutokana na damu na nguvu za binadamu wenzao. Si haki. Ghairi ya hayo, maslahi yao hao Waarabu hawakuyajali.

Kwa jumla majilio ya Waarabu pwani ya Afrika kupitia kwa jicho la msanii M.M. Amir yalisababisha mateso makubwa ambayo kwa kiasi kikubwa yalikuwa kinyume cha maadili yanayotarajiwa katika jamii yoyote ya kibinadamu. Biashara ya utumwa ilipata kusimamishwa kutokana na mabadiliko yaliyokuwa yakitokea katika bara la Uropa katikati ya karne ya kumi na tisa. Kulikuwa na maendeleo ya viwanda nyakati hizo ambayo tunakisia ndiyo yaliyowafanya wazungu kutoona haja zao (kazi za mikono). Ikiwa huu ndio ukweli basi tunaweza vile vile kukisia kuwa Waingereza walipokuwa wakiwataka Waarabu wasimamishe biashara ya utumwa ni kwa sababu hawakuwahitaji tena. Walikuwa wamepiga hatua za kimaendeleo kiufundi.

I.N Shariff (1989;21) anasema kuwa :

> '... watumwa waliopelekwa Amerika hawakupelekwa na Waarabu wala Waswahili; bali walichukuliwa na Wazungu, na katika wazungu hao wengi wao ni waingereza waliosh-shiriki mambo hayo maovu.'

Kwa hivyo ni dhahiri kuwa biashara ya utumwa haikuwashirikisha tu Waarabu. Watu wa rangi mbali mbali walishiriki. Hata hivyo katika sehemu hii tumejikita sana kwa shughuli za Waarabu katika hii biashara kwa sababu hao ndio M.M. Amir alishughulikia na pia ni kutokana na majilio yao na hiyo biashara yao ndio tunaona Watanganyika wakiteswa kinyama. Mbali na kumhukumu M.M. Amir kisanaa hatuna budi kuyaoanisha anayosema na uhalisi wa historia ya Waarabu katika Afrika mashariki ambayo inawachora kama wakoloni wa namna fulani ijapokuwa baada ya Wareno kufika, Waafrika wa pwani waliomba msaada kutoka kwa Waarabu ili wawasaidie katika vita vyao dhidi ya Wareno. Uamuzi huu una sababu zake lakini sehemu hiyo haina nafasi katika utafiti wetu.

## 3:3:0 WAINGEREZA NA WAJERUMANI TANGANYIKA .

Kabla ya Watanganyika kujinyakulia uhuru wao wa bendera mataifa mbali mbali yaliwatawala. Waarabu, Wareno, Wajerumani na Waingereza ni miongoni mwa wageni kutoka nchi za mbali waliofika Tanganyika kwa namna moja au nyingine kuwatawala wenyeji.

J. Illife (1968) anasema ya kuwa mabadiliko makubwa yalitokea katika Afrika ya mashariki karne ya kumi na tisa hasa Tanganyika. Baadhi ya sehemu za nchi ziliachwa katika hali mbaya kutokana na biashara ya utumwa. Ni wakati huo huo ambapo wazungu walikuwa wakiingia sehemu nyingi za Afrika.

Wajerumani walianza kuitawala nchi ya Tanganyika baina ya 1884 na 1898. Ujerumani ilitawala Tanganyika kutokana na mikataba isiyo ya kihalali iliyofanywa baina ya Carl Peters na baadhi ya machifu wa sehemu za kaskazini mwa Tanganyika.

Ni dhahiri ya kuwa ni kuja kwa hawa wazungu, - Wajerumani na Waingereza ndiko kulikoleta haja ya Watanganyika kupigania uhuru wao. Kwa hivyo sehemu hii ni muhimu sana kwa sababu ndiyo inayotupatia sababu ya uhuru wa Tanganyika.

M.M. Amir akizungumzia kuhusu Wajerumani anataja namna waliyokuja na mbinu ambazo zilikusudia kuwafaidi Watanganyika ;

Vitendo vya uhalifu
Na mambo maharibifu
Alifanya pungufu
Uasi ukapungua

Reli kutoka mzizima
Mpaka huko kigoma
Katandika kwa gharama
Kwalo tajishukuria

Ndiyo, haya yote walifanya. Nchi ikawa tulivu na hata reli wakazitengeneza. Lakini je haya waliyafanya kwa sababu ya Mtanganyika ? Ukweli ni kwamba wakoloni walipokuja Afrika walitaka kuwatawala wenyeji na pia kuleta baadhi ya wananchi wa huko kwao

kuja kuishi katika Afrika kama masetla. Hali za mawasiliano na uasi ulipunguzwa ili umfae mtawala na vile vile walowezi waweze kuwa na imani katika hizi koloni. Tufahamu vile vile kuwa wakoloni walitaka kuzipunguzia nchi zao mzigo kwa kuwahamisha baadhi ya wananchi wa nchi za ng'ambo hadi Afrika. Kwa hivyo yote waliyoyafanya Wajerumani yalikuwa ni ya kuwanufaisha wao wenyewe. Reli walizozitengeneza zilikuwa za kuwafaa katika usafirishaji wa bidhaa zao.

Tukiacha hayo waliyoyafanya kwa manufaa yake katika nchi ya Tanganyika, M.M. Amir anasema kuwa siasa ya Wajerumani haikuwa bora kuliko ile ya Waarabu. Katika uongozi wao, Waafrika waliteswa kupita kiasi. Mbele ya Mjerumani Mwafrika hakuwa kitu :

Tabia yake yabisi
Kwa kemeo na matusi
141 Akatuita Mafisi
Nasi tukavumilia

Kakaza watu minyoo
142 Mpaka ndani ya koo
Akatungenza choo
Vinywani akatunyia

Kwa kweli ikiwa binadamu yuaweza kufanywa hivi basi ni dhahiri kuwa Wajerumani hawakumthamini kamwe Mwafrika. Rangi ya Mwafrika ilimfanya aonekane kama mavi mbele ya mzungu licha ya kuwa alikuwa kwao alikozaliwa :

Kacharaza watu mboko
Kwa ukali na vituko
144 Hapakuwa na kishiko
Wengi wakamchukia

Mbishanaji ni nani
145 Mzungu na Afrikani
Kusimama hakamani
Mwenzi kupata njia

Yote haya Watanganyika waliyapitia. Ni chini ya utawala wa Wajerumani ambapo Watanganyika wengi walipoteza maisha yao kupitia vita vya ukombozi. Vita vinavyosifika sana ni vya maji maji vya 1905-1907 (rejelea 2:5:0). Waafrika hawakukubali watawaliwe na Wajerumani bila pingamizi. Mateso yalipozidi Waafrika waliungana na kupigana vita vikali. E.N Hussein (1969) katika tamthilyake ya Kinjeketile anayaeleza haya kwa uzuri sana. Wengi katika vita vya maji maji walikataa kusalimu amri wakiona ya kuwa vizazi vya baadaye vingewalaumu daima kwa kuwakubalia wageni kuwatawala na kuwanyanyasa.

Mbele ya Mjerumani, Mwafrika hakuwa na haki,sheria iliyokuwepo ilimfaa tu Mjerumani. Mwafrika angeadhibiwa tu hata na askari, hapakuwa na haja ya kumpeleka Kortini . Askari yeyote wa kijerumani alikuwa na huo uwezo.

Chini alitukanyaga
148 Akatufanya mizoga
Heri jani la uyoga
Kitemo laweza tiwa

149 Na wendapo kushitaki
Katu huipati haki
Badili yake hihaki
Uzidi kuongezewa

Katika huu mkabala tunamuona M.M. Amir akipania kutekeleza wajibu wa Mwanafasihi ambaye hapaswi tu kushangilia viongozi wake bali na hata kushtumu maovu ambayo wanayafanya. Tutatahadharisha

hata hivyo ya kuwa labda haya yanasemwa naye kama Mtanganyika aliyekuwa akililia nchi yake.

M.M. Amir anatueleza yale yaliyotokea baada ya vita vya kwanza vya dunia ambavyo vilikuwa kati ya Wajerumani na Waingereza. Jambo ambalo tunaweza kulipata katika vita vya 1914 - 1918 ni kuwa Waafrika wengi wa Afrika mashariki waliingizwa katika vita ambavyo havikuwahusu. Wengi walipoteza maisha yao. Na juu ya yote udongo wa Watanganyika ukafanywa ndio uwanja wa vita vikuu duniani :

Palizuka nuksani
Mngereza na jerumani
153 Wakatiana nguvuni
hozi kuigombania

Inakuwa muhimu kwa M.M. Amir kuvitaja hivi vita kwa sababu mbali na yale mateso yaliyoletwa, Wajerumani walishindwa na Waingereza na kwa hivyo baraza la kimataifa likaipatia Uingereza mamlaka ya kuitawala nchi ya Tanganyika.

M.M. Amir anayaeleza yale mambo yaliyotarajiwa kutoka kwa Uingereza baada ya kupatiwa huo wadhifa. Jambo ambalo M.M. Amir analiweka wazi ni kuwa nchi ya Tanganyika ilikuwa changa na iliyostahili kuongozwa hadi ifikie kiwango cha kuweza kujiongoza yenyewe :

Chukueni urubani
167 Muwarushe baharini
Waegesha ufukweni
Kwa kinyani na afia

Watanganyika walitakikana kupatiwa heshima zao. Haki zao zilitakikana kulindwa kwa kila hali. Kulingana na M.M. Amir Waingereza walitakikana kuwa wenye manufaa katika kila nyanja kwa Watanganyika. Lakini je ni yapi M.M. Amir anayotufunulia kuhusu Waingereza ? Kutokana na anayoyasema ni bayana kuwa ijapokuwa Waingereza walikubali hayo masharti na kuahidi kuyaheshimu, hayo siyo yaliyotokea :

Asemapo neno lake
Sili wache silinene
192 Na fikara zichemke
Haiwi kulifutia

Katika maswala waliyotakikana kusuluhisha ni vigumu kutokana na maoni ya M.M. Amir kupata waliyoyatimiza. Ilikuwa vigumu mtu kuwa na hakika ya kuwa alilotaka angetimiziwa :

Nenda rudi nenda rudi
Kwa viaga na ahadi
197 Na pengine isifidi
Haja kubarikia

198 Kila mkazi wa mbali
Hukonda kwa shtighali
Zikamwishia nauli
Na gome hajabandua

Na yote hayo si shei
199 Wala kwao si adui
Adui anayedai
Uhuru kuulumbia

Kwa hivyo Waingereza hawakuwa wakitimiza majukumu ya viongozi. Viongozi bora ni wale ambao wako tayari kuwatumikia watu wanaowatawala bila ngoa. Hapa tunaendelea kupatiwa picha inayodhihirisha kudharauliwa kwa Waafrika.

Waingereza kama wenzao Wajerumani, walitia bidii sana katika kutekeleza yale mambo ambayo yangewafaidi wao. Walielekeza wajibu wao katika mambo ya kiafya ili kuzuia magonjwa kama ya kuambukizana wakifahamu ya kuwa hayo yangeweza kumfika mja yeyote. Walijaribu kadiri walivyoweza kuimarisha barabara ili ziwafae katika shuguli zao za kiuchumi :

Lakini sipumbazike
Iko kiti ndani yake
219 Hutenda kwa tija zake
Si kuauni raia.

Katika kuonyesha dharau kwa Waafrika watu ambao waliwaona duni, Waingereza waliwafikiria wahindi kama wenzi wao. Hao walifikiriwa kuwa kufu yao. Chochote kilichokuwepo wao ndio waliofaidika.

Katika bunge lililoanzishwa mwaka wa 1920 Wahindi walipatiwa fursa ya kujiunga nalo ili kuwasilisha malalamiko yao kuanzia mwaka wa 1931. Ni miaka ishirini na tano baadaye ndipo walipomteua mbunge mmoja kuwawakilisha Waafrika. Mwaka wa 1958 wengine walichaguliwa wakawa wanane. Hii ilitokana na jitihada za Waafrika wengi na usaidizi kutoka kwa baraza la Mataifa, usaidizi wao katika kupigania haki za Watanganyika walio wengi. Hata hivyo M.M Amir anasema kuwa hao wajumbe walichaguliwa ili kuwapumbaza Waafrika, wafikirie ya kuwa pia na hao wanawakilishwa :

Hakika wajumbe hao
Wendapo kwenye kikao
291 Hawatoi ndimi zao
Lao ni kuitikia.
Jawabu kwao haliwi

292 Wala halikubaliwi
Kwa ukosevu wa Kawi
Mshabaha wa niabua

Jambo ambalo M.M. Amir amejaribu kutubainishia ni kule kunyimwa kwa Waafrika haki zao. Kama tulivyotaja hapo mbeleni ni kuwa Wakoloni wote waliwadunisha Waafrika na hawakuwapatia fursa katika kuamua mambo yaliyowahusu. Mwafrika hakuwa chochote mbele ya Mwarabu na Mzungu.

M.M. Amir kupitia huu utenzi amefupisha mateso na maonevu Watanganyika walishuhudia. Ni katika hali kama hizi ambamo Waafrika wengi walijitolea katika kupigania uhuru wa nchi zao. Hawangeweza kuvumilia zaidi ya hapo walipokuwa wamefika.

## 3:4:0 WAAFRIKA KATIKA SIASA .

Kutokana na mateso na maonevu Waafrika waliyoyapata kutoka kwa wakoloni, walikuja kutambua ya kuwa juhudi zao tu ndizo ambazo zingewakomboa.

Katika sehemu zilzotangulia tulishughulikia maswala ambayo yaliwaingiza Waafrika katika siasa nyakati za ukoloni. Tunaona jinsi Waafrika walivyopigana na kupinga ukoloni wa Waarabu. Kushindwa kwa Watanganyika katika vita vya kupigania uhuru kuliwafanya wafikirie upya jinsi ya kukabiliana na wakoloni.

Watanganyika walitambua umuhimu wa upangaji, umuhimu wa umoja na mbinu bora zaidi za kutumia katika mapambano yao. Nia yao ya

kwanza ilikuwa uhuru wao.

Katika enzi za ukoloni wa Waingereza, wenyeji waliamua kuunda chama ambacho kingetumiwa kutoa malalamiko yao. Chama cha kwanza kuundwa kilikuwa Tanganyika African Association (T.A.A). T.A.A. ilikusudia kupigania haki ili watu waepukane na shida :

Tuzipiganie haki
299 Tuepukane na dhiki
Vilivyo hatutosheki
Huenda tukapumua.

Chama cha T.A.A kilikuwa na makao yake Dar-es-Salaam. Ijapokuwa chama hiki kiliundwa ili kutetea haki za Waafrika, ukoloni uliendelea kuwepo.

R. Mwaruka (Ibid) anadai kuwa hiki chama kilikuwa na upungufu kwa kuwa hakikuweza kutimiza madhumuni ya siasa kikamilifu. Haya pia ndiyo yaliyowahi kusemwa na Julius Nyerere akikiunda chama cha TANU, 1954.

R. Mwaruka (Ibid : 27) anasema kuwa ni watu wachache ambao walijiunga na chama cha TAA. Anaendelea kusema kuwa hapakuwa na mvumo. Na wengi hawakujua.

Julius Nyerere alipojiunga na chama cha TAA 1953 baada ya muda mfupi aliomba wanachama wenzake wayachunguze upya madhumuni ya chama. Mnamo mwaka wa 1954 chama kilibadili jina na kuwa TANU

Kama tulivyotaja hapo mbeleni, ni mwaka wa 1945 ambapo Mwafrika wa kwanza aliteuliwa kwenye bunge na hiyo ilikuwa hatua nyingine mbele katika siasa ya Waafrika.

Kutokana na uongozi wa TANU kutaka usawa ambao ndio unohitajika katika jamii zetu, wanawake walianza kuhusishwa katika siasa. M.M. Amir anatuelezea haya kwa kutaja utenzi wa Bibi Titi Mohamed

Kwa hivyo Waafrika walipoanza kupinga ukoloni, kwao kuunda chama chao cha kwanza cha kisiasa na kwa mmoja wao kuteuliwa kujiunga na bunge kunachukuliwa kuwa hatua muhimu kwa wao kujiingiza katika siasa ya nchi yao.

## 3:5:0 MCHANGO WA NYERERE.

Katika kazi zote ambazo zimewahi kuishughulikia historia ya uhuru wa Tanganyika, JUlius Kambarage Nyerere hakukosa kutajwa. Mchango wa Julius Kambarage Nyerere umepewa sifa na kila yeyote ambaye amewahi kuandika historia ya Watanganyika.

M.M. Amir yaelekea amemlimbikizia sifa zote Nyerere. Sisi tutajaribu kuchunguza namna anavyomchora Nyerere. Je, M.M. Amir ni mmoja wa wale washairi ambao wanawatukuza tu viongozi kwa sababu wana huo wadhifa au ni kweli kuwa hawa viongozi wanazistahili hizo sifa ? Je, M.M. Amir kama tulivyotaja katika haipothesia yetu, ni mzalendo sana kiasi cha kumrundukia Nyerere sifa zote ? Umuhimu wa sehemu hii ni kuwa itajaribu kutubainishia haya.

M.H.Y Kaniki (1974:2) anasema ya kuwa mambo mawili yanaweza kusemwa kuhusu Nyerere. Kwanza, ukoloni ni kitu kilichokuwa cha kawaida ambacho kilimuunganisha Nyerere na Waafrika wenzake nchini Tanganyika, pamoja na waanzilishi wa chama cha TANU. Pili,

tajriba yake kama mwanafunzi hapa Afrika mashariki na Uingereza ndiyo iliyomdhihirishia yale maswala ya ukoloni yaliyohitaji uhakiki mkali. Waaidha, ni wakati uanafunzi wake ambapo alipevusha akili na mtizamo wake kuhusu siasa na vile vile namna ya kushughulikia mambo.

M.H.Y Kaniki (Ibid), R. Mwaruka (Ibid) pamoja na M.M. Amir wanasema ya kwamba ni kutokana na misingi kama hii ndipo Nyerere akaweza kugundua baada ya muda mfupi sana upungufu wa chama cha kwanza cha Watanganyika, T.A.A. Nyerere alisema kuwa msingi wa T.A.A haungeweza kuukabili vilivyo ukoloni wa Waingereza :

Alishikwa na jaabu
Na kuingia raghaba
386 Akanena sitoshiba
Ila moja tawambia

Siasa za chama hiki
387 Naona haziwafiki
Kisha zitaleta dhiki
Sisi na zetu dhuria

Ni wakati huu alipoomba jina la chama libadilishwe kuwa TANU. Baada ya hili kukubaliwa ni mwaka huo, 1954 Julai ambapo chama cha TANU kilizaliwa kwa msingi wa chama cha TAA. Jukumu la kwanza la chama cha TANU lilikuwa bayana, - uhuru wa Watanganyika.

Katika hizi jitihada M.M. Amir anasema :

Tumezikwa kaburini
Hali tuko duniani
395 Si unyonge kitu gani
Taka akawazibua

Tutakeni nchi yetu

396 Tuishi kama wenzetu
Tanganyika si ya mtu
Sikae tukale waa.

Tuudaini uhuru
397 Tutizame akhera

Na mengine teletele
Yatakuja pole pole
398 Bali shabaha ni ile
Uhuru kushikilia

Ili kuwa kiongozi atakayefaulu ni muhimu uheshimiwe na wale watu unaoongoza na Nyerere yaelekea aligundua umuhimu wa kufanya watu wawe na imani katika yale aliyokuwa akiwaambia .

Vile vile Nyerere alijichukulia jukumu la kuwaelemisha wananchi wa Tanganyika juu ya mambo muhimu ambayo yangewasaidia katika kupatikana kwa uhuru :

Mawazo tupeaneni
Kweli tuambianeni
421 Na hasada tuacheni
Masengenyano na ngoa

423 Mti mmoja uongo
Pekee pasi kiungo
Hausimamishi jengo
Jamaa na waapia.

Aliwasihi Watanganyika watambue ya kuwa walikuwa wakipigana na adui mmoja. Kwa hivyo kukawa na haja ya wao kuungana. Kutokana na umoja wao Nyerere hakuwa na shaka kuhusu ushindi wa chama pamoja na Watanganyika.

Alihimiza usawa miongoni mwa Watanganyika wote. Jambo ambalo baadaye tunamuona akiliendeleza na kulikuza kwenye Azimio la Arusha la mwaka wa 1967.

M.M. Amir anatuchorea kiongozi ambaye alikuwa ndio mfano unaostahili kuigwa katika maswala kama hayo yaliyowakumba Watanganyika. Amemchora kiongozi ambaye alihitaji kuungwa mkono na wananchi wenzake katika jitihada zake. Mwandishi anayefaulu katika kutumia nadharia ya uadilifu ni yule anayewatumia wahusika wake kama vyombo vya ushuhuda wa matendo mema. Vile vile huwafanya wahusika wake kama vielezo au mifano ya aina hizo za maisha na kwa kufanya hivyo, akatoa nafasi kwa msomaji wake kuielewa hulka ya binadamu na kwa kuielewa akapata nafasi ya kujielemisha ili apindue au arekebishe mwenendo wake.

M.M. Amir anajaribu kumsifia Nyerere kote kote. Anasema kuwa tangu mwanzo alijihusisha na siasa nyumbani na ng'ambo. Nyerere akiwa Tanganyika alishughulikia na kuwaunganisha Watanganyika na kuwatabiria ya mbele. Alilalamikia hali mbaya ya Watanganyika hasa kuhusu maswala kama ya ushuru, kutwaliwa kwa ardhi yao, kuhusu ujinga na ufukara ambao ulikuwa umesakini nchi yote.

Huko Ulaya kwenye baraza la Udhamini M.M. Amir anatuonyesha jinsi Nyerere alifika huko na kusisitiza dai lao la uhuru. Hakuwa tayari kukata tamaa. Kwa maoni yetu M.M. Amir amemsawiri Nyerere kama kiongozi aliyeweza kuwatabiria Watanganyika mambo ya baadaye na kuwahimiza wawe tayari kila mara kupigania uhuru wao. Aliwakumbusha umuhimu wa kujiunga na chama cha TANU katika kuleta umoja ambao ungekuwa kifaa muhimu dhidi ya ukoloni.

Mbali na safari za ndani alisafiri kwenda nchi kama Ujerumani

, Uingereza, Marekani ambako alipata misaada ya kuyainua maisha ya Watanganyika.

Kwa hivyo, hata ijapokuwa M.M. Amir hatuonyeshi ubaya wowote wa Nyerere tunakisia ya kuwa ikiwa ulikuwepo basi ulizidiwa na uzuri wake. Na hii hoja inapata uzito kutokana na mawazo ya A.N. Shija (1971 :4) anaposema ya kuwa ni vigumu kumpata binadamu al-iye na wasifu usio na dosari, au kumuona aliye na hulka isiyo na tone la wema. Maisha ya binadamu ni mchanganyiko wa hali hizi mbili naye hujulikana zaidi kwa ile hali iliyoizidi nyenzake. Ikiwa uovu umezidi wema, basi mtu huyo hujulikana kwa sifa ya uovu na ikiwa wema ndio uliozidi uovu, basi atajulikana kwa wema.

Kwa hivyo M.M. Amir ametupatia kiongozi aliyekuwa tayari kuw-apatia wananchi wake maadili ya kufuata. Hakukusudia kutumia nguvu katika mbinu zake. Alikuwa tayari kwa mijadala ambayo inge-wakomboa Watanganyika.

Ijapokuwa sehemu kubwa ya <u>utenzi wa uhuru wa Tanganyika</u> (Ib-id) imemrundukia Nyerere sifa nzuri maoni ya M.M. Mulokozi (1975) ni muhimu kufikiriwa. Anasema kuwa :

> Na imani yao mpya katika siku za usoni
> mapenzi yao kwa nchi zao na sifa zao
> kwa mashujaa wao, washairi wa kiswahili
> wa Afrika mashariki walijikita katika
> kuhakiki hali iliyokuweko kidhahania.
> waliishangilia hali iliyokuweko kwa nguvu
> jinsi walivyokuwa wakiushambulia ukoloni. 2

Anaendelea kusema kuwa hii sherehe haikudumu kwa maana baadhi ya hao washairi walianza kugundua ya kuwa uhuru haukuwa " lele-

mama ". Walitambua baadaye kuwa uhuru ulimaanisha kazi, kujitolea na kuwa tayari kuijenga na kuilinda nchi yao.

A.G. Gibbe (1978:10) anamuunga mkono M.M. Mulokozi kuhusu huku kushangilia viongozi bila kutua na kufikiria.

Kwa maoni yetu tunaonelea ya kwamba M.M. Amir amemsifu sana Nyerere. Ni kweli kuwa nafasi ya Nyerere katika kupigania uhuru wa Tanganyika ilikuwa kubwa. Hata hivyo ingelikuwa bora zaidi kama angechukua fursa hiyo pia kulaumu baadhi ya viongozi kuhusu feli zao maanake si kweli kuwa Nyerere na wenzake walikuwa kamilifu tangu mwanzo hadi mwisho

Vile vile inashangaza namna M.M. Amir anavyoandikia kuhusu Macloud, waziri wa makoloni. Picha inayotujia ni ya shujaa na ilhali inafahamika wazi kuwa wazungu (wakoloni) walikuwa kitu kimoja tu. Wakoloni ijapokuwa wakati fulani wangesema maneno matamu, walijawa na hila na mauti myoyoni mwao. Kwao Mwafrika alibaki mshenzi tu.

Wakanena jimbi letu
Watupu hatune kitu
1147 Lakini zawadi yetu
Ni hii koja pokea

Ya pili hii chuchuli
1148 Katika wetu uhai
Mila yetu ya asili
Leo twakutambikia

1149 Hatupakani masizi
Alama kuu ya enzi
Pamoja na ya mapenzi
Hukosi wavitambua

Iko deni watudai
1150 Katika watu uhai
Malipo hatuyajui
Ajuaye ni jalali

Ndio, wakati unapokipata ulichokuwa ukitaka furaha hukuingia. Lakini ni vigumu kuamini kuwa M.M.Amir kama mshairi anayestahili kuonyesha maovu yote ya wakoloni kusahau mara moja jukumu lake na

kutusawiria hali inayoelekea kuonyesha kuwa Watanganyika walikuwa wakifurahia kutawaliwa kwao.

Yaelekea kuwa M.M. Amir alidhihirisha uzalendo wake kufikia kiasi cha kutoweza kufikiria hali halisi ya baadaye ya Waafrika wao wenyewe wakijitawala. Hata hivyo ieleweke kuwa Nyerere Mwenyewe alikuwa kiongozi aliyeweza kutazama mbele na kutambua mawingu yaliyokuwa yametanda ikiwa Watanganyika hawangejitolea na ndio sababu katika Azimio la Arusha tunamuona akihimiza dhana ya uhuru na kazi.

Ni kutokana na uongozi wake ndipo Tanganyika ikapata uhuru mnamo maka wa 1961.

1531 Leo mwisho wa utesi
Kati ya nyinyi na sisi
Uhuru wenu pokea

## 3:6:0 PINGAMIZI KWA WAPIGANIAJI UHURU.

Hakuna mahali katika bara la Afrika ambapo uhuru ulipatikana kwa urahisi. Vizuizi mbali mbali viliambatanishwa na kupatikana kwa uhuru katika nchi nyingi za Afrika.Vita na hatua kabambe ilibidi zichukuliwe ndipo uhuru ukapatikana. Damu nyingi ilimwagwa na shida nyingi zikawa ndiyo hali ya kawaida. Nchini Tanganyika, wengi waliokuwa wakipigania uhuru walipata pingamizi kutoka sehemu mbali mbali.

Chini ya Waarabu, Waafrika walinyanyaswa na kunyimwa haki zao Waliodhubutu kutetea haki zao waliteswa na mara nyingine kuuawa. Hapa tunamaanisha hata na wale waliotaka kujikomboa kutokana na utumwa uliofanywa kwa kiasi kikubwa na Waarabu.

M.M. Amir akishughulikia ujaji wa Waarabu anasema :

Kulijaa Tahamaki
97 Ya vigumba na mikuki
Wanyonge wakahiliki
Kama matone ya mvua

Alidumisha hekima
98 Kula na watu wazima
Wajumbe na maulana
Kusudi apate njia

Kuwadhulumu viumbe
103 Kwa biashara ya pembe
Alifanya ndio jembe
Nchini akaliuna

Anaendelea kusema kuwa :

Kwa kuwa tokea jadi
Mwarabu alifaidi
125 Alifanya jitihada
Wenziwe kuwaondoa

126 Moyoni kalia wivu
Akaleta ushupane
Akawaonyesha mbavu
Ushinde akautwaa.

Kutokana na tamaa na wivu wake haimkiniki Mwarabu angempatia Mwafrika fursa ya kujikomboa.

Wareno waliwatawala wenyeji na kuwafanyisha kazi wenyeji mwa-mbao katika hali mbovu na bila malipo. Hawakupatiwa fursa ya ku-jikomboa.

Wajerumani ndio ambao walitatiza jitihada za wenyeji za kujikomboa. Wengi wa viongozi waliojitolea waliuawa. Bushiri alipiganao lakini mwishowe aliuawa. Katika vita vya Maji Maji watu wengi walikufa hata Kinjeketile mwenyewe.

Chini ya utawala wa Waingereza, Watanganyika hawakupatiwa fursa ya kujitetea hata bungeni hadi baadaye.

Katika usajilishaji wa vyama vya kisiasa wanasiasa walipata shida. Ilichukua muda mrefu kwa Waingereza kuyakubali matawi ya chama cha TANU kusajiliwa.

Kuna sheria ambazo ziliundwa kama anavyosema M.M. Amir ili kutatanisha jitihada za wanasiasa mathalan baada ya chama cha TAA kuundwa Waingereza walitambua kuwa watu walikuwa wameanza kujishughulisha na siasa sana.

Mngere alipoona
Bamtu wamekazana
319 Jicho wakafumbiana
Kanuni kuzitangua

320 Kaunda mpya kanuni
Wale wa serikalini
Watatiwa hatiani
Siasani wakiingia

321 Inda ikapata kasi
Kama palipo utesi
Pakamwagwa majasusi
Kwa kuonyeshwa takua

325 Palijiri takilifu
Iliyoletwa na hofu
Hatima ikasadifu
Viongozi kulegea

Sheria zingine zilitolewa na serikali kama Moshi ambako kulitolewa amri ya kutopatikana watu zaidi ya kumi wakikutana:

Ilikuwa nchini
648 Watu kumi si kanuni
Kukutana hadharani
Bila ruhusa kupewa

Serikali ya Waingereza ilitisha kuwaachisha kazi Watemi, Majumbe na Maliwali ikiwa watoto wao wangejihusiha na siasa. Hii inasikitisha na katika baadhi ya serikali za kiafrika viongozi wameziiga hizi mbinu za wakoloni dhidi ya wenzao; jambo hili ni kinyume cha maadili ya jamii zetu.

## 3:7:0 UPUNGUFU WA WATANGANYIKA .

Kama inavyofahamika hakuna binadamu aliye kamilifu. Mara nyingi katika maswala yanayowahusu wanadamu huwa kuna chembe chembe za upungufu ambazo lazima zishughulikiwe kikamilifu ndipo hatua za kimaendeleo ziweze kufikiwa. Si lazima matakwa ya wananchi wa taifa moja kuwa mamoja.

Tulitaja katika sehemu zilizotanguliam ya kwamba Waingereza walihofu sana ile siasa iliyokuwa ikizuka miongoni mwa Watanganyika hususan wale ambao walikuwa wamekipata kisomo cha mkoloni. Walianza kukitumia hicho chombo walichopewa na mkoloni dhidi yake Kwa hivyo Waingereza walipogundua ya kwamba mambo hayakuwa yakienda namna walivyopenda, walianza kutafuta kila mbinu ambayo ingewaharibia Watanganyika mipango yao. Katika kufanya hivi walianza kuwatumia baadhi ya Waafrika ambao walikuwa radhi kuuza haki zao kwa ajili ya wazungu. Kulizuka vibaraka wa serikali ya kikoloni pamoja na majajusi ambao walipata habari kutoka kwa viongozi wa

Waafrika na kuwapelekea Waingereza.

Huku kusaliti viongozi wa Kiafrika na wale Watanganyika waliokuwa wameuuza uraia na uzalendo wao kuliwasababishia Watanganyika matatizo makubwa sana. Wengi wa hawa wasaliti walipatikana katika chama cha United Tanganyika Party (U.T.P).

Jambo ambalo M.M. Amir hatuonyeshi hapa kwa wazi ni huu upungufu. Analotaka tu kutuonyesha ni namna ambavyo TANU ilivishinda hivyo vyama vingine vya kisiasa kama vile U.T.P, Kongoresi- chama cha weusi na A.M.N.U.T.

M.M. Amir anapozungumzia juu ya hali ilivyokuwa Tanganyika wakati wa sheria katili za kikoloni picha tunayopata ni ya woga miongoni mwa Watanganyika :

324 Palijiri taklifu
Iliyoletwa na hofu
Hatima ikasadifu
Viongozi kulegea

Walikwepa ajali
328 Kwenda dunia ya pili
Kwenye malazi thakili
Na posho la kubakia

Wengine wao walihofu kupoteza kazi zao kama anvyoendelea kusimulia :

Baadhi walifikiri
Wao ni wahifakiri
Wasipotii amri
Kazi zitawapotea

Inaeleweka kuwa katika hali kama hii watu huhofia maisha yao na kazi zao ambazo huwapatia cha kutegemea.

Baadhi ya Watanganyika yaelekea hawakuwa na imani katika viongozi wa Kiafrika. Hawakuamini ya kuwa Waafrika wangeweza kutaw-

ala katika njia inayofaa. Hali ya sasa katika nchi nyingi za Kiafrika inatupa sababu nzuri ya kufikiri hao kuwa waliouona upungufu wa viongozi walijua walichokuwa wakisema. Hata hivyo wakati huo jambo lilokuwa muhimu lilikuwa ni uhuru wa Watanganyika :

Wakaropoko suali
Tutabirieni hali
802 Nyakati za serikali
Yenu vipi itakua.

Baadhi ya watu kama anavyotuambia M.M.Amir yaonekana hawakuwa na uvumilivu. Walitaka mambo yafanyike kwa haraka. M.M. Amir anaonyesha hata hivyo ya kwamba binadamu hawalingani tabia :

Wakihimiza kwa nini
Matokeo hatuoni
916 Hii serikali gani
Kwayo hatuna tamaa

Hali kama hii ilileta wasiwasi na ilihitaji tu viongozi ambao wangewaelemisha wananchi wao. Hapa tunamuona M.M. Amir akimuonyesha Nyerere kama kiongozi aliyechukua hatua zinazostahili katika kuwahimiza wananchi juu ya umuhimu wa subira.

## 3:8:0 HITIMISHO .

Utenzi wa uhuru wa Tanganyika umetuonyesha mateso na jitihada ambazo ilibidi Watanganyika wachukue ndipo uhuru wao kupatikana.Wengi wa Watanganyika waliyapoteza maisha yao na kwa jumla maisha yalikuwa magumu kwa Watanganyika wengi.

M.M. Amir alielekea kurekodi hali ilivyokuwa tangu nyakati za wakoloni wa jadi hadi kufikia nyakati za Waingereza ambapo Tanganyika ilijipatia uhuru wake 1961.

Jambo ambalo limejitokeza wazi wazi ni uzalendo alioudhihirisha M.M. Amir na kutokana na huu uzalendo sehemu kubwa ya utenzi huu imetengewa Rais wa kwanza wa nchi ya Tanganyika Julius Kambarage Nyerere na chama cha TANU. M.M. Amir ameonyesha hatua mbali mbali ambazo Nyerere alichukua katika kuwaongoza na kuwaelekeza Watanganyika katika vita vyao vya ukombozi dhidi ya wakoloni.

Tumeonelea ya kuwa ijapokuwa mengi ya yale ambayo M.M. Amir amesawiri hayakukinzana na historia, mwandishi ameelekea kusimulia zaidi sifa za Nyerere na chama cha TANU bila ya kutua na kudadisi bila ubinafsi wowote hali halisi ya maana ya uhuru.

TANBIHI :

1. Tazama R. Mwaruka, 1968
2. " Mulokozi, 1975.

## SURA YA NNE

### 4:1:0 UTANGULIZI .

Kutokana na uchunguzi wetu tumeweza kugundua muoano mkubwa kati ya maudhui yaliyomo katika diwani ya Tungo Zangu (1977a) na Malenga wa Mrima (1977b). Kuanzia sasa tutakapokuwa tukiirejelea diwani ya Tungo Zangu (Ibid) tutaitambulisha kwa (1977a) na diwani ya Malenga wa Mrima itajitokeza kama (1977b).

Huu muonano wa maudhui umetulazimu kuzishughulikia hizi diwani mbili kwa pamoja.

Diwani zote mbili zinagusia masuala muhimu katika jamii. Kwa hivyo tutajaribu kadiri tutakavyowez a kuyaangazia haya masiala ambayo M.M. Amir ameandika kwa matilaba ya kuiboresha jamii yake. Sehemu ambazo zimechambuliwa na kama vile Unyumba, Malezi, siasa na Uzalendo, Maajaliwa na jukumu la mwanasanaa katika kuielemisha jamii.

### 4:2:0 UNYONGE .

Katika diwani zote mbili M.M. Amir amejaribu kuonyesha hali ya unyonge ambayo inadhihirika wazi wazi katika jamii zetu. Swala la unyonge ni kitu kilicho dhahiri sana kwa watu wengi wa Tanzania na Afrika kwa jumla. Wengi wa watu ambao wanapatikana katika ulimwengu wa tatu ni wale ambao huishi kwa taabu. Kazi wazifanyazo ni za kisulubu na mapato yao mara nyingi huwa duni.

Itafahamika ya kwamba wengi wa washairi wetu ni watu waliokulia katika maisha ya dhiki ya wakulima. Mazingira yao kama anavyodokeza I.S.Y Sengo (1987 ) yaliweza kuwapa tajriba pevu ya kufahamu matatizo mengi yanayowakumba wanajamii wenzao. Jambo la kusikitisha kama tutakavyoonyesha baadaye ni kuwa matatizo mengi yanasababishwa na baadhi ya wanajamii ambao ni walafi na hawana maadili yanayopendekezwa katika jamii.

J. Adeola (1975:150) anafikiria ya kuwa si haki kwa wataalam wa Kiafrika kusahau ya kuwa watu wa Afrika ndio ambao wamedhulumiwa sana. Na huu ukweli unapasa kuwafanya waandishi wa kiafrika na wahakiki kujihusisha kikamilifu na swala la hali duni ya Waafrika . **( Tafsiri na msisitizo wetu )**

Nchi zetu zinapokuwa katika hali mbaya ya kiuchumi na kiufundi tunaona hali ya unyonge ikijitokeza. Mataifa mengi ya kiafrika huanza kuombaomba kutoka nje na hii inayafanya yategemee kwa kiasi kikubwa mataifa yaliyoendelea kwa misaada. Nchi ya Kenya imekumbwa na hali hii na inatokana na viongozi ambao hawakujali hatima ya nchi yao. Walizigeuka kaida za uongozi na kujiingiza katika mambo ya ufisadi. Katika (1977b:16) M.M. Amir anaonya kuwa nchi iombayo, "daima hukaa chini, maganja ya mpewaji". Hapa tunaonyeshwa ile hali ya unyonge mataifa yetu mengi yanapitia. Kwa kuwategemea wafadhili ambao wagomapo ni watu maskini wanaoteseka zaidi.

Katika kiwango cha kitaifa tunawaona viongozi ambao huwanyanyasa wananchi wenzao wakiwa na cheo. Wanyanyasi ndio wachache

ambao huhodhi mali yote na aghalabu kupitia njia zisizo za kiadilifu. Kama tulivyotaja ufisadi umesheheni katika jamii ambayo ina viongozi wasiofuata maadili.

Katika <u>Malenga wa Mrima</u> (uk.40) M.M. Amir anaonyesha jinsi wenye mamlaka huzivunjilia mbali sheria na haki za raia. Wanyonge huwa hawana la kusema mbele ya wadhalimu wao.

Anawauliza hivi :

Huwaje mkadharau, vilemba juu ya tosi
Wengine mkasahau, wenyewe mkajitusi
Uzima hawishi kiu, inamisheni vikosi
Dhamana mwendo wa ngisi, unyonge hauna mwisho

Anaendele kutuhadharisha kwa kutoa rai kuwa :

Ucheni Unyonge `ngawaje hautikisi
Ni mwingi madongedonge, tunao katika sisi
Mamlaka ni vilinge, hayajilisi

A. Mazrui akionyesha kuguswa kwake anasema :

Enyi wadudu mlo mbaoni
Mloungana kwa udugu wa imani
Nyingi mkusanyapo yenu riziki
<u>Sisi twasongeka kwa kazi na dhiki</u>
Na mfuatapo jaala yenu bariki
<u>Sisi twachamka kwa wingi wa chuki</u>
(Msisitizo wetu)

Haya yote yanaonyesha ya kwamba viongozi ambao hawana moyo wa udugu na ushirikiano na raia ndio wanaowaletea wenzao uchungu na dhiki maishani na kuwafanya wawe wanyonge.

Tunaweza vile vile kuupata unyonge katika familia. Hapa kuna unyonge wa mwanamke kutokana na mateso ayapatayo kutoka kwa mume wake. Waaidha kuna watoto wanaoteswa na mama zao wa kambo. Watoto

wasiolelewa na mama mzazi huteswa na kuchukuliwa kuwa watumwa.

Utenzi wa mama wa kambo kutoka ukurasa wa 63 hadi 82 katika (1977a) unaonyesha dhuluma afanyiwayo mtoto na mama wake wa kambo Mtoto ananyimwa chakula, mapenzi na afanyiwalo ni kulimbikiziwa tu kazi. Ukosefu wa mama mzazi ndio unaosababisha haya yote. Kutotajiwa kwa baba mzazi katika kujaribu kuyachunguza maslahi ya mtoto wake kunaonyesha namna mshairi anavyowasawiri baadhi ya wazazi wanaolisahau jukumu lao la ulezi.

Huu utenzi unaonyesha jinsi mama wa kambo anavyomdhalilisha mtoto wa mwenzake :

Na penginepo anyimwe
Asimuonyeshe kamwe
Alipo asukumwe
Na mate kumtemea

Fikiri maovu gani haya
Yanavyokata maini
Lao waona machoni
Huwezi kuvumilia

Dondoo hili laonyesha jinsi watoto wanavyoteseka kutokana na mama ambao wana chuki na ambao hawana maadili kwani ni dhahiri ya kuwa mama mwenye mapenzi hawezi kumtendea haya mtoto.

Hali hii ya unyonge huwafanya baadhi ya wanajamii kuikubali hali yao. Yaelekea mshairi anauangalia unyonge katika mkabala wa majaaliwa.

Katika (1977a:13) anasema :

Miuja ya ulimwengu aliyoumba karima

Ni mafungu kwa mafungu ni wapi ilipokoma?
kama sisi kwako ni kwangu hufyonsa damu ya nyama
Ni kama huu unyonge, si senene kitugani?

Katika hili shairi mbali na kutufanya tuamini ya kuwa unyonge unatokana na takidiri,mshairi anatuonyesha vile vile mahala ambapo hudhihiri. Aneleza namna mtu anavyojikuta mnyonge kwa kukosa kile akitamanicho kwa moyo wake wote lakini akakikosa na matokeo yake huwa kukondeana na moyo kumwangama.

Kifo kinapotokea huwa pia kinaleta unyonge kwa yule anayebaki na baadhi ya jamii yake :

Ujane naashiria, dalilize na alama
Upunguzavyo dunia na kuzidisha tuhuma
Huu ni unyonge pia,suraye haikutama
Kama si baba na mama wadhani vingekuwaje!
(Msisitizo wetu).

Ni unyonge vile vile kuzaliwa pweke maanake hata ikiwa wazazi wako wanakupa mapenzi bado utataka kuwa na yule utakayemwita dadako au kakako. Ni kweli kuwa watu huutafuta uzazi hapa duniani kama almasi kwani kila mara kuna ile haja ya kuwa na undugu na ushirika wa kijamii. Kitu muhimu duniani ni kuwa na wenzako ambao wakati wa shida na raha watakuwepo kushiriki nawe kikamilifu.

Katika shairi la "Mlijuu" (1977a:19) mshairi anatuonyesha kuwa hao watu wanaonyanyaswa ndio hasa nguvu za wale wanaowatesa hasa katika utawala.

" Nguvu zote ni chini, na mizi kila mahali."

Ni bahati mbaya kuwa wale wanaotaabika ndio huwachagua viongozi na husahaulika baada ya muda mfupi. Viongozi katika

jamii zetu wana ubinafsi unaowafanya wajitakie tu makuu na kuzisahau mbeko za uongozi bora.

T.A. Mvungi, kuhusu unyonge unaoletwa na utawala anasema :

> Mtu kiteni kakaa, watu wamekalisha
> Leo anatuambia, tena atuabudisha
> Lakini mpanda ngazi bila shaka atashuka.3

T.A. Mvungi (9188:23) anashtakia hali ilivyo na viongozi Afrika kwa jumla anapodai ya kuwa iliyo wazi kuhusu uongozi wa Afrika ni utumwa. Hii inathibitisha madai kuwa Waafrika wamewafanya Waafrika wenzao kuwa watumwa na wanyonge na kwa hivyo hakuna tofauti kubwa baina ya viongozi wa Waafrika wengi na wakoloni.

Katika "Buibui" (1977b:75) M.M. Amir anautaja unyonge utokanao na kutokuwa na uhuru wa kujitetea katika hali ambazo wenye mamlaka hawafuati sheria maalum. KUna adhabu zitolewazo kwa watu na ambazo katika hali ya kawaida zisingeruhusiwa kutokea. Tunawaona viongozi ambao wanawategemea vibaraka ambao watabuni mbinu za kuwatia raia wenzao taabani ili waupate mradi wao. Anasema :

" Unyonge wa kila nia, vikuku umetuvika "

Analiendeleza swala la unyonge jinsi linavyoletwa na viongozi katika " Mboni " uk.69. Hapa anawataja viongozi ambao huwasahau raia walio mbali nao na kuwasaidia tu wale wanaosabihiana na ilhali wote wamekuwa wakipigania uhuru. Tunaipata hali kama hii katika "Kimbunga " uk. 87.

Kwa jumla mshairi anaonyesha kuwa unyonge upo katika nyanja zote za maisha. Kiasi kikubwa cha mashairi tuliyoyapitia yanaon-

yesha ya kuwa ni binadamu wanaowaletea wenzao unyonge na hii kwa sababu hawana maadili yanayohitajika katika jamii. Hawana ule moyo wa udugu ambao Tolstoy anasisitiza.

Ijapokuwa wakati mwengine mshairi anaelekea kuonyesha kuwa unyonge unaweza kumpata mja yeyote hii haimaanishi ya kuwa Mungu ndiye amependa watu wawanyanyase wenzao. Jambo muhimu ni kwa wanadamu kuishi kwa kuyafuata maadili ambayo yatawaletea ushirika katika jamii. Ile jamii ambayo ina watu wanaoelemishana mara nyingi wanajamii wake huishi kwa furaha.

Mashairi mengine yanayozungumzia unyonge ni pamoja na " Mwambaje", "Kutindikiwa" katika (1977b) na katika (1977a) baadhi ya mashairi ni kama vile " Ndiyo na siyo" uk.43, "Hawaa" uk.48.

## 4:3:0 UADILIFU .

Mashairi mengi katika diwani mbili tunazozitalii yanagusia swala la uadilifu kwa namna moja au nyingine. Mshairi amekusudia kuwaongoza wanajamii katika kuwatendea wenzao mema.

G.B. Mungania (1985:35) akiyashughulikia mashairi ya M.E. Mnyampala anasema :

> Maadili ni mafundisho yatolewayo
> kwa njia ya ushairi na ambayo
> huongoza kwenye haki.
> Hakuna jambo lililo baya zaidi
> liwezalo kuikumba jamii kuliko
> kule kupotea kwa utu wake. Msanii
> ana wajibu wa kuhakikisha ya kwamba
> jamii yake inajihifadhia au kujiregeshea
> heshima yake iliyopotea.4

Tunalofahamu ni kwamba M.M. Amir anaiandikia jamii inayoshuhudia maovu kwani hakuna kiumbe aliye kamilifu. Kwa hivyo hii inampatia fursa nzuri ya kuchagua jambo ambalo kwalo atalichezea vizuri maanake anayo data tayari. Anayoyafanya M.M. Amir yanapiga mwengo yale C. Achebe ayasemayo kuhusu jukumu la mwanasanaa. Msanii yuapaswa kuwa mwalimu wa jamii yake katika maswala muhimu ya kiuadilifu.

D. Daches (1981) akizungumzia juu ya P. Sidney anasema kwamba Sidney (Ibid) ni mmoja wa wahakiki waliowaona washairi kuwa watu walioandika mshairi wao kiuadili. Washairi wanatazamwa kama waundaji wa dunia ambayo inawaongoza wale waifuatayo kukubali maadili na kukataa matendo mabaya. Kwa hivyo yeye, kama anavyosema G. Hough, ni kwamba ushairi kupitia ushairi wake anatupa fursa kutokana na yale ayaandikayo kufuata (kuchagua) nyendo nzuri na kuacha mbovu.

Kwenye shairi la "Mbeko" (1977a:3) M.M. Amir anazungumzia swala la mbeko na anazizungumzia mbeko zinazopaswa kuigwa na anashangaa ni kwa nini wanadamu hawazifuati. Mshairi anataja nia yake ya kutaka wanajamii kufahamishana kuhusu hii dhana ya mbeko ili ifahamike barabara kwa kila yeyote anayehusika. Inatujuzu hapa kufahamu umuhimu wa kuwaelemisha wanajamii juu ya jambo lolote ambalo wanatarajiwa kutimiza. Itakuwa si haki kuwalaumu watu kwa jambo ambalo hawalifahamu. Anasema :

Twambizaneni kwa dhati, maana ya hii mbeko
Ilivyo mwanzo na kati, na mwisho huko iliko

Suraye tuzatiti, pasiwe na hangaiko
Ujana kuwekwa mbeko, huwaje mkaghuniwa.

Katika hili shairi tunaona jinsi mshairi anavyolalamika juu ya wanadamu walafi ambao hawawajali wenzao hata wanapowaona taabani :

Mwafukia mashimoni, pesa mifuko mifuko
Shukuki yenu mwakari palipo na maanguko

Anatoa rai hata hivyo kwamba :

Kwa kila mpa dunia, Kwa utu mwema na cheko
Sambe hukosa fidia siku za joto na mwako
Msi haya kutambua, apeleze kuzamako
Matendo kuwekwa mbeko, huwaje mkaghuniwa?

Inakuwa muhimu kutokana na hili shairi kwa waja kutilia maanani mbeko katika matendo yao waishipo humu duniani kwani wana lao fundo kwa mema watakayowatendea wenzao.

Matendo ya binadamu yanapaswa kuwa ya kimaadili kwani jinsi matendo yetu yalivyo ndivyo maisha yatakvyokuwa. M.M. Amir anajaribu kuhimiza maisha mazuri kwa wanadamu wote. Maudhui yapatikanayo katika " Maisha na Matendo" (1977b:2-3) yanalingana na yale ya "Msi kusana moyewe" (1977a:10-11) ambayo yanaonyesha jinsi matendo ya watu huyafanya maisha yao kuwa ya matatizo au ya furaha.

Shairi la "Shani ya mwadilifu" (1977a:47) linazungumuzia sifa za mtu mwadilifu. M.M Amir anasema kuwa mwadilifu huwa ana moyo mkunjufu na hujiepusha na mabaya kwan i yuapaswa kuishi maisha mema :

Mtu kisha makini, daima ni mwangalifu
Kasoro penye machafu, hugwaza akapotea

M.M. Amir anatofautisha mwadilifu na yule mzazi tumpatayo katika " Utenzi wa mama wa kambo" uk. 63-82 kwa kusema kuwa:

Hulea wake mtoto, si mchusa si mchofu
Kwa karadha, na mapito, hangofi kamwe halafu
Ndiye maji zimia moto, kiamboni twamsifu.

Maudhui yaliyomo katika " Shani mwadilifu " yanaonana na yale ya shairi la " Utii " (1977b:22) ambapo mwandishi anazionyesha sifa za raia mwema. Katika "utii" anasema :

Raia mwema ni yule aliyejaa utii
Si ubishi na kelele, akanywalo hasikii
Raia asiyetii ni fisadi wa nchiye

M.M. Amir anaonyesha ya kuwa wale raia ambao hawazitii sheria za nchi pamoja na viongozi huwa ni fisadi kubwa wa nchi maanake hawa ni watu ambao huleta hali ya wasiwasi kwa wananchi wenzao. Kututii kwa sheria hudhihirika kupitia kwa wizi na aina nyingine ya uhalifu. Kwenye "Shani la mwadilifu" anasema ya kuwa ` Hanazo mbovu alama, za shari na uumbufu. Yeye huziandama sheria na huwa kwenye mstari wa mbele'.

Sifa ambazo mshairi anampatia Nyerere ni za kiadilifu na anakuwa mfano mzuri kwa jamii yake. Nyerere anasawiriwa kama kiongozi ambaye hana tamaa za kidunia na kila alitendalo huwa amelipima kwa namna iliyo ya busara sana. Ni kiongozi ambaye huwaonya wananchi wake juu ya mabaya yanayoweza kuwafika wasipofuata sheria kwa hivyo akawaongoza namna ipasavyo.

Tunaweza kwa hivyo kumtofautisha Julius Nyerere na viongozi au watu walioko mamlakani na ambao hawana busara kama yake. Hawa wanasawiriwa katika " Mamlaka" (1977b:39) ambapo mshairi anatupatia mfano wa wale wanaowadhulumu wenzao :

> Mwasusuma mamlaka, kwa kishoto na wepesi
> Zimewajaa hamka, mwendapo hamwishi kasi

Na baada ya kuonyesha tabia zao mbaya anawaonya ya kuwa washikapo madaraka wasione hapo basi wakaanza kupuruka kwa mbawa zao na mikusi. Katika shairi la " Ndwele ya kujipa " (1977b:45) mshairi anatusawiria mfano wa viongozi wasio waadilifu. Mfano ni ule unatolewa katika " Buibui" (1977b:75) ambapo mshairi anamzungumzia mfalme ambaye hakufuata mbeko za uongozi katika kutoa adhabu yake ila yeye alichukua hatua zake kutokana na yale aliyokuwa akiyasikia tu kwa watu. Mshairi anasema kuwa huyu alikuwa kiongozi ambaye popote aambiwapo neno husadiki na hukumu ikafuata nyuma. Viongozi wa sampli hii huwa wanawaadhibu wananchi ambao hawana hatia yoyote kwani hawafuati sheria ambazo ndizo zinazopaswa kuwaongoza.

Kwa kuyaendeleza maadili ambayo yanapaswa kuwa yakiwaongoza wanajamii lakini ambayo hayapo, mshairi anatuchorea picha inayoonyesha watu wakinyimwa haki zao. Katika shairi la " Shoto " (1977a:4) anasema :

> Nakupa uzito wangu, wauchukua kwa shoto.

Hii inatoa imani ambayo raia huwa nayo katika viongozi wao. Wale ambao wanapaswa kuzuia rushwa wanashindwa kutimiza jukumu

lao. Ajabu ni kuwa katika jamii nyingi hao wanaozitoa hotuba za kuwakataza raia kushiriki katika rushwa ndio wanaokuwa katika mstari wa mbele kwa mambo kama hayo. Kwa kiasi kikubwa mshairi analalamikia juu ya hali ambayo imekuwa mazoea kwa wanajamii kutoa rushwa ili watimiziwe miradi yao na vile vile wale wanaopaswa kuwafanyia wananchi kazi wanategemea kupata 'kitu kidogo' kwanza Hii ni hali mbaya katika jamii maanake wale ambao hawana 'kitu kidogo' hawawezi kupata haki yao.

Shairi la " Vua mazuri " (1977a:14) M.M. Amir anashauri juu ya kuvua mazuri. Wanajamii wanapaswa kuvua maneno ya chuki ili yasaliayo yawe mazuri :

> Yachuje yako maneno usijifanye ni siki
> Au kama msumeno, Ukerezao visiki
> Ni fisadi ya mavuno ndugu na urafiki.

Lengo mojawapo muhimu la mbeko ni kuleta na kukuza udugu katika jamii lakini hapa tunaonyeshwa yale mambo ambayo yanaweza kutatiza udugu na ambayo hapana shaka mshairi anahimza yaachwe.

Katika shairi la " Nduma kuwili " (1977a:23) M.M. Amir anatoa mfano wa mja ambaye hana msimamo katika matendo yake. Kwa hivyo mshairi anatahadharisha dhidi ya kumfuata mtu kama huyu kwani hujivika pande mbili mtu wa sampli hii ni mnafiki. Ni wanadamu wanaotanda msimotandwa. Mshairi anakataa ya kuwa hata mtu wa aina hii angekuwa mwalimu yeye angetumia busara kumkataa. Waaidha hatima ya mtu kama huyo huwa ni matesoni.

Katika " Tuchimbeni Dafina " (1977a:29) Mshairi anaonyesha

namna baadhi ya watu ni popo wamezoea giza yaani wale watu waliozoea kufanya maovu. Lakini yeye kama muadilifu anakana :

Lakini sisi hatumo, fungo hilo twalikana
Giza kwetu ni mashimo ya watu kuzikiana

Anapozungumzia swala la heshima, M.M. Amir anatuonyesha ya kuwa hekima ni kipingee muhimu sana katika kutatua maswala muhimu katika jamii.

'Nchi iingiapo ndwele mazonge yakikithiripo palipokita ukata hekima ndicho kipawa cha faraja na fahari. Huwafaa wengi.'

Tumezitalii baadhi ya sifa za maisha ya kimaadili kwa mujibu wa M.M. Amir. Hata hivyo, inatujuzu kutaja kuwa binadamu ni kiumbe dhaifu na kwa hivyo inakuwa nadra kuwakuta wale wanaoishi maisha ayapendekezayo mwandishi bila kukeuka kaida. Ikumbukwe hata hivyo ya kuwa nia hatimaye ya kila msanii wa kimaadili ni kuiboresha jamii yake. Wanadamu watapaswa kila mara kufahamu umuhimu wa kuishi maisha ya kiuadilifu.

## 4:4:0 SIASA NA UZALENDO.

Diwani zote mbili zina mashairi yanayozungumzia siasa lakini inaonekana ya kuwa ni katika diwani ya Malenga wa mrima ambapo mna mashairi mengi yanayogusia swala la siasa na uzalendo sana. Kama itakavyodhihirika tunaona M.M. Amir anaisifia sana siasa ya ujamaa. Shairi la "Azimio la Arusha" linapatikana katika diwani zote; (1977a:40) na (1977b:14). Kama tulivyodokeza katika sura

ya tatu yaelekea mshairi mwenyewe alikuwa mfuasi wa viongozi wa Tanzania walioanzisha siasa ya ujamaa na kwa hivyo yeye akawa mmoja wa wale washairi wanaolaumiwa kuwa :

" Wanarudia kikasuku yale maneno
Yasemwayo na viongozi wa nchi
Majukwani,magazetini na kwenye
Vyombo vingine vya umma bila ya
Kuyacheua". 5

Shairi la "Azimio la Arusha" linalitazama Azimio la mwaka wa 1967 kuwa mkombozi wa Tanzania. Mshairi ni mmoja wa wale walioolitizama hili Azimio kuwa mkombozi wa Watanganyika kutoka kwa taabu zao zote. Matatizo ya nchi changa Afrika yalikuwa yameanza kuwadhihirikia raia na wao walifikiria ya kuwa dhana ya ushirika ambayo ilipendekezwa na Azimio ingeweza kuwaauni wananchi wote. Jambo ambalo wengi wa viongozi na wananchi walisahau kufahamu ni kuwa watu walitofautiana kimtizamo kuhusu hayo maswala. Dhana yenyewe ya ujamaa ilikuwa nzuri lakini watu walikuwa na ubinafsi mwingi na hawakuwa tayari kushirikiana katika kuleta maendeleo jinsi walivyotarajia.

Katika hili shairi, mshairi anapendekeza wananchi wayakubali yote viongozi wao wapitishayo "

'Kimbelembele waume pasiwe msema hasha'

Mawazo kama haya yana hatari zake. Katika hali za kisasa ambapo kuna uhuru mwingi wa kuzungumza si rahisi kwa umma kunyimwa hiyo haki ya kutoa maoni yao. Nchi ni yao na yote yaafikiwayo yawanahusu kwa kila namna na ikiwa watanyimwa haki hiyo huwa wanahisi ya kuwa viongozi wao ni wa kidikteta.

Mshairi anatalii maswala muhimu ambayo Azimio la Arusha lilihusisha. Watanzania walipaswa kuishi pamoja vijijini, mali ilipaswa kutaifishwa na watu walipaswa kushirikiana katika maendeleo. Wale ambao walikiuka haya walikuwa raia wasio watiifu. Anamalizia shairi kwa kusema :

Hili anayepuuza ni mche mui kotesha
Azimio la Arusha, lijile kutukomboa

Kama tulivyodokezea hapo juu, umma wote haukuwa tayari kufanya yale ambayo Azimio la Arusha lilipendekeza. kwa hivyo ijapokuwa yaliyosemwa yalikuwa maswala mazuri kidhahania hata wale viongozi ambao walipaswa kushirikiana na wananchi katika kuyafaulisha malengo ya Azimio la Arusha walienda kinyume cha hotuba yao:

Waongozi hao waliokuwa wakiwashawishi
wananchi juu ya ubora wa Azimio hilo
Baadhi yao walionekana walienda kinyume
cha hotuba zao. Walionekana kuhimiza watu
waishi vijijini wakati wao wenyewe
hawakupanda kuhama mijini na mengi mengineyo

Na kwa viongozi kama hawa ambao hawana maadili katika matendo yao mshairi anawashauri ya kuwa :

Kwa mabambo na pepeo msingi hauchimbiki
Kamwe si hivyo vifao, kinyumeni unafiki
Tembe ya maendeleo, nakana haipatiki
Msingi hauchimbiki,kwa mabambo na pepeo.

Itagunduliwa ya kuwa wengi wa viongozi wa kisiasa katika nchi zetu za Kiafrika ni wanafiki na hii imewaweka raia wengi wa Kiafrika katika hali ya dhiki kubwa. Viongozi ambao wanapaswa kuzion-

goza nchi zao kwa namna inayofaa wanakuwa ndio wanaowatumbukiza raia zao motoni kwa kuwa wanayajali tu masilahi yao.

E. Kezilahabi (1974) anasema :

> Wako wapi hoho! waliojidai mabikira?
> Haha! wako wapi waliojidai utakatifu?
> Watu hao wema wapole wako wapi?
> Sifa wanayo heshima hawana
> Ai wako wapi wapenda ujamaa
> Waliokipiga kelele juzi.

Tunaweza kuona kuwa kutokana na mtizamo wa M.M. Amir katika shairi la "msingi" anaelewa ya kuwa ijapokuwa maneno yasemwayo yanaweza kuwa na nia nzuri. Kutoshughulika kikamilifu kwa umma na hasa viongozi, yaliyokusudiwa huenda yasitimizwe. Miaka ilipopita na kukawa hakuna jema lililopatikana jinsi ilivyokuwa imetarajiwa hata Nyerere mwenyewe alikiri kuwa ijapokuwa siasa ya ujamaa ilikuwa nzuri, watekelezaji ndio walioshindwa kufikia matarajio yao kwa sababu hawakuelewa maswala ya kimsingi kuhusu ujamaa. Nchi yenyewe ya Tanzania nayo pia haikuwa tayari kwa siasa ya aina hiyo maanake yo yenyewe ilikuwa masikni.

Tunafikia wakati ambapo tunamkuta mshairi akijikanganya kuhusu msimamo wake wa 'kujitegemea' katika shairi la " kujitegemea " (1977b:16) na " Azimio la Arusha " (1977b:14).

Katika " Azimio la Arusha " anasema ya kuwa :

> Kuombaomba si kwema, Taifa huaibisha
> Wananchi ni kusimama na nyoyo tukazikosha
> Kwamo zinapokingama, ibaki kusawazisha.

Katika shairi la " kujitegemea " M.M. Amir anatoa rai kuwa

nchi yapaswa kujitegemea. Anadai kuwa nchi ikiweza kujitegemea :

` Bepari na wanyonyaji wasalie maguguni '

Tunaloliona katika hili shairi ni maoni ambayo ni muhimu sana kwani nchi nyingi za Kiafrika zinategemea usaidizi wa nchi zilizoendelea. Mashairi haya yalichapishwa zaidi ya miaka kumi na sita iliyopita lakini hali ya mataifa ya kiafrika haijakuwa bora. Badala yake Waafrika wengi wamejikuta katika hali mbaya zaidi. Mshairi anashauri wananchi wajitolee na washirikiane katika kuifanya nchi yao ijitegemee kwani nchi iombaombayo " daima hukaa chini maganja ya mpewaji ".

Hata hivyo jambo ambalo linafanya tufikirie kuwa anajikanganya ni pale ambapo katika shairi la " Nchi iwapo kukutu " (1977 b:18) yuasema kuwa nchi iwapo kukutu hukimbilia mlimbi.

Inaonekana ya kuwa katika hili shairi, mshairi anaanza kutambua ya kuwa si rahisi katika ulimwengu halisi nchi kujitosheleza katika kila haja. Yeye anaonyesha uzalendo alio nao kwa nchi yake ya Tanzania. Anawashauri wananchi wenzake kuwa wajihoji na kutambua kila wanachohitaji na ambacho wanakipata ugenini. Maendeleo ni dhana inayotokea sehemu nyingi, wakati tofauti na kwa namna tofauti. Kwa hivyo nchi zitaendelea kutegemeana. Nchi kama ya Tanzania, si rahisi kwayo kupuuza watalamu wa kigeni kwani ikiwa ina matumaini ya kuendelea hasa katika nyanja za kiufundi basi itabidi tajiri wataalamu wa kigeni ili wawapatie huo ujuzi utakao wawezesha kujitegemea. Na hili si swala la aibu kama anavyosema mwenyewe baadaye :

Hapataki ukinzani, ghera na mafutufutu
Yalikwanzapo zamani, nchi za ng'ambo na mwetu
Si aibu wala zani, izingatie kukutu
Nchi iwapo kukutu, hukimbiliwa mlimbi.

Mtizamo wake wa kizalendo katika shairi la " nchi yetu Tanzania " (1977b:19) anawahimiza wananchi wenzake wajitolee katika kuijenga nchi yao . Mshairi anagundua mambo matatu muhimu ambayo mataifa mengi ya kiafrika yalikusudia kutatua baada ya uhuru. Kulikuwa na swala la ujinga, umaskini na ndwele. Haya maswala mshairi anayazungumzia na kuwasihi wenzake:

Kwa nguvu moja na shime tuutimize muradi

Sote pia tujitume, ni jambo limetubidi
Kwa pole tudemedeme, zitue zetu fuadi
Tusijigeuze ndeme, tukaitwa wakaidi
Tutekeleze muradi, kimbelembele waume.

Siasa ya nchi hushirikisha raia na viongozi na kwa hivyo mshairi anatuonyesha jukumu alilo nalo kiongozi. Anapaswa kuwaelemisha wananchi kuhusu maswala muhimu yanayowakumba kama maadili bora maishani. Mshairi ametuonyesha namna Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanzania alivyoungana na wananchi kwa kuwahimiza washirikiane katika kuijenga nchi yao. Shairi la " Jamhuri " (1977b:15) ni mojawapo ya matokeo ya uongozi bora wa Nyerere. Anapousifia katika shairi la " Mwalimu Julius Nyerere " uk. 13 anaonyesha jinsi alivyo tayari kuifia nchi yake ikibidi. Hii ni sifa moja ya kiongozi mzalendo. Shairi la " Utii " (1977b:22) linazungumzia uraia mwema na ambao unaonyesha wananchi waliowazalendo na ambao wako tayari wakati wote kuitumikia nchi yao.

Kwa maoni yetu, viongozi waadilifu ni wale wanaojitolea kuitumikia nchi zao kwa kila hali. Na tunapozungumzia swala la uzalendo ni lazima tuelewe ya kuwa unawahusu wanasiasa, viongozi na raia. Ni lazima haya makundi yote yajitolee kwa kuweka hatima ya nchi yao mbele kabla ya tamaa zao za kibinafsi. Ni lazima wote wafuate maadili na mbeko za wanajamii.

Mashairi mengine ambayo yanazungumzia hili swala ni pamoja na "Ujamaa" (1977b:21) na "sabasaba" (1977b:20).

## 4:5:0 MAONYO KUHUSU MAOVU YA DUNIA.

Kuna mashairi mengi kuhusu maovu ya wanadamu duniani katika diwani zote mbili. Mshairi kama msanii mwadilifu amejitwika hilo jukumu la kuiboresha jamii kutokana na mifano mingi ya uovu anayoitoa. Kwa kuwatolea waja mawaidha papo hapo anawaonya dhidi ya hayo maovu. Kwa hivyo mshairi amechukua nafasi kubwa katika ushairi wake ya kuwaelemisha wanadamu.

Uovu duniani ni swala ambalo limeshughulikiwa na washairi wengi. Hii ni kwa sababu wanaishi katika jamii iliyasakini kwa uovu na wanazo ithibati. Baadhi yao huandika kutokana na tajriba zao wenyewe.

H.M. Mbega (1984:23) anaonya :

Ulimwengu jifa na kusimangana
Kingiacho ufa hakuingi tena
Kizima kikafaa, hakidumu sana
Walipwao sifa kabisa hakuna.

H. M. Mbega (Ibid) hawaoni watu ambao wana sifa nzuri tu zisizo na doa hata moja. Anaendelea kuwaonya wanadamu kuhusu uovu wa dunia katika shairi la "Dunia" (1984:72) kwa kutahadharisha :

Hii dunia potole, siipende
Nenda nayo polepole, sijipinde
Itakuzushia gole likushinde
Utabakia uole usitende.

Katika (1977b:33) shairi la " Dunia njia panda " mshairi ana maudhui kama haya ya H.M. Mbega (Ibid) kuhusu dunia. Anayaweka hivi:

Dunia njia ya panda, kama nyinyi hamnazo
Aendae akienda, asiende mfululizo
Waume imewashinda tokea zamani hizo
Dunia njia panda, hukanganya wasafiri

Mshairi anaendeleza maudhui yake kwa kusema kuwa kuna njia mbili; kuna ya kivulini na ya pili ni njia duni iliyo na shimo la mateketezo. M.M. amir anahimiza umma kuzibainisha hizi njia mbili wasije wakateketea kwa kuifuata ile njia duni.

Mshairi anawalaumu wanadamu kwa kupotea :

Tumekuliwa na hamu, sahau na mapuuzo
Ile imwagayo damu ndilo letu pendekezo

Ingawa kwa hivi sasa hakukosi vielezo
Na marubani huasa, kwa kemi na matangazo
Hatushiki twajitosa, tukaacha maagizo

Mshairi anawalaumu wanadmau kwa kukataa kufuata maagizo yatolewayo kwao. Wanadamu wengi wanajiingiza katika mambo ambayo yanaielekeza hatima yao katika maangamio.

Akitolea mfano wa viongozi ambao wanawafanyia raia zao maovu M.M. Amir anasema :

Ni ulevi wa kikao, wendapo ukakuvaa
Hunyanyasa wapitao, udugu na zako jamaa
Humtambui mwemao na ajaye wamwambaa
Fungueni makataa uole pombe na cheo.(1977a:54)

Shairi la "mamlaka" (1977b:39) mshairi anaendeleza maovu yafanywayo na wale walioko mamlakani. Wanaonywa ya kuwa madaraka yasiwafanye kufikiria kuwa dunia ni yao. Anawaambia :

Ushikapo madaraka, sione hapo ni basi

Hili ni onyo ambalo ni muhimu sana kwa viongozi wengi ambao husahau kuwa na utu katika matendo yao.Nchi zetu nyingi zimekuwa na viongozi wakatili ambao wamewadhulumu wananchi wao. Afrika, viongozi kama vile Amin aliyeitawala nchi ya Uganda miaka ya sabini aliwahi kuwatesa watu wengi. Lakini sasa hayuko.

Shairi la " Ubadhirifu " (1977a:26-7), mshairi anazishughulikia tabia mbovu za watu ambazo haziendi sambamba na maadili ya jamii.

Mwenda mbiyo mtakavyo, roho zinavyowatuma
Mkapuuza mwenzavyo, kwa kiasi na kupima
Hamjui kama sivyo, mwishowe ni kuatama.

Mshairi anaendelea kuwaonya kuwa hata wale waliokuwa wakijisifu kuwa wao ndio waweza vyote kwa sasa hawapo tena. Wameangamia kabisa. :

Fakani tuwaonao, walokuwa wakivuma
Kwa ari na mali zao, kila jambo kwao jema

Si chochote hivi leo, wasaliye wima wima

Ukweli wa maisha ndio huo hasa. Dunia yataka tahadhari kubwa maanake kama asemavyo A. Nassir katika Hichens :

Suu ulimwengu bahari tesi
Una matumbawe na mangi masi
Aurakibao juwa ni mwasi
Kwa kula khasara ukhasiriye

Maisha yanawaponza wengi ambao wanaiendea kwa kasi. Maisha yataka ujasiri mkubwa.

Katika " Ndwele ya kujipa " uk. 45 wa Malenga wa mrima Mshairi anaendelea kuonya ya kuwa shida maishani mara nyingi humjia tu yule ambaye anayezitaka. Maudhui haya ndiyo yapatikanayo pia katika shairi la " Maisha na matendo " katika Tungo zangu uk.2 ambapo mshairi anaonyesha kuwa ni matendo ya mtu ambayo yataamua yale maisha atakayoishi. Matendo ya watu yanapaswa kuwa mazuri la sivyo maisha yake nayo yatakuwa mabovu. Kwa hivyo ili maisha ya mtu kuwa bora yuapaswa kujiepusha na uovu.

Anasema :

Hata aliye karibu, vivyo nimetafiti
hatoki penye hesabu, yu kati ya mtikati

Katika shairi la " Hatari " (1977a:12), mshairi anaziangalia nyingi za hatari wanadamu wajipatamo kuwa ni wao wenyewe hujipikia kama tulivyoona hapo juu katika "Ndwele ya kujipa " na " Maisha na matendo ". Inavyoeleweka ni kuwa katika jamii kuna wale watakaojikuta katika feli halafu wakaanza kuwalaumu wenzao kwa feli hizo. Mshairi anatuchorea picha inayokubaliana na msemo

kuwa majuto huja baadaye. Katika maisha watu wanajidai kuwa mahodari wakijanata mbele za watu kuwa hawashindiki. M.M. Amir anaonyesha katika diwani zake hadaa za dunia na jinsi zinavyowakanganya wasafiriamo duniani. Mshairi anaelekea kuendeleza falsafa yake kuhusu utala uliomo duniani na jinsi anavyoona bora zaidi kwa waja kuepuka njia mbi. Dunia imejaa fondogoo lakini yeyote atakaye kufaulu maishani inapaswa asiende mfululizo.

Kwa hivyo M.M. Amir anatahadharisha kuwa katika dunia hii aendaye kwa pupa na chapukizo pasi ya kuzichuja njia zake hapati punje ya tija ila hukumbana na visiki kila mahala.

Mashairi mengine mengi yanawaonya wanajamii dhidi ya kufanya matendo ambayo yatawaangamiza. Wanajamii wanapaswa kuelemishwa juu ya maswala muhimu maishani na hapa M.M. Amir amejaribu kadiri alivyoweza kwa kuwatahadharisha kama mshairi mwadilifu.

## 4:6:0 MALEZI.

Diwani zote mbili zinashughulika swala la malezi lakini ni katika diwani ya Tungo zangu ambamo tunapata utenzi unaotuonyesha malezi ya mama wa kambo ambaye anachorwa kuwa mlezi mbaya.

Malezi ya watoto ndiyo msingi wa maisha katika jamii. Malezi ayapatayo mtoto akiwa angali mchanga ndiyomuhimu na ndiyo ambayo humpatanisha na jumuia yake. Wakati huu wa utoto ndio ambao mtu anapoumbika katika ulimwengu mdogo unamzingira.

M. Mnyampala (1965) anasema :

> Malezi kitu cha mbele popote kila mzazi
> Watoto bila malezi ni shamba lisilo mbolea

Kwa kiasi kikubwa tunapata kuwa malezi ya utotoni aghlabu huwaathiri watu katika ukubwa wao. Na watoto wanapokuwa na kuanza kupotokwa kitabia wakati mwingine hili huwa limesababishwa na jinsi alivyolelewa.

Ni haki ya kila mtoto kupatiwa malezi anayohitaji kutoka kwa mzazi wake. Litakuwa jambo baya ikiwa mzazi atawaacha watoto wake katika hali ya ukiwa bila kuwajali ilhali hawana mwingine wa kumtegemea.

Ni haki ya mtoto kuvishwa, kuelemishwa, kulishwa na kupewa mahali pa kulala. Hakuna mwingine aliye na wajibu mkubwa kama huu isipokuwa mzazi kwa mtoto wake.

Mbali na hayo, ili mtoto awe raia mwema wa jamii, ili pia mienendo yake na maisha yake ya baadaye yasiwe mabaya, wazazi wanapaswa daima kutimiza jukumu lao.

Kwa vile fasihi inapaswa kututolea mifano bora ya kuiga ni jukumu la mwandishi yeyote yule kuhakikisha ya kuwa yuko katika mstari wa mbele katika kuwaelemisha wanajamii kuhusu haya masiala muhimu.

M.M. Amir katika shairi la "Ukazi mwema" (9177b:69) anataja mambo muhimu yahitajikayo :

> Mwadilifu duniani, ni achungaye maisha
> Na avhungile za nyumbani.kulisha na kuwavisha

Si kwelemea njiani,wapwamu kunufaisha
Ungejua laitini, maovu husababisha
Ni nani hili mbisha kwa haki na kulingana

Itunze, nafsi yako, uwe kuistawisha
Ulee watoto wako, na mema kuwafundisha
Iwe ni tabia kwako,moyoni kujivalisha
Pindi uonapomwako, ni mambo kuyapotosha
Ni nani hili mbisha, kwa haki na kulingana

Wana wafunze elimu, na dini kuwazindusha
Waje wawe mahakimu, kupandisha ni kushusha
Wahuni na madhalimu, hapa vivyo nakumbusha
Ndiyo wagavi wa sumu, heri nao kujepusha
Ni nani hili mbisha, kwa haki na kulingana

Katika hizi beti tulizozidondoa tunaona namna ambavyo kwa maoni ya mshairi ni muhimu sana kwa maisha ya baadaye ya mtoto. Watakuwa raia waliofaulu maishani kutokana na elimu waliyoipata na watakuwa wahuni na wadhalimu kutokana na malezi waliyoyapata wakiwa wachanga. Malezi mazuri ni mojawapo ya misingi imara kwa raia adili.

Kwa maoni yetu, malezi bora ni yale yanayohakikisha ya kuwa mtoto amepewa maadili yahitajikayo katika jamii. Mtoto anapaswa kufundishwa jinsi ya kuwa raia mwema kulingana na maadili ya jamii yake. Kumnyima mtoto kama haki zake za kimsingi - chakula, mavazi, elimu, mahala pa kulala haipaswi kamwe kuruhusiwa.

Swala hili linaeleweka vile vile tukiangalia jinsi Rehema alivyolelewa na mamake wa kambo katika Nyota ya Rehema. 6

Kwa hivyo mama wa kambo anaonyesha mfano mbaya wa kuigwa ambao hauna hata chembe moja ya ubinadamu (uadilifu).

Rai anayoitoa katika shairi la "Lea Mwema" (1977b:25) kido-

go ni kinyume cha uadilifu. Mzazi yuapaswa kuwalea watoto wake wote na kuwahimiza waishi kwa udugu ili baadaye wawe raia wema. Lakini ikiwa atamkataa na kumdharau yule ambaye haelekei kuzifuata kaida zilizopo hapo atakuwa hatimizi wajibu wake wa uzazi kikamilifu Kama tulivyotaja hapo awali mtoto ana haki ya kulewa kwa hali iliyo safi bila kubaguliwa.

Kwa hivyo mshairi asemapo kuwa :

Uleapo lea mwema, kigego usimlee
Ni mbovu yake hatima, mtupe kando pekee
Mwambae ana tuhuma, kwa mbali apotelee
Ndwele isiyopojaza, si uchimvi kitu gani!

Atakuvutia janga, mashimoni utopee
Usiivumbue kinga, jamii wakuzomee
Ubaki maingainga, tulia nikunenee
Ndwele isiyopojaza,si uchimvi kitu gani

Mlee mwenye huruma, kwa cheko umchekee
Umjaze memamema, ufapo akuombee
Msi uso wa kwinama, pako asisogelee
Ndwele isiyopojaza, si uchimvi kitu gani

Tunapaswa kutahadhari na mawaidha kama haya. Mwandishi hatuambii ni kwa nini huyu mtoto ni mtovu wa nidhamu. Hatuambii ni yapi anayoyaona maovu katika huyo mtoto. Jukumu la mama mzazi lapaswa kuwa la kumlea yule mtoto ili awe raia mwema.Maovu mengi kama tulivyosema yanatokana na misingi mibaya utotoni.

Ikiwa mtizamo wa mshairi ni kama huu basi aidha hana msimamo madhubuti kuhusu malezi au tunaweza kusema kuwa yeye si tofauti na mama wa kambo katika "Utenzi wa mama wa kambo" (1977a:63-82).

Itakuwa si kawaida kwa mzazi kufikiria kuwa mtoto wake atami-

etea jeraha lisilopona badala ya yeye kufikiria vile vile kuwa atampatia mtoto wake jeraha lisiloweza kupona au kumuangamiza kwa kutomkosoa.

"Utenzi wa mama wa kambo" ambao tumeutaja hapo juu unamchora mama wa kambo kama mtu katili asiyejali maisha ya watoto wa mke mwenza au wale ambao mama yao hayuko. Sura yetu ya pili ilipendekeza ya kuwa malezi ya watoto yalikuwa jukumu la jamii yote na wala si wazazi tu. Hata hivyo, katika utenzi huu tunachora picha ya mateso kwa mtoto baba yake aondokapo.

Mshairi anasema kuwa :

Mama wa kambo hasidi
Kwa malezi si mufidi
Apendaye kufaidi
Ampe mwana kulea

Katika macho ya mama wa kambo, mtoto ni mtovu wa nidhamu kweli kweli. Inafikia hata kiwango cha kumchungulia mama wa kambo akiwa msalani. Baba mwana anaporudi kutoka shughuli za kila siku ni uzushi wa namna hii anaoupata kutoka kwa mke wake ambaye pia ni mama wa kambo wa kwa mtoto huyo.

Ni vigumu kukana kuwa siku hizi kuna chembe chembe za unyanyasi wa watoto wanaolelewa mbali na mama zao na hasa wanaojikuta chini ya himaya ya wanawake wa pili. Familia nyingi zinapovurugika kutokana na shida nyingi ambazo zimeletwa na mabadiliko ya kijamii, watoto ndio wanaoteseka.

Mshairi hakutuambia mahala ambapo mama halisi wa huyo mtoto

alipo. Hakutuambia ikiwa alifariki au ikiwa waliachana. Haieleweki vile vile iwapo yupo pahala pengine kama ilivyo kawaida ya wanaume wa kiafrika kuwa na zaidi ya wake wawili, mmoja mjini anapofanya kazi na wengine vijijini. Ikiwa wametalakiana au ikiwa wameachana tu tunaona hali kama ile aizungumziayo **Balisidya** (1987: 38) anaposema ya kuwa :

> Hali mbaya iliyopo sasa baina
> ya wake na bwana zao ndiyo
> inayosababisha malezi mabaya
> ya watoto na matokeo duni
> ambayo ni hali kama hizi. 7
>
> (Tafsiri yetu)

Kwa sababu ya kuchelea hali ya watoto wao wakati ambapo hawako, wanawake wengi huvumilia mateso ya ndoa. Kwa wanawake wengi wa Kiafrika watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa hivyo huwa vigumu kwao kuwaacha. R. Lugano (9189) anasema kuwa :

> Regina anawakilisha wanawake wengi
> katika jamii za kiafrika ambao wanavumilia
> mateso mengi kutoka kwa bwana zao kwa
> sababu ya watoto wao. Wanachelea kwamba
> wakiondoka, bwana anaweza kuleta mama wa
> kambo ambaye atawatesa watoto wao. Vile
> vile inawezekana kuwa wanaendelea kukaa
> chini ya dhuluma ya bwana zao kwa kukosa
> mahali pa kwenda. 8

Balisidya (Ibid:30) anasema kuwa tatizo lipo katika utunzi wa watoto kutokana na sheria na mila. Kwamba mila inamruhusu mwanamume kuwatunza watoto baada ya talaka ilhali sheria wakati mwingine humruhusu mwanamke kuwatunza watoto wake.

Inasikitisha kwa hivyo ikiwa ni kweli ya kuwa huyu mama wa kambo anaweza kumnyima mtoto haki zake za kimsingi.

Aweza kuona kunguni
Wabumao mvunguni
Akadai hawaoni
Hali mwana aumia

Nguo zaweza chafuka
Zikatia na kunuka
Mama hajazikumbuka
Kwamba bora kuzifua

M.M. Amir anamuona mama wa kambo huyu kuwa haini na ambaye atajitia ni mzuri sana bwanake akiwapo hata amuulize mtoto "Leo mwana mbona huli? Kula upate afia". Kwa M.M. Amir huu ni unafiki na inaumiza sana ikiwa wakati mwingine wakiwa wamebakia peke yao nyumbani mtoto amshtakiapo hali yake ya njaa yeye huwa hamtilii maanani hata ikiwa amekipika hicho chakula.

Ikiwa mtoto anateswa kutokana na uhusiano mbaya katika nyumba basi tuna sababu nzuri za kumlaumu huyu mama wa kambo maanake mtoto hana hatia.

"Utenzi wa mama wa kambo" kwa namna fulani unadhihirisha taasubi za kiume kwa upande wa mshairi kwani yeye haonyeshi ni kwa nini baba mtoto asilaumiwe kwa taabu azipatazo huyu mtoto. Baba hamuulizi mtoto wake hali yake. Yeye anaambiwa tu vile mtoto anavyofanya mambo yasiyo na mbeko kama kumchungulia mamake akiwa msalani. Ni jukumu la wazazi wote kushirikiana katika malezi ya watoto. Huenda ni mume katika hiyo familia ambaye amemletea huyo mtoto hizo shida zote kwa kumfukuza mama halisi wa huyo mtoto. Kwa hivyo kwa mshairi kumchora mama wa kambo kuwa ndiye mwenye makosa tunafikiri mshairi amelitizama hili swala kutokana na taasubi za kiume badala ya kuliangalia hili swala kwa upana wake.

4:7:0 MAJAALIWA.

Baadhi ya mashairi katika diwani hizi mbili yanazungumzia dhana ya majaaliwa. Binadamu anaishi humu duniani kwa mapenzi ya karima. Yale yatufikiayo ni yale ambayo yamekwisha kupangwa na Mungu. Huu ndio mtizamo unaochukuliwa na wale wanaoamini katika majaaliwa. Mtazamo kama huu hata hivyo hutofautiana na ule wa wa-namarksi wanaoamini ya kuwa ni binadamu ambaye anaweza kuleta ma-pinduzi ili kuyaboresha maisha au hali yake.

Ijapokuwa kuna ukweli kaatika kauli hili, kuna mambo mengine ambayo inabidi yapingwe hasa wapinzani wa majaaliwa wanaposema ya kuwa kuamini katika majaaliwa ni namna moja ya kuwadhulumu wanaj-amii. Wanaoamini katika majaaliwa wanafahamu ya kuwa kuna baadhi ya vitu ambavyo binadamu hana uwezo wowote kwavyo na tunakubal-iana nao katika baadhi ya sehemu ambazo haimkiniki kuna binadamu yeyote anayeweza kubadili. Maswala kama kifo ni amri ya Mungu.

M.M. Amir analitizama swala la unyonge kuwa la kimajaaliwa na kuwa hapana lolote binadamu analoweza kufanya kuirekebisha hali hiyo. Katika (1977a:13) anasema :

> Miuja ya kilimwengu <u>aliyoumba karima</u>
> Ni mafungu kwa mafungu, ni wapi ilipokoma
> Kama si kwako ni kwangu hufyonza damu na nyama
> <u>Ni kama huu unyonge</u> si senene kitu gani
> (Msisitizo wetu).

Mshairi anaelekea kudhihirisha kuamini kwake katika majaaliwa na kuikuza hii dhana. Katika shairi la "Kipato na ukata" (1977b: 35) anasema :

Jishike uvitawalevina kileo na tata
Ishi navyo pole pole kwa usiri na kunyata
Hujui lipi keshole, nyuma litalifuata.

Katika hili shairi binadamu anachorwa kuwa kiumbe ambaye hawezikujua jinsi kesho yake itakavyokuwa. Hana uwezo maanake Mungu wake tu anayeweza kufahamu hali yake ya kesho.

Katika shairi la "Kuvundikiwa" mshairi anaonyesha namna pato lilivyo bahati tu. Kwa binadamu yeyote kuwa na pato hiyo ni bahati na sibu tu na kwa hivyo chochote binadamu alicho nacho ashauriwaasijidai nacho. Si ajabu kumpata yule aliye nacho akikosa na yule ambaye hana akipewa :

Dunia humgeuza mja pasi kawilio
Nuru akaona giza, giza likawa mgao
Tonge angalitimiza asijue kitoweo
Si mageni si ya leo, wangapi huvundikiwa
(1977b:60).

Katika haya mawazo tunaona muoano mkubwa na ya S. Robert (9168) anaposema kuwa :

Bahati na julikana
Kwa sifa na utukufu
Humfanya bira sana
Mtu aliye dhaifu
Natukuze na majini
Duni kuwa maarufu
Mwenye macho kama hana
Bahati huwa kipofu.

Katika "Takidiri" (1977a:15) M.M. Amir anaonyesha namna ilivyo ngoma kuibadili takidiri. Anasema :

Hata kwa rupia, haina budi kutimu
Ishikapo takidiri,haina budi kutimu

Kwa takidiri hapana handaki inayoweza kumstiri mja kwani yanatokana na yule ambaye anaaminika kuwa na uwezo kushinda viumbe vyote duniani. Katika utamaduni wa watu wengi yale mabaya na majanga yawapatayo watu hutizamwa katika mkabala wa kimajaaliwa. kwa hivyo mara nyingi wanajamii huhimizwa kufanya yale yanayowapaswa kwa mujibu wa Mbeko za jamii husika.

Aghalabu hali wanamojikuta wanadamu, ziwe za heri au za taabu huwa ni kwa mapenzi ya Mungu. Inaaminika kuwa anayewapa wale wengineriziki au mali ndiye anayewapa wale wengine umasikini- na kutokana na hii wale walionavyo mara nyingi hutahadharishwa ya kuwa mpanda ngazi hushuka na inakuwa ni njia mojawapo ya kuwapa wanajamii matumaini katika kesho yao.

Jambo lingine kama tulivyodokezea ambalo M.M. Amir anaendeleeza ni kule kutojua kile kitakachotokea. Binadamu anakuwa kiumbe ambaye hawezi kubashiri litakalotokea. Na huu unakuwa mfano mzuri hasa tunapotizama teneti za majaaliwa. Ni kwamba ikiwa katika hali fulani lilikuwa linatarajiwa jambo halafu lisitokee kwa namna ilivyotarajiwa ni sababu za kidakidiri zinazotolewa kutetea hali hiyo. Anaendelea kusema :

Ichomapo haitoki, pesi haina usiri
Haichagui rafiki, Diwani wala waziri
Huzinga kama fuluki hupiga ikaathiri
Ishikapo takidiri haina budi kutimu

M.M. Amir katika " Makiwani" (1977b:64) anatoa sababu za kimajaaliwa kwa kifo. Katika kuwaliwaza waliofiwa anasema :

Acha sifanye matungu, na kukithiri kilio

<u>Kufa amri ya Mungu</u>, wengi kuzimu wendao
Kila mtu anafungo, haijawa makulio

Wakristo huweza kuwaliwaza waliofiwa kwa kuwakumbusha ya kuwa masihi alishinda kifo na kwa hivyo wasilie wakati mmoja wao anapowaacha kwa sababu maisha ya duniani si matamu kuliko yale ya baada ya kifo cha mwili. Katika hali kama hii wao huhimizwa kuzisafisha roho zao ili hiyo siku ifikapo wawe wasafi kiroho. S.Robert (Ibid) anazungumzia maswala kama haya anapoitaja siku ya watenzi wote.

M.M. Amir anaendelea kusema :

Yu wapi asiye zamu roho dunia si yao
Kutangulia Adamu na mitume wengineo
Nasi imetulazimu kufumba macho kamao.

Mungu ametusaliti, wanyonge na wenye vyeo
Tulio juu ya uti wake na waume wao
Yatufikie mauti, pasiwe asiliyeo

Inakuwa rahisi kwa wanajamii kusadiki ya kuwa binadamu hana uwezo dhidi ya mipango ya Mungu. Mwandishi anawataja mitume, wenye vyeo na wengine wengi watukuka. Hapa anaonyesha kuwa ule utajiri tunaohodhi na kuwanyanyasa wenzetu hautatufaa tufapo ikiwa matendo yetu hayakuwa mazuri. Mali hiyo yote itaachwa watu wakiozeana ardhini. Hata madaktari wenyewe wakati huo ufikapo ni nadra kuepuka kifo.

## 4:8:0 MAPENZI NA SWALA LA UNYUMBA .

Mashairi yanayopatikana katika sura hii yanajadili swala la



UNIVERSITY OF NAIROBI

uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume. Ni uhusiano ambao unaweza kuwa wa nje ya unyumba au hao watu wakiwa wameoana.

Swala la unyumba au mapenzi limezungumziwa na waandishi wengi kwani ni kipengee muhimu cha jamii. Ni swala linalohusu mtu yeyote katika jamii. M.M. Amir analitalii hili swala kwa kuangalia baadhi ya mambo muhimu yanayoweza kuukuza uhusiano huu na yale mambo ambayo ni hatari kwa uhusiano pia.

Mshairi anataja uvumilivu kuwa kitu muhimu katika kufanikisha uhusiano. Ili watu wawili kuishi pamoja si lazima wawe kabila moja, umri sawa, kufu sawa. La! Wanapokubaliana kukaa pamoja ndipo panakuwa na haja ya kuvumiliana kwani hakuna binadamu ambaye hana upungufu wa aina moja au nyingine. Shairi la "Wenzano" (1977b:70-1) linataja haya mambo muhimu :

> Kwenzana si kwa vimo, vya wawili kulingana
> Kwenzana siyo kwa sura, zenu kumithiliana
> Na wala kwenzana si kwa rangi bali ni tabia
> kuwa sawa.

Kwa maoni yetu, watu wataweza kuelewana na kuishi kwa furaha ikiwa wataweza kuelewa upungufu wao na kujaribu kusawazisha hizo tofauti walizo nazo kwa namna ya kuvumiliana. Ikiwa tofauti za kitabia haziwezi kuvumilika hakuna jingine linaloweza kufanywa hata kama msichana ni malaika.

Shairi la "Kitumiye kwa marefu" (9177a:18) linaonyesha umuhimu wa kumuelewa mwenzako barabara kabla ya kufikia uamuzi wa kusema kuwa ni mchumba mzuri. Anaweza kuwa na sifa nzuri za kijuu

juu lakini yapaswa kuchunguzwa kwa muda mrefu. Mshairi anasema :

Suraye pia ni nzuri, mfano wa zamzama
Si chumvi wala sukari, kwa kati yamesimama
(lakini) Tumia sirudi nyuma, ukijuwa viinivye

Anamalizia shairi lake kwa kuonya kuwa :

Chochote kwa siku haba, ndaniye nimetizama
Hupati yake nasaba, nimezingatia ama
Ziba masikio ziba, ujue kulipokoma.

Mambo muhimu kama haya yakichunguzwa mambo yangali mabichi. Mitafamku ipatikanyo katika ndoa nyingi huenda ikaepukika. Hali zitokeazo baadaye ambazo zinafanya maisha kuwa magumu sio kwa wahusika wale wawili tu bali kwa watoto na jamii kwa jumla, zinaweza kupunguka.

Tunaona jinsi anavyochora picha mbaya ya mwanamke ambaye anachelea atamharibia jina. Katika shairi la "Hawaa" (1977a:48) Mshairi anasema :

Hawaa simpe mwako, zingaumbwa na ghilibi
Naelewa utokako, makeziyo na nasaba
Hutanipa masumbuko, haondokea msiba
Hawaa shika adabu nachelea mwisho wangu.

Shairi la "Bao la namu" (1977b:74) Mshairi anatuonyesha matendo maovu ya mwanamke ambaye haiheshimu ndoa yake. Kwa kiasi kikubwa tunaona hali ya umalaya ikichorwa.

Nakuuzakwa kikao, mamboyo yamenifika
Wenyeji na wapitao, daima kukuzunguka
Wakakidhi haja zao, papo umetambarika.

Jinsi mwanamke huyu anavyosawiriwa inatufanya tuhisi ya kuwa

hana chembe ya Mbeko hata moja. Hii ni kwa sababu ikiwa yeyote atakayemwendea atatoka huko akiwa ameridhika kiuchu basi hapana haja ya yeye kuwa rafiki au mke wa mtu bali analistahili hilo jina la kahaba.

Jambo ambalo hatuelewi kutikana na shairi hili ni chanzo cha hiyo tabia mbaya. Hatuambiwi upande wa mwanamume mwenyewe. Hatuambiwi huyo mwanamume huwa ameenda wapi wakati haya yote yakifanyika. Wanawake wengi wananyimwa mapenzi na waume zao na katika hali kama hii inakuwa vigumu kwa mwanamke kuvumilia zaidi. Wanawake wengine huenda wakavumilia tu kama tuonavyo katika "Kipi kisicho mwenza?" (1977b:36) ambapo anaonyesha vile watu huzoeana : "Giza kazoea popo, kwa chumo hanadhihaka, umkutapo alipo, popo amechangamka"

Kwa hivyo ikiwa tutachukua mwanamke ambaye ijapokuwa bwanake anamtesa na anaishi kwa uchungu itakuwa ni kuwa yeye ni mvumilivu, hamnachui mumewe:

> Maji ya chumvi samaki, wa baharini hukunjuka
> Huishi humo hatoki, huzama na kuibuka.

Shairi la " Msuka kamba motoni" (1977b:43) linatuswiria picha ya mwanamume anayenyonywa na mwanamke ambaye hana mapenzi kwake ijapokuwa huyo bwana anateseka kila siku kwa ajili yake. Mshairi anasema kuwa huyu mwanamke furaha yake ni pale tu apewapo au atendewapo: mara tu baada ya siku mbili au tatu huwa amekwisha kuyasahau kuyatupa yote aliyotendewa. Hili ni jambo lifanyikalo lakini Mshairi anaandika akiwa na chembe za kitaasubi maanake

haonyeshi vile upande ule mwingine ulivyo hasa tukizingatia shairi la "Bao la namu" uk. 74.

Hatimaye katika baadhi ya mashairi yake, Mshairi anawashauri wasomaji wake kuwa na mchumba mmoja na kuziheshimu ndoa au uhusiano wao.

Haya anayaeleza katika "Ushikwapo shikamana" (1977a:22),"Penda wote amini wachache" (1977a:26), "ndimi nachaye viwili" (1977 a:32), "Waucha mkekao" (1977a:61).

4:9:0 HITIMISHO .

Imetudhihirikia wazi wazi kuwa katika hii sura ndipo Mshairi ameshughulikia masiala muhimu maishani. M.M. Amir ameweza kutalii sehemu mbalimbali za jamii ambazo ni muhimu sana katika maisha ya mwanadamu wote.

Kutokana na utafiti wetu, Mshairi ameisawiri hali ya uovu ambayo kwa bahati mbaya yaelekea kuwa matokeo ya wanadamu wenyewe. Ijapokuwa baadhi ya shida zipatikanazo katika jamii zimeonyeshwa kuwa matokeo ya majaaliwa, kwa kiasi kikubwa M.M. Amir anaonyesha ya kwamba wanajamii wenyewe ndio wajiingizao katika vitendo ambavyo huwapotosha na kuwaletea huzuni mwingi.

Kwa maoni yetu tunaonelea ya kwamba diwani mbili za **Tungo Zangu** na **Malenga wa mrima** zimejikita zaidi katika kuwaelimisha na kuwaonya wanajamii kuhusu masiala muhimu maishani.

Mshairi amechukua nafasi ya mzazi, mwalimu, kiongozi na raia katika kuiangalia jamii yake.

**TANBIHI.**

1. Tazama J. Adeola (1975:150)
2. " A. Mazrui (1988)
3. " T.A. Mvungi (1985)
4. " G.B. Mungania (1986)
5. " Wamitila (1992)
6. " M.L.N Balisidya (1987)
7. " R. Lugano (1989).

SURA YA TANO.

## 5:1:0 HITIMISHO.

Tunaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba diwani za M. M Amir ambazo tumekuwa tukishughulikia zimezungumzia hali halisi ya kijamii hasa ya Afrika. Tukichukulia kwa mfano Utenzi wa uhuru wa Tanganyika tunaona kuwa humu Mshairi amejaribu kueleza hali ilivyokuwa siku za awali wakoloni walipokuja na kuvuruga hali "tulivu" zilizokuwepo miongoni mwa Waafrika wengi.

Hata hivyo kabla ya kuyaingilia maudhui hayo katika diwani za M.M. Amir, tuliziwekea kazi zake misingi ya kuhakikia katika sura ya pili ambayo iliyatalii mambo ya kijumla lakini ambayo yalikuwa muhimu kwa sura zilizofuata.

Katika sura ya nne tuliweza kubainisha yale yaliyotokea baada ya ukoloni. Hapa tuliweza kuchunguza jukumu la Msanii muadilifu na mchango wake katika kuleta na kukuza mbeko zinazotakikana katika jamii. Ilitubainikia ya kwamba M.M. Amir alikuwa amekumbana na uozo mwingi katika jamii na kwa hivyo kama Mwanambeko akapania kuiboresha jamii yake kupitia mashairi yaliyomo katika diwani zake mbili - **Tungo zangu** na **Malenga wa Mrima** ambayo yana mafunzo mengi.

Katika sura ya tatu tuliweza kuona mateso ambayo Waafrika walipata hasa chini ya Wajerumani na Waarabu. Waarabu waliwatesa



UNIVERSITY OF NAIROBI

sana Waafrika wakati wa biashara ya utumwa na Wajerumani nao waliwanyanyasa sana Waafrika wakati wa utawala wao wa Kikoloni. Kuhusu haya maswala muhimu ilitujuzia ya kuwa M.M. Amir alifaulu kupitia ushahidi wa kihistoria kuziamsha hisia za hadhira yake. Inawafanya wasomaji wake ambao nchi zao zilitawaliwa na wakoloni na vile vile nchi zao kuhusishwa na biashara ya utumwa na kuelewa malengo ya wakoloni na Waarabu. Tumeweza kubainisha ya kuwa haya makundi yote ya madhulumu yalikuwa kwa manufaa yao na wala sio kwa Waafrika wote hata wale waliotumiwa.

Nchi nyingi za Afrika zilitawaliwa kikoloni. Kodi walizotozwa ziliwataabisha na kama asemavyo D.M. Rosenberg (1991:15) akishughulika swala la kodi kwa Waibo kule Nigeria, anataja kuwa Waibo hawakuelewa ni kwa nini mtu aliyekuwa huru alipaswa kulipa kodi kwa ajili ya shamba la Miungu. Waibo waliona kodi kuwa kitu kilicholetwa kuwaua. Anaendelea kusema kuwa ni kwa sababu ya kodi ndipo kukawa na zogo la wanawake mnamo mwaka wa 1929.

Rosenberg (Ibid) akimnukulu Afigbo anaongezea kuwa :

> The riot was an assertion by the people that no cultural group, no matter what high notions it might have about its civilization, could be good enough to rule another cultural group. The British were therefore invited to go to their country so that the people would resume control of their own destiny. 1

Katika muktadha wa Watanganyika kodi na kazi za kulazimishwa zilileta vita kama vile tulivyovishughulikia vya maji maji mnamo mwaka wa 1905-7. M.M. Amir ameweza kutuonyesha ya kwamba Waafrika walipofika mwisho wa kustahimili kwa walikata shauri kupiga-

na vita na vile vile kutumia mbinu za kushawishi ili wapewe uhuru wao.

C. Achebe (1962:161) yuasema :

> Ni lazima tupigane ili tuwafukuze hawa watu kutoka ardhi yetu." ... Watu wetu wenyewe na vijana wetu wameungana na adui. Wamejiunga na dini yake na wanasaidia katika kuendeleza serikali yake. Ikiwa tutataka kuwafukuza wazungu kutoka Umuofia halitakuwa jambo gumu kwani ni wawili tu. Lakini je, itakuwaje kuhusu hawa watu wetu ambao wanafuata mienendo na wamepewa madaraka ?

Maneno ya C. Achebe (Ibid) yana mashiko sana. Kulikuwa na Waafrika wasaliti na vibaraka wa wakoloni. Ijapokuwa Waafrika wengi waliteseka kulikuweko na wale waliokuwa radhi kuwasaliti ndugu zao Waafrika. Katika utafiti wetu, haya yamejitokeza hasa katika **utenzi wa uhuru wa Tanganyika** ambamo M.M. Amir anatuonyesha wale watu waliounda vyama kukipinga chama cha TANU wakati walipotakikana kuungana ili wawafukuze wakoloni. Kuna wale waliziasi tamaduni zao ili kuufuata utamaduni wa mkoloni. Je hawa wangefanywaje ? Hilo ndilo swali aliulizalo Achebe. Katika shairi la "Kizamani" tunaona hali hii ya ukengeushi:

> Simo hii 'kizamani' sasa ndipo inamizi
> Yacheza ngoma ugani, kwa majasho na mititizi
> Achuchukaye mwendoni,angiamo mwenye shazi
> Ibilisi kawahozi mwabinia kizamani.

Ni dhahiri ya kwamba kulingana na vile maudhui yake yanavyojitokeza, vipindi vya kihistoria vinaonyesha jinsi jamii ya M.M. Amir ilivyobadilika kulingana na wakati. Miaka ya sabini ambamo diwani za **Tungo zangu** na **Malenga wa mrima** zilichapishwa ndio wa-

kati ambapo jamii nyingi za Afrika mashariki zilkuwa zikionyesha athiri nyingi ambazo zilikuwa zimeachwa na wakoloni. Kwa matokeo ya mvurugo wa utamaduni wa Kiafrika ndio baadhi ya maswala ambayo M.M. Amir ameshughulikia katika hizo diwani mbili tulizotaja.

Kutokana na diwani zote tatu tunaweza kuibaini falsafa ya Mshairi kuhusu maisha. Yaelekea kuwa M.M. Amir kama Shaaban Robert anayaona maisha kuwa yamejaa uovu. Hata hivyo kwa kuchukua uadhifa wa kuielemisha na kuionya jamii, M.M. Amir anaonyesha matumaini yake katika kuiboresha jamii. Anaamini ya kuwa wanajamii wakiyarudia maadili ya jamii kutakuwa na maisha yaliyo na furaha. M.M. Amir anachukua huu mtizamo kwa sababu anaamini ya kuwa matatizo mengi yanasababishwa na wanadamu wenyewe. Tumeweza kubainisha kuwa kila mwanadamu ana nafasi ya kuwa na ufanisi duniani.

Mojawapo ya haipothesia zetu ni kuwa Mshairi ni mwanadamu anayeamini katika majaaliwa. Kutokana na utafiti wetu tunafikiria ya kwamba M.M. Amir anaamini yakuwa ufanisi na ufakera wa wanadamu ni amri ya Mungu. Kuhusu kifo Mshairi anatoa wazo kama hili. Kwa hivyo kwa kiasi kikubwa Mshairi anaamini katika majaaliwa. Dhana ya majaaliwa inahusiana sana na dai kuwa Mshairi ameathiriwa na dini ya Kiislamu. Uchunguzi wetu unaonyesha ya kuwa katika baadhi ya masiala ayashughulikiayo, M.M. Amir anaandika na mkabala wake wa kidini. Mbali na dini ya Kiislamu kumuathiri Mshairi, imetubainikia ya kuwa anaonyesha vile vile mtizamo wa kiujamaa.

M.M. Amir ameweza vile vile kuyashughulikia masiala ya kisiasa kama mzalendo lakini anaonyesha udhaifu wa kutoweza kuwakosoa viongozi wa chama chake. Wengine wanaweza kudai kuwa M.M. Amir ameonyesha uzalendo wake kwa sababu ya viongozi waliokuwepo na chama walichokuwemo. Kuna uwezekano ya kuwa Imani yake ilikuwa katika baadhi ya viongozi na hasa wale wa chama cha TANU. Tukimrejea A. Gibbe ambaye anasisitiza ya kuwa washairi hawapaswi kuimba kutukuza tu bali waelemishe na kuwakosoa viongozi wao, tunagundua ya kuwa kwa kiasi fulani M.M. Amir hakuangalia upande wote. Aliegemea tu upande mmoja wa Julius Nyerere kama Rais wa Tanganyika na chama cha TANU.

Baadhi ya mashairi ya M. M. Amir yametuonyesha kuwa ulifikia wakati fulani akabadili msimamo wake kuhusu nchi yake ya Tanganyika kujitegemea. Mshairi yaelekea aligundua ya kuwa si rahisi kwa nchi yeyote kujitosheleza hasa nchi maskini kama ya Tanganyika wakati ule.

Haipothesia yetu iliyodai ya kuwa Mshairi ana taasubi za kiume inapata mashika katika diwani ya **Tungo zangu** ambamo Mshairi anamlaumu mama wa kambo bila kuchunguza swala la malezi kwa upana wake. Aidha katika baadhi ya mashairi, M.M. Amir anamsawiri mwanamke kuwa ndiye muovu tu. Anamlaumu kuwa yeye ni malaya, kiumbe asiyekuwa na shukrani bila kuuchunguza upande wa mume.

Kwa jumla M.M. Amir ameyashughulikia maswala muhimu katika jamii kwa kuturudisha nyuma ili tufahamu yaliyotokea wakati wa ukoloni. Yale ambayo yanashughulikiwa katika diwani za **Tungo zangu** na **Malenga wa Mrima** ni maswala muhimu yanayoonyesha uozo

katika jamii hata sasa.

Tunapendekeza utafiti uendelee kufanywa hasa ule unaoweza kumlinganisha mshairi na wengine wa kimapokeo. Aidha utafiti kuhusu fani yake unaweza kufanywa kwa sababu hakuna kazi ya kihakiki inayoweza kuwa kamilifu.

**Tanbihi :**

1. Katika Muaka (Mh.) (1991)

## MAREJEO :


Abdalla, A (1973) **Sauti ya Dhiki.** Nairobi, O.U.P

Abdulaziz, M.H. (1979) **MUYAKA 19th century Swahili Popular Poetry,** Nairobi, K.L.B.

Amir, M.M. (1967) **Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika**, Dar-es-Salaam, N.P.C.

(1977) **Tungo Zangu**, Dar-es-Salaam, T.P.H.

(1977) **Malenga wa Mrima**, Dar-es-Salaam, O.U.P.

Balisidya, M.L.N (1987) " The construction of Sex and Gender Roles in Penina Mhando's Plays " Katika **KISWAHILI** juzuu 54/1 & 54/2 Dar-es-Salaam, TUKI.

Davies, R.C na Finkie, L (1989) **Literary Criticism and Theory: The Greeks to the Present,** New York. Longman.

Dorsch, T.S (Mfr) (1965) **Classical Literary Criticism.** England, Penguin Books.

Fanon, F (1967) **The Wretched of the Earth.** London, Pelican Books.

(1970) **Black Skin White Masks**, Frogmore. Paladin.

Gakwandi, A.S. (1977) **The Novel and Contemporary Experience in Africa**, London, Heinemann.

Gibbe, A.G (1978) "Fasihi na Jamii. Baadhi ya Washairi wa Kiswahili 1960-1977" katika **KISWAHILI**, juzuu 48/1, Dar-es-Salaam, TUKI.

Gwassa, G.C.K (1967) **Records of the Maji Maji Rising Part one**, Dar-es-Salaam, E.A.L.B.

Halimoja, Y. (1977) **Historia ya Masasi**, Dar-es-Salaam, E.A.L.B.

Hough, G. (1966) **An Essay on Criticism.** England, Duckworth.

Kaniki, M.H.Y. (1974) " The Party of Independence and National Consolidation" Katika

**Towards Ujamaa**, Dar-es-Salaam.E.A.L.B.

Kaplan, C (1986) **Criticism. The major Statements**. N. York, St. Martins Press.

Kayongo-Malle, D. (1984) **The Sociology of the African Family**, London, Longman.

Kezilahabi, E. (1971) **Rosa Mistika**. Nairobi, K.L.B.
(1976) **Ushairi wa Shaaban Robert**, Nairobi, K.L.B.

Mazrui, A. (1988) **Chembe cha Moyo**, Nairobi, Heinemann.

Mbiti, J. (1969) **African Religions and Philosophy**, London, Heinemann.

Mlacha, S.A.K. (1988) "The Effects of Foreign Cultures to the Younger Generation. A case study of Kezilahabi's three Novels" Katika **KISWAHILI** juzuu 55/1 & 55/2, Dar-es-Salaam, TUKI.

Mnkondo, ...et al (1971) **Tanzania Kabla na Baada ya Uhuru**, Dar-es-Salaam, E.A.L.B.

Mnyampala, M. (1965) **Waadhi wa Ushairi**, Dar-es-Salaam,E.A.L.B

Mohamed, S.A. (1980) **Sikate Tamaa**, Nairobi, Longman.

Muaka, J.A. (Mh) (1991) **UFAHAMU: The journal of the African Activist Association** Vol.XIX no.1 Los Angeles, UCLA.

Mulokozi, M.M. (1975) "Revolution and Reaction in Swahili Poetry". Katika **KISWAHILI** juzuu 45/2, Dar-es-Salaam, TUKI.

Mungania,G.B (1986) "Maudhui Mbalimbali Katika Ushairi wa Mathias E. Mnyampala" **Tasnifu** ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi.Haijachapishwa.

Mvungi, T.A (1988) **Chungu Tamu**, Dar-es-Salaam, T.P.H.

Mwakipesile, J (1974) "Taratibuzetu za maisha'.Katika **Historia fupi ya Utamaduni wa Mtanzania**. Dar-es Salaam, Foundation Books.

Omari, C.K (1980) **Urithi wa Utamaduni wetu**, Dar-es-Salaam T.P.H.

Peck, J. na Coyle, M (1984) **Literary Terms and Criticism**, London, Macmillan Education.

Robert, S. (1967) **Masomo Yenye Adili**, Dar-es-Salaam, Nelson and Sons Ltd.

(1967) **Utenzi wa vita vya uhuru**, Nairobi, O.U.P

Senkoro, F.E.M.K. (1987) **Fasihi na Jamii**, Dar-es-Salaam, Press and Publicity centre Ltd.

Shariff, I.N. (1988) **Tungo Zetu. Msingi wa Mashairi na Tungo Nyinginezo**, Trenton, The Red Sea Press.

Topan, F.M (Mh) (1971) **Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili**, Nairobi, O.U.P.

Wamitila, K.W. (1992) "Maudhui katika Ushairi wa K.K.Kahigi na M.M.Mulokozi " Tasnifu ya M.A chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

Wellek, R. (1973) **Theory of Literature**, N.York, Penguin.